# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 22 Mei, 2019

*(Bunge lilianza saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, bado tupo kwenye Mkutano wetu wa Kumi na Tano, na leo ni Kikao cha Thelathini na Tatu.

Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:** Kiapo cha Uaminifu.

**SPIKA:** Kiapo cha Uaminifu. *(Makofi)*

## KIAPO CHA UAMINIFU

Mhe. Dkt. John D. Pallangyo

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu!

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASINI NA UTALII:-**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Constatine John Kanyasu; Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Tunaanza na TAMISEMI, swali la kwanza ni la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kwa niaba yake Mheshimiwa Ritta Kabati tafadhali.

Na. 271

**Kukarabati Miundombinu ya Shule za Msingi – Mufindi Kusini**

**MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y MHE. MENDRAD L. KIGOLA)** aliuliza:-

Miundombinu ya shule nyingi za msingi katika Jimbo la Mufindi Kusini ni chakavu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati miundombinu ya shule hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto kubwa zinazoikabili Sekta ya Elimu hapa Nchini ni uhaba na uchakavu wa miundombinu ya shule ikiwemo nyumba za

walimu, vyumba vya madarasa pamoja na vyoo. Serikali kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu *(Education for Results – EP4R)* inaweka kipaumbelea na kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu hiyo ya elimu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi imepokea jumla ya shilingi milioni 223.2 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Shule za Msingi Kilolo na Makalala. Shule ya Msingi Kilolo ilipokea jumla ya shilingi milioni 136.6 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu, ujenzi wa madarasa manne na ujenzi wa matundu sita ya vyoo na Shule ya Msingi Makalala imepokea jumla ya shilingi miloni 86.6 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na matundu sita ya vyoo. Serikali itaendelea kutoa fedha kwa kadri ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu ya msingi kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, nilikuona swali la nyongeza.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali ya nyongeza. Kwa kuwa Mkoa wetu wa Iringa ni mkoa ambao kwa kweli una baridi sana na wanafunzi wengi wamekuwa wakisoma kwa shida kutokan ana uchakavu mkubwa uliopo wa shule zetu za msingi. Na shule zetu nyingi za msingi toka zimejengwa hazijawahi kukarabatiwa, nishukuru baadhi ya wazazi wa Mkoa wa Iringa wamekuwa wakisaidia katika ukarabati na Mheshimiwa Waziri nafikiri alikuja akaona baadhi ya shule ambazo tumeanza kuzikarabati.

Je, Serikali iko tayari sasa kusaidia angalau kidogo baadhi ya shule ule ukarabati ambao wazazi wanafanya na Serikali ikasaidia japo kidogo ili tuweze kukarabati shule nyingi za Iringa?

Mheshimiwa Spika, swali letu la pili, kwa kuwa pia sambamba na hilo, shule nyingi za sekondari maabara nyingi

hazijakamilika na wanafunzi wengi sana wamekuwa wakifanya mitihani bila kusoma vizuri kwa sababu ya kutomalizika kwa maabara.

Je, Serikali sasa inasemaje kuhusiana na kumalizia maabara ambazo bado hazijaisha ili wanafunzi wetu wa Iringa waweze kusoma na kufaulu vizuri?

**SPIKA:** Ahsante sana, majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya dada yangu, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mkoa wa Iringa pamoja na mikoa mingine ina changamoto hizo za uchakavu wa miundombinu. Lakini naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu safari zangu za Mkoani Iringa tulivyofika pale katika Manispaa ya Iringa aliienda kunionesha akiwa na timu yake pale, miongoni mwa shule ambazo yeye mwenyewe na wadau wenzake waliweza kushiriki katika ukarabati.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, lengo la Serikali yetu ni kuhakikisha tunafanya kila liwezekanalo kufanya ukarabati wa shule hizi ndiyo maana juzijuzi Serikali yetu imetoa zaidi ya shilingi bilioni 35.5 kwa lengo la kuhakikisha kwamba tunaongeza nguvukazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kubadilisha miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, nikiri wazi kwamba katika suala zima la maabara kweli kuna changamoo kubwa, kama lengo la Serikali lilivyo kwamba *agenda* yetu kwa mfano katika bajeti ya mwaka 2019/2020 ambayo nimeiwasilisha hapa Bungeni siku chache zilizopita,

zaidi ya shilingi bilioni 90.08 tunazielekeza katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini karibuni bilioni 58 kati ya hizo zinaenda katika elimu ya sekondari na lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba maabara tunaziimarisha katika maeneo yetu na ndiyo maana juzijuzi tumetoa fedha zaidi ya shilingi bilioni 16 ambazo tunakwenda kununua vifaa vya maabara kwa vijana wanapokuwa sekondari waweze kusoma vizuri masomo yao.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, *High School* ya Kirando tumejenga maabara leo miaka minne, na mlileta vifaa vya maabara vinakaa chini vinaliwa na mchwa. Lini Serikali itapeleka pesa kumaliza majengo matatu ambayo yako tayari yameshapigwa bati lakini yamekaa kama vichaka vya kuchezea panya ndani?

**SPIKA:** Sekondari ya Kirando inahitaji msaada, wananchi wameshachangia; Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Keissy na *DC* wake wa Wilaya ya Nkasi, ndugu yangu Saidi Mtanda, katika wilaya ambazo zinafanya kazi kubwa sana ya ujenzi wa miundombinu ni Wilaya ya Nkasi.

Mheshimiwa Spika, na niseme juhudi iliyofanywa na wananchi katika eneo hilo, hasa ujenzi wa hiyo maabara, juzijuzi kama nilivyosema tulipeleka fedha ili wabainishe yale maboma, nadhani hilo ni miongoni mwa maboma. Nimuagize Mkurugenzi katika vile vipaumbele ambavyo tumepeleka fedha hizi za maboma hilo liwe sehemu mojawapo, sasa sijui kama watakuwa hawajaingiza. Lakini tutafuatilia, kuhakikisha ofisi yetu maabara hiyo inakamilika, maabara iweze kufanya kazi, Mheshimiwa Keissy usiwe na hofu.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali lingine bado tuko Wizara hiyo hiyo, linaulizwa na Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini. Mhesimiwa Issaay.

Na. 272

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Mbulu**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Kupitia Sera ya Serikali ya kila kata kuwa na kituo kimoja cha afya, ni kata mbili tu zimebahatika kuwa na vituo vya afya kati ya kata kumi na saba (17) za Halmashauri ya Mji wa Mbulu; vituo hivi viko kwenye Tarafa za Daudi na Endagikot:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga kituo kimoja cha afya Kata za Kainam au Muray kwa ajili ya kupeleka huduma ya afya katika Tarafa ya Nambis yenye kata nne na vijiji ishirini na mbili na wakazi 24,800 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012?

(b) Serikali ina sera ya kutoa huduma za afya bila malipo kwa watoto walio chini ya miaka mitano na akina mama wajawazito; je, Serikali inachukua hatua gani katika vituo ambavyo bado vimeendelea kuchangisha kundi hili muhimu katika jamii?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Seleiman Said Jafo, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya uhaba wa vituo vya afya katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu. Kutokana na hali hiyo, Serikali iliamua kuanza na ujenzi wa Vituo vya Afya viwili na Daudi na Tlawi vilivyogharimu jumla ya shilingi bilioni moja kwa kila kituo kupata shilingi milioni 500. Hata hivyo, Serikali inatambua na imesikia kilio cha Mheshimiwa Mbunge, Serikali itafanya juhudi kwa kadri iwezekanavyo ili kuwasaidia wananchi wa kata hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza bajeti ya dawa kutoka shilingi bilioni 31 hadi bilioni 270 ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi yakiwemo makundi yenye msamaha wa matibabu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imeidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 104 kupitia Mfuko wa Afya wa Pamoja, ile *basket fund,* ambapo sehemu kubwa ya fedha hizo ni kwa ajili ya dawa na vifaatiba. Hivyo, Serikali haitarajii kuona akina mama wajawazito pamoja na watoto wenye umri chini ya miaka mitano wakichangishwa. Serikali haitasita kuchukua hatua kwa wote watakaobainika kuwatoza makundi hayo kwa kuwa ni kinyume na maelekezo ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa muuliza swali Mheshimiwa Issaay, Mbunge wa Mbulu, uliza swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyofanya ya ujenzi wa Vituo vya Afya vya Daudi na Tlawi. Hata hivyo, katika swali langu la msingi nilikuwa nimeomba kituo hiki kwa ajili ya tarafa kwa sababu Jimbo la Mbulu Mjini lina tarafa tatu, tarafa mbili zimeshapata vituo vya afya ambavyo ni vituo pekee katika Jimbo la Mbulu Mjini.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Tarafa ya Nambis ambayo iko pembezoni kama sehemu ya vijijini haina kituo cha afya na ina zahanati mbili tu katika kata hizo nne. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kutafuta fedha za dharura ili walau zahanati moja katika zile mbili kwenye tarafa hiyo ikapandishwa hadhi na kuongezewa majengo na miundombinu mingine ya huduma ili wananchi hao

wapunguziwe adha ya kusafiri mbali na huduma bora zaidi za afya?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; katika mpango wa awali wa vituo viwili vya afya; Kituo cha Afya Tlawi na Kituo cha Afya Daudi, Serikali ilikuwa na nia njema ya kupeleka vifaatiba na vitendeakazi vya milioni 440. Je, ni lini sasa Serikali yetu itakamilisha upelekaji wa vifaa hivi vya milioni 440 katika Vituo vya Afya Daudi na Tlawi ili kuweza kuboresha huduma ya afya?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, swali limeeleweka. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nikiri wazi kwamba Mheshimiwa Zacharia amekuwa ni mfuatiliaji sana na hata wiki iliyopita tulikuwa pamoja kujadili mambo mbalimbali katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, saula la jinsi gani tupate fedha za haraka, naomba Mheshimiwa Mbunge nikuahidi kwa sababu kwanza ufahamu kwamba juzijuzi tulikuwa twende wote pamoja kule Jimboni Mbulu lakini kulikuwa na mkutano ule wa Ma-*DC* ambao ulikuwa unafanyika tumeshindwa kwenda. Kwa hiyo, ahadi yetu tunatarajia Mwezi wa Sita tutaenda hata ikiwezekana *site* hiyo tutaweza kufika. Lakini kikubwa zaidi tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo tutafute fedha kuisaidia hilo eneo ambalo umezungumza kwa lengo kubwa la kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, *agenda* ya vifaatiba ni kweli tumejenga vituo takribani 352 na katika vituo hivyo vituo 44 vya kwanza vimeshapata vifaa lakini vituo vingine bado vifaa vinakuja. Kwa hiyo, tutafanya kila liwezekanalo vituo vyote 352 ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambavyo Mheshimiwa Rais amevijenga vyote vitapata vifaa kwa lengo kubwa wananchi waweze kuhudumiwa vizuri. Kwa hiyo, usipate shida Mheshimiwa Issaay, tunalifanyia kazi.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa wa Bunge Vijijini, Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la msingi lipo kwenye Jimbo la Mbulu Mjini na mimi nipo Jimbo la Mbulu Vijijini. Jimbo la Mbulu Vijijini kuna kata 18, Mheshimiwa Waziri umefika umekuta kituo kimoja cha afya kama mke wa Mkristo; unaonaje ndugu yangu? Maretadu wamejenga kituo cha afya wamefika lenta; utatupatia fedha ili walau tuwe na kituo cha pili cha afya?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri tafadhali, kituo cha afya.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kweli nimefika Mbulu na ni kweli ni changamoto kubwa ndiyo maana Serikali katika eneo lile kutokana na shida kubwa tulianza na ujenzi wa Kituo cha Afya cha Dongobesh. Lakini hata hivyo tuliamua kutoa fedha zaidi ya shilingi *1.5 billion* kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbulu Vijijini.

Mheshimiwa Spika, nafahamu Mbulu jinsi ilivyo kuna maeneo wengine wako katika Bonde la Ufa na wengine wako juu. Tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo kama maombi Mheshimiwa Mbunge alivyoyaacha mara kadhaa ofisini kwetu tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo wale watu wa kata zingine kule za mbali tuangalie jinsi gani tutafanya tupate fedha kuwasaidia ujenzi wa kituo cha afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Mahawe nilikuona.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, Tarafa ya Bashnet iliyopo Babati Vijijini haina kituo cha afya hata kimoja na kilichopo kinatoa

huduma sawasawa na zahanati. Je, ni lini Serikali itakumbuka Tarafa ya Bashnet? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, huko Bashnet, Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, tunatambua changamoto ya Mkoa wa Manyara kwa ujumla wake na ndiyo maana Serikali tulitoa *3.9 billion* kwa ajili ya vituo vya afya vile vyote na tumetoa takribani shilingi bilioni 3 kwa ajili ya hospitali za wilaya. Lakini hata hivyo, nafahamu Babati Vijijini ina changamoto kubwa ndiyo maana tulianza na Kituo cha Afya cha pale Magugu na kituo cha afya kingine, lakini mwaka huu tumewapatia ujenzi wa hospitali ya wilaya katika bajeti ya mwaka huu ambayo nimeisoma si muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo hilo Mheshimiwa Mahawe alilolizungumza tutalichukua kulifanyia kazi, nini kifanyike kwa haraka kwa mpango wa Serikali kuwahudumia wananchi wa Babati Vijijini, tunafahamu wengine wanatoka mbali na huduma hizi ni huduma za msingi kuokoa maisha ya akina mama wajawazito. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mahawe naomba ondoa hofu, kama upiganaji wako ulivyo wa kawaida kwa Mkoa mzima wa Manyara, kilio chako kimesikika tutakifanyia kazi.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 273

**Bar na Club Zilizopo Kwenye Makazi ya Watu**

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Kuna baadhi ya *Bar* na *Club* ambazo zimejengwa kwenye makazi ya watu ambazo zimekuwa kero kwa jamii:-

Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu *Bar* na *Club* hizo ambazo zinakiuka sheria na maadili ya jamii?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri, ukizingatia kwamba mwezi huu ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, tafadhali. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba biashara nyingi, zikiwemo za uendeshaji wa *bar* na *club* zipo kwenye maeneo ya makazi ya watu. Serikali inawaelekeza wamiliki wote wa *bar* na *club* kuwa wanapaswa kuzingatia maelekezo ya Sheria ya Vileo Sura Na. 28 ya mwaka 1968, kifungu cha 14(1) katika uendeshaji wa shughuli zao. Aidha, Serikali haitasita kuchukua hatua kwa vitendo vyovyote vitakavyobainika kukiuka sheria na kusababisha kero kwa wananchi wengine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Msabaha, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nianze na hapa kwenye huu Mkoa wako wa Dodoma. Niko maeneo ya katikati hapo Mjini, baa hizi zimekuwa kero kwa wananchi ambao wamejenga maeneo karibu na hizi bar.

Mheshimiwa Spika, isitoshe, wamekuwa wanatoka wanawake mbalimbali, wengine wanatoka Dar es Salaam, wanatoka Morogoro, wanatoka mikoa mbalimbali wanakuja hapa kwenye Jiji hili la Dodoma kwa sababu ni Makao Makuu ya Serikali. Tatizo kubwa bar hizi zinapiga miziki na matusi makubwa sana kwa jamii, imekuwa ni kero kubwa sana kwa jamii.

Je, ni lini Serikali itahakikisha inafanya msako maalum kwa Mkoa huu wa Dodoma, hasa ukichangia maeneo ya Mjini niliyoyataja Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuna hawa akinamama ambao hawataki kufanya kazi wanajiingiza kwenye haya masuala yasiyokuwa ya stahiki za kijamii yaani kama tukisema kama Marekani wao wana tozwa kodi, Uholanzi wanatozwa kodi, sasa hawa wanawake askari wa Dodoma wamekuwa mara kwa mara askari kanzu wamekuwa wakiwachukua mara kwa mara lakini wanarudi tena kwenye maeneo haya haya wanakuwa wanafanya matukio ambayo hayaendani na jamii ya Kitanzania na maadili.

Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha inawachukua wanawake wote hawa ambao wanafanya biashara haramu ambazo hazina stahiki na kuangalia hata wanawapeleka kwenye mashamba ya JKT wakafanye kazi? Naomba jibu la Serikali

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Maryam wanafanya biashara gani zisizo stahiki? Majibu Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Msabaha, meti wangu wa kambi yetu ya Bulombola kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kilio hiki cha Dodoma kikubwa zaidi nini mkakati wa Serikali? Nimuelekeze Mkuu wa Mkoa kwa sababu akiwa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama ya Mkoa, na Mkuu wake wa Wilaya kuhakikisha kwamba vile vitendo vya hovyo vyote ambavyo vinakiuka utaratibu waweze kuvisimamia kwa sababu Jeshi la Polisi hapa lipo waangalie nini kinachofanyika kuhakikisha hadhi ya Jiji la Dodoma linabakia kama lilivyo badala ya kuchafuliwa.

Mheshimiwa Spika, mkakati hawa watu ambao hii kauli nyingine uliyoizungumza ya watu inawezekana wanafanya biashara zisizo sawasawa, ndiyo maana Serikali mnakumbuka mwaka jana hapa tulipitisha sheria asilimia 10 iende katika vikundi ya vijana, akinamama na walemavu. Imani yetu ni kwamba kwa vile ukiangalia Dodoma pato lao

ni kubwa mpaka juzi juzi wamekusanya zaidi ya shilingi bilioni 55 *own source collection.* Kwa hiyo ukichukua hapo asilimia nne yake maana yake ni fedha nyingi sana, kwa hiyo vikundi hivi ninaimani kwamba viongozi wetu watendaji wetu hasa maafisa maendeleo ya jamii chini ya Mkurugenzi wakiweka utaratibu mzuri wa kuwawezesha hawa akinamama tutawatoa katika suala zima hatarishi walilokuwepo nalo kwa wao kwamba kujiingiza katika shughuli halali za kiuchumi za Taifa letu hili.

**SPIKA:** Tuone kule Moshi mambo haya yapo pia Mheshimiwa Shally Raymond

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwenye awamu ya tatu nyumba za Serikali ziliuzwa na nyingi zilikuwa zile za *Shanti Town* kule Moshi, Oysterbay Dar es Salaam, Gangilonga na Wilolasi Iringa na hapa Kilimani Dodoma na kwingineko. Nyumba hizo zilikuwa ni za makazi na zilikuwa ni eneo tulivu sana zikiitwa uzunguni. Lakini nyumba hizo ndiyo zimegeuka sasa ni Bar, ni maeneo ya kuoshea magari kule Moshi *Shanti town* zinasumbua wananchi na watoto hawalali. Ni lini sasa Serikali italeta sheria hapa Bungeni kama zile sheria za awali hazifuatwi ili zikatazwe kabisa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli hii ni kero kubwa sana mpaka hivi leo asubuhi nilikuwa naongea na Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mrisho Gambo kwamba ukiangalia kuna jengo la sinema karibu ya Shule ya Sekondari ya Arusha Girls na Shule ya Sekondari nyingine katikati, inaonekana badala ya kuweka jengo la sinema la kawaida sasa imekuwa sehemu ya *night club* na mambo vuruguvurugu hata hivyo kuhatarisha hasa madhara makubwa kwa wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Spika, lakini maeneo hayo uliyoyazungumza ni kweli mkakati wa Serikali nadhani sheria

ipo isipokuwa ni *enforcement* ya hizi sheria tu ndiyo inatakiwa. Kikubwa zaidi niwaelekeze viongozi wetu katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa ambao ni Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya palepale ninaimani wakizingatia vizuri eneo hili la kusema kuleta utulivu katika maeneo yao ninaamini kwamba jambo hili halitokuwa na mashaka. Kwa hiyo, niwaagize wakuu wa mikoa wote sasa waanze kufanya ufuatiliaji wa karibu kukomesha vitendo hivi vya hovyo vinavyotokea katika mazingira yetu ambao siyo jambo jema katika Taifa letu.

**SPIKA:** Ahsante sana, swali hili la unywaji wa pombe uliokithiri mpaka wanaume wanasahau kuwajibika na kadhalika haiwezekani swali hili likapita bila Mbunge wa Rombo kupata nafasi, Mheshimiwa Joseph Selasini nimekuona uliza swali. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru hizi bar zinamilikiwa na watu wakubwa sana na wenye fedha hata miongoni mwetu vilevile kuna baadhi ambao tuna hizi bar, na ni kutokana na mipango miji kutozingatiwa. Sasa ni kwanini Serikali isitoe tu tamko kwamba kuanzia sasa bar hizi zinazojengwa hovyo hovyo ni marufuku na atakayetoa kibali hatua zitachukuliwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo tafadhali

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema na Mheshimiwa Mbunge amesema wamiliki wa hizo bar wengine ni wakubwa inawezekana wengine wako humu ndani, kikubwa zaidi sheria ipo. Jambo kubwa linalotakiwa kufanywa sasa hivi ni kufanya usimamizi wa sheria, ndiyo maana hapa nimezungumza siwezi kutoa matamko tu hivi hivi kwa sababu sheria tayari ipo ni lazima tuzingatie tunasema STK – Sheria, Taratibu na Kanuni.

Mheshimiwa Spika, nina imani viongozi wangu wote wa ngazi za chini huko chini hasa wakuu wa mikoa na wakuu

wa wilaya naomba wawe wakali hasa kuona haya mambo yasiyokuwa sawasawa wayasimamie kuondoa hii kero ambayo Mheshimiwa Selasini hapa ameizungumza.

**SPIKA:** Ahsante tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, sasa tuhamie Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, swali litaulizwa na Mbunge wa Bumbwini Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed tafadhali uliza swali lako Mheshimiwa Mbunge wa Bumbwini.

Na. 274

**Matokeo Mabaya ya Mtihani ya Kidato cha Nne**

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED** aliuliza:-

Matokeo ya mitihani ya Kidato cha Nne yamekuwa mabaya kwa kipindi kirefu sasa na hali haijapatiwa ufumbuzi wowote:-

(a) Je, nini tamko la Serikali kuhusiana na hali hiyo?

(b) Je, ni juhudi zipi za makusudi ambazo Serikali inakusudia kuchukua ili kupandisha hali ya ufaulu wa wanafunzi hao?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa William Tate Ole Nasha.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed Mbunge wa Bumbwini lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ufaulu wa wanafunzi katika mtihani wa kidato cha IV umekuwa ukiongezeka mwaka hadi

mwaka ambapo katika mwaka 2018 watahiniwa waliofaulu ni asilimia 78.3 ikilinganishwa na asilimia 77.09 ya mwaka 2017, asilimia 70.35 ya maka 2016 na asilimia 67.91 ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuongeza ufaulu katika ngazi mbalimbali za Elimu. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga na kufanya ukarabati mkubwa wa miundombinu katika shule ambapo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, zaidi ya shilingi bilioni 93.8 zimetumika katika uboreshaji wa miundombinu ya shule 588 zikiwemo (Msingi 303 na Sekondari 285) yakiwemo madarasa 1,190, mabweni 222 na vyoo 2,141, mabwalo 76 na nyumba 99.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Serikali imeendelea kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo, vifaa vya maabara katika shule na vifaa vya kielimu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Vile vile katika kipindi cha mwaka 2017 hadi Aprili, 2019, Serikali imeajiri jumla ya walimu 17,884.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imeendelea kuimarisha Idara ya Udhibiti Ubora wa Shule ambapo imenunua na kusambaza magari 45 ya udhibiti ubora wa Shule na pikipiki 2,897 kwa ajili ya Maafisa Elimu Kata. Katika mwaka 2019/ 2020 Serikali inatarajia kujenga ofisi 100 za wadhibiti ubora wa shule na kuongeza idadi ya watumishi hao. Hivyo, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuendelea kuimarisha ubora wa elimu nchini.

**SPIKA:** nimekuona Mheshimiwa muuliza swali Mbunge wa Bumbwini uliza swali la nyongeza.

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu ambayo Serikali imetoa ambayo ni ya kawaida sana hayako katika uhalisia yako *much shallow* kwa kweli katika swali langu la msingi lililenga zaidi ufaulu wa wanafunzi kutoka kidato cha IV kwenda kidato cha V, sio labda majengo zaidi aaah! Ni kiasi gani

asilimia ngapi inafaulu kutoka IV kwenda V na pia lilenga zaidi kwenye *subject matter.*

Sasa je, Serikali inajiridhishaje hata hizi takwimu ulizonipa nina mushkeli nazo nitaomba zaidi kama ziko takwimu za ufaulu kutoka IV kwenda V nipatiwe kwa Tanzania nzima. Sasa swali langu la nyongeza ni hili. Je, Serikali kupitia Wizara inayohusika inajiridhishaje kwamba zile *competences* zilizoainishwa kwenye *syllabus* zinafikiwa? Hapo ndiyo ulipo mushkeli wangu.

**SPIKA:** majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu yale ya takwimu yale mtashughulika nayo baadaye, lakini haya ya kisera.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amesema majibu yetu yamekuwa ya kawaida na ni *shallow*. Ukweli wa mambo tumejibu kutokana na swali alilouliza yeye kauliza matokeo ya mtihani wa kidato cha IV yamekuwa mabaya kwa kipindi kirefu sana na hali hii haijapatiwa ufumbuzi wowote na maswali ikawa ni nini tamko la Serikali kuhusiana na hali hiyo, lakini vile vile akauliza kuhusu juhudi.

Mheshimiwa Spika, sasa tamko la Serikali nililokupa ni kwamba tumekupa takwimu kuonyesha kwamba ukiangalia kuanzia mwaka 2015 mpaka sasa kumekuwa na ongezeko la ufaulu katika mitihani ya Kidato cha IV kutoka mwaka hadi mwaka. Mwaka huu tumefikia asilimia 78, wakati mwaka 2015 tulikuwa asilimia 67. Sasa kama unataka kujua ni kiasi gani cha hao wanaoenda kidato cha V hapo sasa ungeleta swali lingine au ungeuliza kwenye swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, na kuhusiana na hilo suala alilouliza la *competences* naomba nimuhakikishie Mbunge kwamba tunajaribu kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba elimu yetu inakuwa bora na ndiyo maana nimeorodhesha hatua au mambo mbalimbali ambayo tunayafanya ikiwa ni pamoja na kujenga miundombinu, ikiwa ni pamoja na kuajiri walimu, tunapitia mitaala, tumehuisha mfumo wa udhibiti

ubora. Kimsingi tulipo sasa ni bora kuliko tulikotoka na nimuhakikishie tu pamoja na Mheshimiwa Wabunge wengine kwamba Serikali itaendelea kuweka mkazo ili kuendelea kuboresha elimu yetu.

**SPIKA:** Nimewaona Mheshimiwa Najma Giga na Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Najma Giga.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi kwa vile suala la elimu kwa ujumla wake siyo suala la muungano na kwamba Baraza la Taifa la Mitihani pamoja na elimu ya juu ndiyo vya muungano. Sasa swali langu liko hapa Sera za elimu pamoja na mitaala kwa vyovyote itakuwa ni tofauti baina ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Sasa kwa nini Serikali zetu mbili kwa lengo la kuimarisha elimu Tanzania zisikae pamoja zikatengeneza sera ya elimu na mitaala inayofanana ili kuinusuru Zanzibar kila mara kutokea kumi za mwisho. Ahsante dhamira ni kuimarisha muungano.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anashauri kwamba Serikali zetu mbili zikutane na kujaribu kukaa ili kuangalia uwezekano wa mitaala yetu iweze kufanana. Ni wazo ametoa sio wazo baya kwa sababu ni nchi moja tutaenda kuliangalia sio kitu ambacho hakiwezekani.

**SPIKA:** Mheshimiwa James Mbatia nilishakutaja.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana ukitaka kuangamiza Taifa lolote anza kuangamiza au kuharibu mifumo yake ya elimu inayolinda utu wa binadamu. Mwaka 1979 mabadiliko ya mtaala hayakuweza kukidhi changamoto za mabadiliko ya elimu ya wakati huo na Mwalimu Nyerere akaunda Kamisheni ya Makweta. Sasa ni

miaka 37 tangu Kamisheni ile kufanya uchambuzi wa elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Sera ya elimu ya 2014 na mtaala wake haukidhi changamoto za elimu za sasa za lengo la nne la maendeleo endelevu ya dunia la elimu bora sawa shirikishi kwa wote. Sasa je Serikali haioni umuhimu wa kuweza kuchukua mifumo kama za Finland, Vietnam na kwingine ili tuweze tukaendana na changamoto za elimu za dunia za sasa badala ya kufanya elimu yetu *trial and error* kama ilivyo sasa?

**SPIKA:** majibu ya swali hilo la kisera Mheshimiwa Naibu Waziri Laigwanani Ole Nasha.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nikiri kwamba Mheshimiwa Mbatia ni Mbunge makini sana kwenye masuala ya elimu kwahiyo mara nyingi ushauri wake tunauchukua kama ni ushauri mzuri. Naomba tu nimuhakikishie kwamba Wizara yangu Serikali haijawahi kukaa kimya kufanya mapitio ya mitaala pale inapobidi hata hivyo kama unavyofahamu, ubadilishaji wa mitaala huwezi ukawa unabadilisha kila siku kwa kiasi kikubwa unachofanya ni kufanya mabadiliko madogo madogo kama mwenyewe anavyosema maendeleo na mabadiliko ya teknolojia yanayotokea duniani na tunaendelea kufanya hivyo kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile nimuhakikishie kwamba kwa sasa tunafanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ili tuweze kuhuisha ili iendane na mabadiliko ambayo yametokea na iweze kutupa elimu ambayo ni bora zaidi katika wakati tuliopo. Naomba nimuhakikishie vile vile kwamba wakati tunahuisha Waheshimiwa Wabunge watapata fursa vile vile ya kushiriki katika mjadala ambao utatuletea Sera mpya.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kama Mheshimiwa Mbunge atakumbuka wakati tunajadili hotuba ya Wizara yetu tulitoa ahadi ambayo tunataka kuitekeleza ya kufanya

mjadala kuwaita wadau tukutane tuongee ili hayo maoni na mengine tuweze kuyachukua katika kujaribu kuboresha sera yetu na hatimaye hata ikiwezekana na kubadilika mitaala iliyopo.

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge nawaomba tuendelee kwa sababu ya muda na Wizara ya Maliasili na Utalii swali la Mheshimiwa Zainab Nuhu Mwamwindi.

Na. 275

**Kuimarisha Miundombinu – Hifadhi ya Ruaha**

**MHE. ZAINAB N. MWAMWINDI** aliuliza:-

Katika kuboresha utalii katika Hifadhi ya Ruaha.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa kiwango cha lami barabara iendayo Hifadhi ya Ruaha pamoja na kuimarisha miundombinu ya ndani ya Hifadhi hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Nuhu Mwamwindi Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mipango ya kukamilisha ujenzi wa barabara iendayo Hifadhi ya Taifa ya Ruaha yenye urefu wa kilomita 130 kwa kiwango cha lami. Hadi sasa, kipande cha barabara hiyo kutoka Iringa mjini hadi Kalenga chenye urefu wa kilometa 14 kimeshajengwa kwa kiwango cha lami. Sambamba na ujenzi

wa barabara hiyo, pia miundombinu ya ndani ya Hifadhi ya Taifa Ruaha inaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, jukumu la ujenzi wa barabara zilizoko nje ya hifadhi ni la Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini TARURA na Wakala wa Ujenzi wa barabara TANROADS. Wizara itaendelea kufuatilia kwa karibu mamlaka zinazohusika ili kuzishawishi ziweke barabara hiyo katika Mpango Kazi wa uendelezaji wa barabra za Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa ina utaratibu wa kufanya ukarabati wa miundombinu ndani ya hifadhi za wanyamapori kila mwaka, pamoja na kuongeza miundombinu mipya pale inapohitajika. Hifadhi ya Taifa Ruaha, ina mtandao wa barabara za utalii zenye urefu wa takriban kilometa 1,590. Hifadhi ya Taifa Ruaha kupitia mpango wake kukuza na kuendeleza utalii Kanda ya Kusini *REGROW* imepanga kukarabati na kufungua barabara za utalii zenye urefu wa kilometa 1,055 katika kipindi cha miaka mitano ya mradi huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainab nilikuona uliza swali la nyongeza.

**MHE. ZAINAB N. MWAMWINDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Leo nasimama mara ya tatu katika Bunge lako Tukufu nikiikumbusha Serikali kuhusu barabara hii itokayo Iringa kwenda Ruaha *National Park.*

Mheshimiwa Spika, barabara hii urefu wake ni kilometa 104 na kama majibu ya Naibu Waziri alivyosema kwamba imetengenezwa kwa kiwango cha lami kilomita 14. Kwa masikitiko makubwa ninasikitika kwamba barabara hii kwa hizo kilomita 14 imejengwa na Marais wote wanne. Upembuzi yakinifu ulishafanyika na kila mwaka Serikali inapanga fedha za ujenzi wa barabara hii. Je, ni kwanini Serikali inapata kigugumizi kuikamilisha barabara hii?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, barabara zote za ndani ni mbovu na wakati wa masika ni mahandaki, kiasi kwamba upitaji wake na watalii wanapata shida inapunguza pato la Taifa. Swali ni lini Serikali itapanga pesa kwa ajili ya kutengeneza barabara hii? Ahsante sana

**SPIKA:** Majbu ya maswali hayo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri na Utalii tafadhali.

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakiri kwamba katika jibu langu la msingi nimesema tumekwisha jenga kilometa 14 kati ya kilometa 130 ambazo zipo katika barabara hiyo, na barabara hiyo tayari imekwisha fanyiwa upembuzi yakinifu. Mheshimiwa Mbunge anafahamu juhudi za kilometa 14 ambazo zimekwisha fanyika sio haba. Lakini anafahamu yeye ni mjumbe wa Kamati ya Maliasili, tumekuwa naye katika ziara juhudi za Wizara yetu katika kuhakikisha kwamba barabara hizo zinajengwa ni kubwa, nimuombe awe na imani na Serikali kama yalivyo maeneo mengine barabara hii itajengwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake kuhusu ubovu wa barabara zilizopo ndani ya Ruaha ni kweli, pamekuwa na tatizo la ubovu wa miundo mbinu mbalimbali katika hifadhi ya Ruaha. Lakini nimesema katika jibu la msingi tunao mradi mkubwa *REGROW*, ambao tayari tulikwisha saini mkataba na umeanza kutekelezwa, Barabara zote pamoja na miundo mbinu mingine katika hifadhi ya Ruaha imo katika mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, na nimhakikishie kwamba wakati kutengeneza mkataba huo maeneo yote haya ambayo yamekuwa yakisababisha hifadhi hii kushindwa kutumika wakati wa masika yatakuwa yamefanyiwa matengenezo makubwa na moja ya eneo ambalo Wizara yetu imehakikisha kwamba inaipa kipaumbele kufungua utalii maeneo hayo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ninafahamu juhudi zake kubwa za kupingania utalii maeneo ya Mkoa wa

Iringa na kusini kwa ujumla lakini nimhakishie kwamba Serikali inalitilia maanani suala hilo.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Yussuf nilikuona uliza swali lako la nyongeza upande wa CUF.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru katika hifadhi ya Ruaha tatizo sio barabara tu, hata Mto Ruaha mkuu ambao ndio kitovu cha hifadhi ya Ruaha, unatanuka na unakauka kwa baadhi ya vipindi hali ambayo inahatarisha maisha ya wanyama na inahatarisha hifadhi nzima yenyewe kutoweka kabisa. Sasa Serikali inachukua hatua gani kuona kwamba ule mto hautanuki na maji yanaendelea kutitirika katika kipindi cha mwaka mzima ili wanyama wetu waendelee kuhuika katika hifadhi ile?

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Yusuf Serikali izuie mto kutanuka ifanyaje. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli historia inaonyesha Mto Ruaha ulikuwa una *flow* maji yake kwa mwaka mzima na kwa miaka ya hivi karibuni umeendelea kuwa na tabia tofauti kwa maana unapoteza maji katika kipindi cha miezi miwili mpaka mitatu kwa mwaka. Lakini sababu zinafahamika ikiwemo pamoja na matatizo ya taabu ya nchi lakini pia matumizi makubwa yanayofanywa na wakulima walioko kwenye mabonde yaliyoko juu Mto Ruaha.

Mheshimiwa Spika, katika mradi wetu wa *REGROW* moja ya maeneo ambayo yanaenda kushughuliwa ni pamoja na elimu kubwa itakayotolewa kwa wakulima hao. Lakini miundombinu ambayo itatengezwa ili kuwafanya wanaotumia maji kwa ajili ya kilimo katika maeneo hayo iwe ni miundombinu ya kisasa ambayo itaruhusu *flow* ya maji kuendelea kuwepo, kuliko hivi sasa hivi wakulima wanazuia maji na kuyaweka kwenye mabwawa ya akiba kwa mwaka mzima hata kama maji hayo hawayatumii. Kwa hiyo, mpango huu kwa ajili mto huo tunao katika mradi wetu mkubwa.

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge tuendelee bado tupo Wizara hiyo hiyo Maliasili na Utalii swali la Mheshimiwa Dkt. Raphel Masunga Chegeni Mbunge wa Busega, hayupo wa kumuulizia swali hayupo...

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Kwa niaba yake nakuruhusu umuulizie swali.

Na. 276

**Ongezeko la Tembo na Wanyama Waharibifu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA (K.n.y. MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI)** aliuliza:-

Ongezeko la tembo na wanyama waharibifu imekuwa kero kubwa sana kwa wananchi wanaoishi maeneo ya kando kando ya hifadhi na ziwa.

Je, Seikali ina mkakati wa kudhibiti tatizo linalosabishwa na kadhia hiyo?

**SPIKA:** Ahsante sana, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Constatine Kanyasu.

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali Mheshmiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni Mbunge wa Busega kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kanuni za wanyamapori wakali na waharibifu za mwaka 2011 zimeanisha aina wanyamapori ambao wanapaswa kushughulikiwa kama wanyamapori wakali na waharibifu. Kwa mujibu wa kanuni hizo, jedwali la tatu limeorodhesha wanayapori hao ambao ni tembo, kiboko, mamba, nyati, chui na simba.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mikakati ifuatayo katika kunusuru maisha na mali za wananchi kutokana na madhara yanayosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu:-

Mheshimiwa Spika, moja kufanya doria za udhibiti wa wanyamapori hatari na waharibifu, kupitia askari wa wanyamapori Tanzania, *TAWA,* Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA),* Halmashauri za Wilaya na Mamlaka ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro na wadau wengine. Lengo ni kuhakikisha kwamba tukio lolote la uvamizi wa wanyamapori wakali na waharibifu linashughulikiwa kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, mbili kutumia mbinu na teknojia mbalimbali mfano kupanda pilipili na kutundika mizinga ya nyuki pembezoni mwa mashamba, kufunga vitambaa vyenye vilainishi vya magari yaani *oil* kuzungushia mashambani na kutumia ndege zisizokuwa na rubani kwa ajili ya kudhibiti tembo.

Mheshimiwa Spika, tatu kuendelea kutoa elimu za uhifadhi kwa jamii ili wananchi waepuke kulima kwenye maeneo ya shoraba.

Mheshimiwa Spika, wapo wanyamapori waharibifu ambao wanaweza kushughulikiwa na mkulima mmoja mmoja pamoja na Wizara ya Kilimo. Wanyamapori hao ni pamoja na nyani, ngedere, tumbili, nguruwepori na ndege aina ya kwelea kwelea na wengine. Aidha, Wizara intoa rai kwa Maafisa Ugani wa kilimo kushirikikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kutoa elimu kwa wananchi juu ya kukabiliana na changamoto zinazotokana na wanyamapori jamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na kadhia hiyo, Serikali imekuwa ikichukua muda

mrefu sana kulipa fidia na kifuta machozi lakini gharama hiyo pia haiakisi gharama ya uharibifu unaofanywa.

Je, Serikali ipo tayari kubadili kanuni zake kwa kuongeza gharama za kifuta machozi?

Mheshimiwa Spika, binafsi nimekuwa nikichukua hatua ya kumpigia simu Meneja wa *TAWA Maswa Game Reserve* lakini amekuwa haonyeshi ushirikiano wowote.

Je, Serikali ipo tayari kuwapatia mizinga wananchi katika vikundi katika Kata ya Lukungu, Mwakiloba, Kilejeshi na Wilaya zote za Mkoa wa Simiyu ili kuweza kukabiliana na tatizo la tembo hao?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri tatizo la tembo kule Maswa.

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Spika, ni kweli yamekuwepo malalamiko ya muda mrefu ya kiwango kidogo cha kifuta machozi na kifuta jasho ambayo yamekuwa yakitolewa na Wizara yangu. Lakini nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu inapitia upya viwango hivyo, na mara itakapokamilisha tutatangaza na kuwajulisha waathirika tumefanya marekebisho na nina imani ingawa haiwezi kulipa thamani halisi ya maisha ya mtu na mazao yaliyoharibika lakini itakuwa imeongeza kiwango ambacho tumekuwa tukitoa kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili nimefahamu kuwa Mheshimiwa Leah Komanya amekuwa akipiga simu mara kwa mara kutetea wananchi hasa wakati mazao yanapokuwa yamefamiwa na wanyama. Nimhakikishie tu kwamba huyu afisa ambaye hatoi ushirikiano tutampa maelekezo, lakini nitoe maelekezo kwa maafisa wetu nchi nzima kuhakikisha wana-*respond* haraka sana wanapopata taarifa za uwepo wa wanyama.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasa hivi wanyama hawa wameongezeka baada ya kudhibiti ujangili kwa kweli

limekuwa ni tatizo lipo nchi zima. Kwa hiyo, niwaelekeze maafisa wanyamapori popote pale walipo kuhakikisha kwamba wana wajibika haraka wanapopata taarifa hizi ili kuweza kutoa ushirikiano kwa wananchi. Na nimhakikishi tutawasiliana ili tuweze kuona namna watakavyoweza kutoa mizinga hii ya nyuki katika maeneo ya vijiji hivi.

**SPIKA:** Ahsante sana nilikuona Mhehimiwa Catherine na Mheshimiwa Andrew Chenge. Tuanze na Mheshimiwa Catherine.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuwa kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu katika Wilaya ya Arumeru katika kijiji cha Ngalinanyuki na hifadhi ya Taifa ya Mumera, na mpaka sasa hivi wananchi wale hawajafikia muafaka wa mgogoro huo.

Je, Serikali sasa ni wakati muafaka wa mimi na Mbunge aliyeapishwa leo na Mheshimiwa Waziri kuongozana mpaka Kijiji cha Ngalinanyuki kwenda kusikiliza wananchi wale ili kero yao ifikie muafaka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Maliasili na Utalii tafadhali.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa hapa Bungeni na Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kujibu swali na nyongeza na Mheshimiwa Catherine Valentine Magige kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwamba kwanza katika eneo la *Arusha National Park* ususani katika sehemu hiyo ya Momera hakuna mgogoro *per se* hakuna mgogoro unaoweza kuita mgogoro. Lakini kwa sababu wananchi walienda mahakamani na walishindwa, kwa hivyo eneo lote lile ambalo walikuwa wanalidai ni eneo la Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na malalamiko ya wananchi na pamoja na kwamba wameshinda kesi mahakamani. Serikali imeona ikate sehemu ya eneo la *Arusha*

*National Park* ambalo lilikuwa ni miongoni mwa mashamba yaliyokuwa ya *settlers* wa eneo lile ili kuwagaia wananchi waweze kuishi kwa raha na amani zaidi. Kwa hiyo, wakati *process* hiyo itakapokamilika wananchi wa Momera watapata eneo ambalo tunazungumzia

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongozana nae kwenda kutoa maelezo hayo nitaomba aongozane na Mheshimiwa Naibu Waziri baada ya Bunge hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge aliyeapishwa leo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nami nakushuru sana kwa kunipa nafasi nisimame mbele ya Bunge lako Tukufu leo kwa mara ya kwanza katika historia ya maisha yangu. Nichukue nafasi hii basi kumshukuru Mungu sana ambaye ndie ametupa uhai na akatukutanisha leo. Lakini pia kwa kunipa nafasi hii ya kuwa Mbunge kwa mara ya kwanza kwenye Jimbo la Arumeru Mashariki.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nimejiandaa kuuliza swali la nyongeza kwenye maji. Namshukuru sana na kumpongeza Rais wetu Dkt. John Joseph Pombe kwa kazi nzuri anayofanya.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, basi niseme kuwa nipo tayari kuongozana na Waziri.

**SPIKA**: itakapofika wakati wa maji nitakupa nafasi. Nilidhani kwenye hili la Momera una la kusema.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, basi Waheshimiwa Wabunge nisubirini kidogo nijapange niseme.

**SPIKA:** Karibu sana, karibu sana Bungeni Mheshimiwa Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika nasema nipo tayari kongozana na Waziri kwa ajili ya kwenda kuzungumzia hilo jambo.

**SPIKA:** Nashukuru sana sasa Mheshimiwa Chenge, Mheshimiwa Chenge uliza swali lako. *(Kicheko)*

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya Bariadi kama ilivyo wilaya ya Busega, Bunda na Serengeti ni miongoni mwa Wilaya au maeneo yanayopakana na Hifadhi ya Serengeti. Lakini kikosi dhidi ya ujangili ofisi zake zipo Bunda na ofisi hiyo ndio inahusika na malipo ya kifuta jasho na kifuta machozi. Imekuwa ni shida sana kwa wananchi wanaotoka nje ya eneo la Bunda kama Baridi na baya zaidi wanapokuja kufanya malipo haya wanakuja kulipia malipo haya kwenye *guest house*.

Je, ni lini Serikali itafungua ofisi ya *KDU* mjini Bariadi ili kuondokana na adha hii hasa kwa akina mama ambao hawapendi kwenda *guest house* kwenda kupokea malipo yao?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii Mheshimiwa Constantine Kanyasu mnafungua lini *KDU* kule Bariadi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ofisi yetu ya *KDU* kwa sasa kikosi cha ujangili ipo Bunda na ni kwa sababu tuliamini kwamba Bunda ni katikati na eneo la Serengeti. Lakini nimhakikishie kwamba eneo hili analo lizungumzia yeye la Bariadi linapakana na Maswa, tunao maafisa wetu wa wanyamapori na tunaye afisa wa wanyamapori katika Maswa G*ame Reserve* na wengine.

Mheshimiwa Spika, tutakachofanya ni kuwaelekeza hawa watu wa *KDU* wahakikishe kwamba wanakuwa na mawasiliano ya haraka na watu wetu wa halmashauri ambao kwa utaratibu ni watu wa kwanza wanafika maeneo ambayo mazao yameharibiwa kabla ya maafisa wa *KDU*

kufika ili kutupa taarifa na kuweza kurahisisha mfumo wa malipo. Kwa hiyo, tumechukua ushauri wake wa kuwa na ofisi Bariadi, na tutakapo liangalia suala hili kulingana na uwezo wetu tutalizingatia.

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa kwa sababu ya muda, mtaona muda wetu umeisha kabisa na bado tuna maswali mengi Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma swali la maji.

Na. 277

**Hitaji na Majisafi na Salama- Manispaa ya Morogoro**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuza:-

Serikali inajitahidi kuwapatia maji wananchi wa Manispaa ya Morogoro. Licha ya jitihada hizo, hadi sasa ipo mitaa ambayo inapata maji kwa mgao na mingine haipati kabisa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha miundombinu ya Bwawa la Mindu ili wananchi wapate majisafi na salama kwa uhakika muda wote?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na shirika la maeneleo la Ufaransa *AFD* inatekeleza mradi wa majisafi na usafi wa mazingira Morogoro iko katika hatua za kumpata mataalam mshauri atakayefanya usanifu wa kina wa bwawa la mindu kwa kwa lengo la kuongeza urefu wa tuta la bwawa ambao utapelekea kuongeka kwa kiwango cha ujazo wa

bwawa. Ongezeko la ujazo wa maji katika bwawa utaiwezesha *MORUWASA* kuongeza kiwango cha ulazishaji wa majisafi hivyo kuondoa mgao katika mitaa inayopata maji kwa mgao. Hatua iliyofikiwa ni kuwa, taarifa ya uchambuzi *shortlist report* imewasilishwa *AFD* kwa ajili ya kupata kibali kabla ya kuwapata watalaam washauri makababrasha ya zabuni kwa ajili ya kuwasilisha mapendekezo ya kiufundi na kifedha.

Mheshimiwa Spika, mtaalam mshauri atakapopatikana atafanya usanifu wa kina pamoja na kuandaa vitabu vya zaburi kwa ajili ya manunuzi ya wakandarasi. Matarajio ni kazi ya ujenzi wa mradi huu kuanza katika mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ishengoma swala la nyongeza tafadhali.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza. Mradi huu ingawaji Serikali wanajitahidi kuwatafutia maji wananchi wa manispaa ya Morogoro, mradi huu naona unachukua muda mrefu.

Je, una mpango gani wa kuwapatia maji wananchi wa manispaa ya Morogoro wa muda mfupi wakiwa wanasubiria mradi wa muda mrefu? Hasa kwenye kata ambazo hazipati maji kabisa ikiwepo Kora A na Kora B, Mkundi, Amagadu, Rukobe, Kilimanjaro pamoja na mitaa mingine ya Manispaa ya Morogoro.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, mradi wa Furwe, Mikese unahusisha pamoja na vijiji vya *Newland* pamoja na mtego wa Simba. Mradi huu wa maji tayari unawapatia maji wananchi wa Furwe. Lakini mpaka sasa hivi ninavyoongea wananchi wa *Newland* pamoja na mtego wa simba hawajapatiwa maji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maji wananchi hawa wa Newland pamoja na Mtegowasimba?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali. Mheshimiwa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze kwa kazi kubwa sana anayofanya kwanza kuwatetea wananchi wa Morogoro. Sio mara yake ya kwanza kuuliza maswali yanayohusiana na maji katika Mkoa wa Morogoro. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi katika mamalaka yetu ya maji safi na usafi wa mazingira *MORUWASA* imekuwa ikitenga 20% katika kuhakikisha inawapatia wananchi maji kabla ya mradi huu mkubwa nataka nimuhakikishie zipo kazi zinazoendelea sasa hivi tupo katika upanuzi wa miundombinu ya maji katika maeneo ya Kihonda Kaskazini maeneo ya Kilimanjaro na maeneo ya viwandani.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, tuna utekelezaji wa *buster pump station* katika maeneo ya Mkundi lakini pia tuna ujenzi wa mradi mkubwa pale zaidi ya milioni 496 katika maeneo ya Mundu na Kilala hii yote ni katika jitihada katika kuhakikisha tunapunguza tatizo la maji katika Mkoa wa Morogoro. Lakini kwa kuwa mama yangu, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma amekuwa muulizaji mkubwa sana katika suala zima la maji, nimuombe leo tukutane na Katibu Mkuu tuangalie namna gani tunaweza tukasaidia katika maeneo ambayo aliyoorodhesha ili wananchi wake waweze kupata huduma hii ya maji, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Catherine Ruge uliza swali lako.

Na. 278

**Upatikanaji wa Maji Safi na Salama Shirati – Rorya**

**MHE. CATHERINE N. RUGE** aliuliza:-

Mji wa Shirati Wilayani Rorya unakabiliwa na changamoto kubwa ya maji safi na salama licha ya kuwa na umbali wa kilometa 3 tu kutoka Ziwa Victoria. Mji huu ni

moja ya Miji Mikongwe ambapo miundombinu yote ya maji ipo tangu enzi za Awamu ya kwanza, lakini hadi leo hakuna maji licha ya kuwepo na Taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi zinazohitaji sana huduma ya maji?

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Shirati juu ya upatikanaji wa maji safi na salama ili kupunguza ukali wa maisha ambapo kwa sasa dumu moja la lita 20 linauzwa mpaka shilingi 100?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imepata mkopo wenye masharti nafuu wa dola za Marekani milioni 500 kutoka Serikali ya India kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji katika Miji 28 kwa upande wa Tanzania Bara na mradi mmoja kwa upande wa Zanzibar ambapo Mji wa Shirati umejumuishwa. Utekelezaji wa miradi hiyo umegawanyika katika awamu mbili, awamu ya kwanza ni usanifu na awamu ya pili ni ujenzi wa miradi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, Serikali ipo katika hatua ya kuwapata Wataalamu washauri watakaofanya usanifu wa kina na uandaaji wa vitabu vya zabuni kwa miradi hiyo ya maji ukiwemo Mji wa Shirati. Ujenzi wa miradi hiyo utaanza katika mwaka wa fedha 2019/2020. Kukamilika kwa miradi hiyo kutamaliza kabisa tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama kwa Mji wa Shirati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Catherine uliza swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru changamoto ya maji katika Jimbo la Rorya

haliko tu katika Mji mdogo wa Shirati, lakini kwenye maeneo mengi katika Jimbo Rorya, lakini Jimbo hili lina bahati ya kuwa na vyanzo vikubwa vya maji ambavyo ni Ziwa Victoria na Mto Mara. Kuna Kata tatu ambazo ziko karibu kabisa na Mto Mara, ambao ni Kata ya Kisumwa, Leba na Nyabulongo, ni nini sasa Mpango wa Serikali kuwawezesha wakazi wa Kata hizi kupata maji safi na salama kutoka Mto Mara.?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, Shule za mabweni hasa za wasichana zimekuwa na changamoto kubwa sana ya maji na hivyo kuwafanya wasichana kupoteza muda mrefu kutafuta maji na hii imeenda kuwaathiri ufaulu wao, ningependa kuwafahamu ni kwa sasa Serikali haiji na Mpango maalum wa kutatua tatizo la maji kwenye mabweni hasa ya wasichana, kwa sababu wao wana mahitaji maalum kama ilivyokuja na Mkakati wa kutatua tatizo la madawati, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri maji tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikupongeze kwa swali zuri lakini kwa namna unavyowapigania wananchi, lakini kikubwa ambacho ninachotaka kukisema. Amezungumza suala la Vijiji vya Kisumwa kukosa maji ambavyo viko karibu sana Mto, mimi nataka nimuhakikishie sisi Wizara ya Maji ni jukumu letu katika kuhakikisha tunawapatia huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nipo tayari kwenda kujionea hali halisi, ili tuweze kuangalia ni namna gani wataalamu wetu wanaweza kufanya mradi ili kuweza kuwasaidia wananchi hao waweze kupata huduma hii muhimu. Lakini kuhusu suala zima la Mpango kuwapatia watoto katika maeneo ya shuleni, upo mpango huo na ulikuwa ukitekelezwa na wenzetu wa TAMISEMI, lakini kwa sasa huduma zote za maji zimeletwa katika Wizara yetu ya maji. Nataka nikuhakikishie kama Mpango ulivyokuwepo na sisi tutausimamia katika kuhakikisha tunatekeleza na maeneo

hayo ili waweze kupata huduma hii ya maji katika hizo shule, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete uliza swali lako.

Na. 279

**Ahadi ya Kumaliza Tatizo la Maji Chalinze**

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE** aliuliza:-

Wakati wa ziara ya Makamu wa Rais Wananchi wa Halmashauri ya Chalinze walihakikishiwa kuwa maji yataanza kutoka kuanzia tarehe 31 Disemba, 2018 lakini hadi leo hali imekuwa mbaya zaidi kuliko ilivyokuwa mwanzo?

(a) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Chalinze juu ya hali mbaya ya upatikanaji wa maji?

(b) Je, Waziri yupo tayari twende pamoja Chalinze kufanya Mkutano kuwaambia wananchi juu ya hali ya maji katika Halmashauri yetu na lini sasa wananchi wa Chalinze watarajie maji kuanza kutoka kwenye mabomba?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la watu wa Chalinze, majirani zako, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete Mbunge wa Jimbo la Chalinze lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto ya upatikanaji wa hali ya maji katika Jimbo la Chalinze. Katika kuhakikisha changamoto hiyo inatatuliwa, Serikali imeshakamilisha mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji kwa awamu ya kwanza na Awamu ya II. Kwa sasa Serikali inatekeleza mradi wa maji Chalinze kwa Awamu ya III kwa

upanuzi wa mtambo wa kuzalisha maji na mtandao wa usambazaji maji katika maeneo mbalimbali. Katika utekelezaji wa Awamu ya II tayari vituo vya kuchotea maji 96 vimeunganishwa na wananchi wanaendelea kupata maji.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza hali ya upatikanaji wa maji wa wananchi wa Chalinze, Serikali inatekeleza mradi mwingine mkubwa kutoka Mlandizi hadi Chalinze Mboga. Mradi huu utakapokamilika utamaliza kabisa tatizo la maji katika eneo la Chalinze.

Mheshimiwa Spika, nipo tayari kufanya ziara pamoja na Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo la Chalinze na kuwaeleza wananchi mipango mbalimbali ya Serikali katika kutatua tatizo la maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ridhiwani swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri lakini pia na Waziri kwa niaba ya Wizara yao, kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya pale Chalinze. Sina swali lolote la ziada kwa mambo mazuri yanayoendelea kufanyika na hatua ambazo zinachukuliwa, la msingi zaidi nikuombe tu Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na mambo mazuri ambayo mnaendelea kuyafanya nikuombeni muongeze kasi, ili watu wa Chalinze waweze kuona uzuri wa kuwepo Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika halmashauri yao, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana nakushuru, swali la mwisho kwa siku ya leo litaulizwa kuelekea Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Swali la Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena na kwa niaba yake Mbunge huyu wa Morogoro Kusini naomba Mheshimiwa Goodluck nimekuona umesimama Mlinga umuulizie swali lake.

Na. 280

**Matukio ya Ukatili wa Wanyama Nchini**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA (K.n.y. MHE. PROSPER J. MBENA)** aliuliza:-

Kumekuwepo na ongezeko la matukio ya ukatili mkubwa kwa wanyama katika nchi yetu hususan kuku, mbuzi na ng'ombe wakati wakisafirishwa kutoka eneo moja kwenda eneo lingine?

(a) Je, Chama cha kuzuia ukatili wa Wanyama nchini yaani Tanzania *Society for the Prevention of Cluelty to Animals (TSPCA)* kinashirikiana kwa kiasi gani na Serikali katika kudhibiti vitendo hivyo vya kikatili wa Wanyama?

(b) Je, kwa mwaka 2018 na 2019 ni kesi ngapi zinazohusu matukio ya ukatili kwa Wanyama zilifikishwa Mahakamani?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Abdallah Ulega tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena Mbunge wa Morogoro Kusini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inashirikiana na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kama vile *TSPCA* katika kudhibiti vitendo vya kikatili kwa Wanyama kwa kuzingatia Sera ya Mifugo ya mwaka 2006 na Sheria ya Ustawi wa Wanyama ya mwaka 2008 kwa kuelimisha jamii kuhusu masuala ya Ustawi wa Wanyama. Pia elimu inayotolewa inalenga kuelimisha jamii kuhusu njia sahihi ya usafirishaji mifugo, matumizi ya Wanyama kazi kama punda na kuzuia ukatili wa Wanyama kwenye minada ya mifugo. Aidha, jumla ya wataalam wa mifugo 25

kwenye minada wamepata mafunzo na pia wafanyabiashara wa mifugo takribani 300. Pia, elimu hutolewa kwa njia ya mabango na vipeperushi kwenye minada mikubwa.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia Kifungu namba 60, wanaokiuka Sheria hiyo wanatozwa faini ya papo kwa papo badala ya kupelekwa Mahakamani. Faini hiyo ni shilingi 50,000 kwa kila anayekiuka Sheria hiyo. Kwa mwaka 2018 jumla ya makosa 3,542 kwa kosa la ukatili wa Wanyama yameripotiwa ambayo yamegawanyika kama ifuatavyo; ng'ombe 847, mbuzi na kondoo 1,578, Nguruwe 85, kuku 539 na punda 490.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga uliza swali la nyongeza.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ukatili mkubwa wa Wanyama unafanywa pindi Wanyama wanaposafirishwa, tumeshuhudia malori yakipita matani na matani yanatoa ng'ombe Karagwe Kanda ya Ziwa yanapeleka Dar es Salaama.

Mheshimiwa Spika, Sasa kwa nini Serikali isitoe agizo ijengwe Kiwanda huko, ng'ombe zichinjwe ndiyo wasafirishwe wapelekwe Dar es Salaam.? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Swali la pili, ukatili mbaya kuliko wote ni upigaji chapa wa ng'ombe, tumeshuhudia ng'ombe wakiteswa kwa kupigwa chapa, Serikali imeshindwa kubuni mbinu nyingine tofauti na hiyo, Je, Serikali inatoa kauli gani na upigaji chapa wa hovyo kabisa na utesaji wa mifugo yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kweli utesaji wa Wanyama ni tatizo kubwa sana, yaani ukiona kuku wanavyobebwa huko mijini, miguu juu vichwa chini kwenye baiskeli, pikipiki. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kuhusu uteswaji wa Wanyama na nini hatua za Wizara katika jambo hili dunia inatushangaa tunavyowatesa Wanyama.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha tunajenga Viwanda vya kutosha vya kuchakata mazao ya mifugo, na ndiyo maana katika baadhi ambapo mifugo inapatikana kwa wingi kama vile Mkoani Arusha katika Wilaya ya Longido tumefanikiwa kujenga Kiwanda ambacho kipo katika hatua nzuri ya kumalizika na hatimaye kuweza kuchakata mifugo.

Mheshimiwa Spika, rai yake ni kwa nini tusafirishe mifugo kutoka Karagwe na Mikoa mingine kama Kigoma na kupeleka katika machinjio, hali ambayo inapelekea kurundikana kwa mifugo katika magari na hatimaye kuitesa mifugo hiyo. Sisi tutaendelea na jitihada ya kuhakikisha mpaka kule Karagwe Kigoma na kwingineko Viwanda hivi vinaenea. Lakini ndiyo maana Serikali inaendelea kuboresha pia vilevile miundombinu yetu ili kusudi hata hizi hali za ukusanyaji wa mifugo kwa wingi katika magari wakati mwingine ni kwa sababu ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Mkoa wa Kigoma, ile harakati ya ujenzi wa barabara ile, itarahisisha mifugo inayotoka katika Mkoa huo ili iweze kufika katika soko na hatimaye kuwanufaisha wafugaji na wananchi wa Mikoa hii ambayo ina mifugo kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ni suala la upigaji chapa ng'ombe, kwanza naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kuwa tunayo Sheria mahsusi kabisa ya utambuzi wa Wanyama katika Sheria za nchi yetu. Sheria hii inatuelekeza kila ng'ombe lazima atambuliwe na hii ni katika kuhakikisha kuwa tunakwenda sambasamba na mahitaji ya Sheria za Kimataifa ya soko la Kimataifa na nyingenezo.

Mheshimiwa Spika, rai yake ni kwa nini tusitafute njia nyingine mbadala, badala ya kuchoma ng'ombe moto, rai hii ya Waheshimiwa Wabunge tunaichukua na tumeanza kufanya kazi ya kuhakikisha tunatumia teknolojia ya hereni, *earrings* kwa upande wa ng'ombe wa maziwa, kwa kuwa Wabunge wengi wanaonekana kuwa wangependa kuona tunabadilisha utaratibu huu wa kuchoma moto tumelichukua

jambo hili na tutalifanyia kazi kwa ajili ya kuweza kuitekeleza vyema Sheria ile ya utambuzi wa mifugo yetu.

**SPIKA:** Niliwaona Mheshimiwa Dkt. Sware na Mheshimiwa Maige maswali ya mwisho ya nyongeza kwa asubuhi hii.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, ukatili wa Wanyama uko katika jamii zetu, hususani pale kwenye masuala ya migogoro unapokuta hifadhi na wanaovamia hifadhi, basi Wanyama wale unakuta wanapigwa risasi ama wanakatwa mapanga, na pia tunauona ukatili huu katika usafirishaji unapokuta idadi kubwa ya Wanyama hawa wakisafirishwa kwa masafa marefu na wakiwa wamebanwa sana katika yale magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitendo hata cha kuwapandisha kwenye yale magari na kuwashusha ng'ombe wale au Wanyama wale wanakuwa wanapigwa, sasa Serikali inajipangaje katika kusimamia hili kimatendo kwamba dhuluma hizi na ukatili huu kwa Wanyama unakuwa umeisha, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Bado tuko kwenye ukatili wa Wanyama mmejipangaje Wizara, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Abdallah Ulega.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni juu ya ukatili unaofanywa wakati mifugo inapokuwa imekamatwa, katika hifadhi na maeneo mengine, Wizara imeliona jambo hili na nataka nilihakikishie Bunge kuwa Sheria ipo ya haki za Wanyama. Mfugo unapokamatwa, unazo haki zake lazima wapate maji, lazima wapate malisho na watazamwe na hata ikiwezekana wapate na chanjo pia vilevile.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiwasisitiza wale wote wanaokamata mifugo waweze kutekeleza matakwa haya ya Sheria lakini kwa kukazia, tumeona kwa safari hii tunakwenda kuiboresha zaidi Sheria yetu ya Mifugo ya haki

za Wanyama, ili hawa wanaokamata kiholela holela ni lazima wahakikishe kuwa siyo kila mtu anaweza akakamata tu anavyojisikia kukamata.

Mheshimiwa Spika, ni lazima watu wetu wanaohusika na tasnia ya haki za Wanyama, kwa maana ya Maafisa Mifugo kote nchini, waweze kushirikishwa, ili haki za Wanyama wale ziweze kutekelezwa ipasavyo, na jambo la pili ni hili linalohusu mrundikano katika magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba jambo hili linafanywa sana, na wafanyabiashara wetu, lakini labda nikueleze jambo moja na nilieleze Bunge lako Tukufu wafanyabiashara wale huwa tunawasimamisha katika magari, na wakati mwingine tunawauliza kwa nini mnawarundika ng'ombe namna hii, sasa majibu yao ya haraka ambayo watakujibu ni kwamba ng'ombe ukiwaacha bila ya kusimama wakawa wameshikana hivi, mmoja akikaa chini, mathalani, ng'ombe huyo hawezi kufika salama anapokwenda ni lazima atakufa, kwa sababu ya kukanyagwa na wenzake.

Mheshimiwa Spika, sasa haya yote tumeyaona na ndiyo maana tukasema kwamba ni muhimu tuweze kuirekebisha ile Sheria. Na ndiyo maana unaweza ukaona wakati mmoja tulipoona kuwa ng'ombe hawa wanajazwa sana Sheria yetu ya barabara ilileta kidogo sintofahamu miongoni mwa wafanyabiashara wa ng'ombe kwa sababu walitakiwa wahakikishe wale ng'ombe wanapokuwa kwenye magari wasitingishike.

Mheshimiwa Spika, na maana yake wanapotingishika, katika Sheria inaleta tabu kwa upande wa ulinzi wa miundombinu yetu, na hili wamefanya kwa sababu wasitingishike kwa kuona kuwa wanawekwa wengi, sasa unaweza ukaona kwamba tunao wajibu kweli kabisa wa kuangalia Sheria zetu na kuziboresha na naomba niliahidi Bunge lako kwamba hili tunalifanyia kazi na tunatoa wito kwa wale wote wanaosafirisha mifugo wazingatie haki za Mifugo, na siyo kuwapeleka katika uholela.

**SPIKA:** Swali la mwisho Mheshimiwa Ezekiel Maige tafadhali, Oohh! Kuna majibu ya nyongeza Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana, juu ya hili suala la ukamataji holela wa Mifugo na jinsi kama Mheshimiwa Mbunge alivyoliuliza.

Mheshimiwa Spika, nataka kuongezea tu kwamba kwa hivi karibuni baadhi ya Watendaji wa Serikali wamekuwa wakiwaona hata Mifugo na wenyewe ni wahalifu, hawa ni viumbe hai wana mahitaji yao ya msingi ya maji, wana mahitaji yao ya msingi ya malisho, wana mahitaji yao ya msingi ya chanjo na tiba.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, hata wanapokamatwa si wahalifu katika namna yoyote katika makosa yoyote ambayo yanamuhusu mmliki wa mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo baada ya kuona hivyo kwamba ukamataji sasa kila Afisa wa Serikali anakamata Mifugo tukaamua kama alivyosema Naibu Waziri kuboresha Kanuni za Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya mwaka 2008 na Sheria ya magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya mwaka 2003, ambapo marekebisho ya Kanuni ya hizi, yatakuwa tayari ifikapo tarehe 01 mwezi wa saba, ili kuweza kushughulika na hawa Watendaji wa Serikali ambao wamegeuza wameleta manyanyaso makubwa sana kwa Mifugo na Mifugo mingi imekuwa ikifa, ikiwa imeshikiliwa kwa sababu zisizojulikana.

Lakini vilevile, kuwaeleza Watanzania wajue kwamba katika raslimali za Taifa, Mifugo ni raslimali ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa vyovyote vile unapofanya, vyovyote vile unavyofanya unaharibu kama Mifugo ikifa ikiwa imeshikiliwa maana yake kwamba raslimali ya Taifa imekufa ikiwa imeshikiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala hili tunalifanya kwa nguvu zote kuhakikisha kwamba ifikapo tarehe 1 mwezi wa saba, hawa tutashukughulika nao, Watendaji ambao wamekuwa wakitoa kisingizio cha kwamba, natekeleza Sheria anasahau kwamba hata mifugo hawa nao wana Sheria zao zinazowalinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatutakubali tena kama Serikali ifikapo tarehe moja mwezi wa saba badala ya huyu Afisa ambaye anasema kwamba anatumia mgongo wa Sheria tutawashughulikia wao kama *individual* na wala siyo Serikali tena. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Maige.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa kwa nafasi nimesikia majibu ya Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga kwa muda mrefu kimekuwa kikitazamwa kama ni jibu la matatizo yote haya, kwa maana ya kuzuia wafugaji wa Shinyanga wasihame, kwa maana ya kuzuia usafirishaji wa Wanyama na utesaji wa Wanyama na Mheshimiwa Waziri alipofika Shinyanga aliwahakikishia kwamba tatizo la Kiwanda kile ni Mwekezaji na akasema Mwekezaji wa kwanza atakayepatikana kuja kuonyesha nia ya kuwekeza kwenye Sekta ya nyama atamleta Shinyanga, kwa bahati mbaya tumesikia amempeleka Ruvu, wana-Shinyanga wamenituma tumuulize Waziri kwamba wana-Shinyanga tumemkwaza nini, hadi yule Mwekezaji wa kwanza apelekwe Ruvu badala ya Shinyanga kama alivyoahidi mwanzo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana kaka yangu Maige kuliuliza hili swali muhimu sana la kuhusu viwanda hivi. Kiwanda cha Shinyanga ambacho kilikuwa chini ya *Tanganyika Parkers* na kiwanda cha Mbeya, ambacho na chenyewe kilikuwa chini ya Shirika

la *Tanganyika Parkers,* hivi viwanda katika uwekezaji wake si viwanda tu ambavyo vilikuwa huru kuwekezwa.

Mheshimiwa Spika, kiwanda hiki kilikuwa kimebinafsishwa kwa mwekezaji ambaye alishindwa naye pia kukiendeleza. Mkataba wake tukauvunja na baada ya kuuvunja mkataba na baada ya yeye ku-*surrender* hati ile Serikalini, tayari utaratibu wa ukamilishaji wa Serikali unaendelea lakini wawekezaji walioomba kiwanda hicho wapo mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niendelee kuwahakikishia wananchi wa Shinyanga na maeneo mengine, mkakati wa kukifufua kiwanda cha nyama cha Shinyanga uko pale pale na wawekezaji wetu walioomba kuwekeza katika kiwanda hicho wapo. Kwa hiyo, taratibu za Serikali zitakapokamilika basi mwekezaji atapatikana, mwekezaji mahiri ambaye atakiongoza kiwanda hicho.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikijaribu kuondoa zile kasoro zilizokuwa zikijitokeza zamani. Unampa mtu uwekezaji kumbe mwisho wa siku anatafuta mambo mengine. Anatafuta labda ile hati akaende akaweke kupata mikopo kwa ajili ya shughuli zingine. Kwa hiyo, tunataka kweli mwekezaji aliyejipanga vizuri ili tukimpa kiwanda hicho aweze kukiendesha.

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge, mtaona muda wetu wa maswali umeisha. Niende kwenye matangazo haraka haraka ili tuweze ku-*catch up.* Wageni walioko katika jukwaa la Spika, yuko mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa *TUGHIMBE Tailors Company Ltd.* Ndugu Given Ngajilo kutoka Jijini Mbeya. Karibu sana. Karibu sana, sana Mkurugenzi Mtendaji wa Tughimbe *Traders. (Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 11 wa Mheshimiwa Eng. Atashasta Ndtiye, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni wazee wa kanisa la KKKT Usharika wa Kinondoni wakiongozwa na ndugu Sipesito.

Wazee wa Kinondoni, karibuni sana. Karibuni mtuombee. *(Makofi)*

Wageni kumi wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ambao ni familia yake kutoka Arumeru Mkoa wa Arusha wakiongozwa na Mke wake ndugu Anna Pallangyo. Wageni wa kutoka Arumeru karibuni sana. Ahsanteni sana mnaweza kukaa. Kipekee mama Pallangyo Anna naomba usimame, ahsante sana, karibu sana. Jamani ndiyo shemeji yetu huyu. Karibu Dodoma, ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni wengine 189 wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, wageni wengine 189 ambao ni viongozi wa CCM kutoka Mkoa wa Arusha wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa huo ndugu Loata Sanare. Ahsanteni sana wana-Arusha, karibuni sana kutoka Arusha, tunajua mko vizuri na rafiki zangu wanawaona, 2020 Arusha kuchele. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Mkoa ndugu Loata Sanare yuko wapi? Ahsante sana, karibu sana Mwenyekiti hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Mohammed Mchengerwa ambaye ni Katibu wa Chama cha Wafugaji kutoka Rufiji Mkoa wa Pwani ndugu Masanja Ntwale. Masanja karibu sana, karibu popote ulipo. Haya mambo ya ajabu, kutoka Rufiji akina Masanja wanatoka huko? Hawa jamaa zangu wameshaenda nchi nzima hawa. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Mwanza ndugu Joel Oremo na ndugu Justin Kaigi. Karibuni sana popote pale mlipo wale kule juu. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Amina Mollel ambao ni ndugu zake kutoka Mkoa wa Arusha wakiongozwa na ndugu Omary Lumato, karibuni sana ndugu zake, karibuni, wale kule. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa James Millya ambao ni ndugu zake kutoka Mkoa wa Arusha wakiongozwa na Katibu wa CCM wa Wilaya ya Monduli ndugu Langaeli Akyoo. Karibuni sana, Arusha leo imetia fora. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni ndugu zake kutoka Mkoa wa Arusha wakiongozwa na ndugu Neema Kaaya. Karibu sana Neema, yule kule juu kabisa. Ahsante Neema. *(Makofi)*

Wageni 12 kutoka kanisa la *International Evangelism* la Ipagala Dodoma, wageni kutoka Ipagala Dodoma karibuni sana popote pale mlipo na mwisho wanafuzni 80 kutoa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini hapa Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Emma Ngilangwa. Kutoka Chuo cha Mipango wale kule juu kabisa. Karibuni sana vijana wetu. *(Makofi)*

Matangazo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moore kupitia Mheshimiwa Shally Josepha Raymond anawataarifu kwamba kutakuwa na ibada ya misa ya Wakristo Wakatoliki mara baada ya kuahirishwa shughuli za Bunge saa saba mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa ya pili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge, Wakristu wengine wote na wageni mliopo mnaombwa kuhudhuria saa saba mchana pale katika ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa ya pili. Wale wa Ibada za Kikatoliki mnaombwa kufika pale Katibu wenu Shally Raymond anawaomba.

Idara ya Utawala wa Bunge inaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Haroon Mulla Pirmohammed Mbunge wa Mbarali ametoa sadaka ya mchele kwa kila Mbunge. *(Makofi)*

Kama mnavyofahamu kila m waka, mwenzetu ni mkulima kwa hiyo mchele huu unatoka shambani kwake kwa hiyo huwa ana kawaida ya kutugawia kidogo sehemu ya mavuno ya shambani kwake na mchele huu ni *first class.* Huwa anachagua ule bora kabisa, kwa hiyo tunamshukuru

kwanza kwa niaba yenu sana, kwa jambo hili la wema lakini pia kuwataarifu kwamba mchele utaanza kugawiwa kuanzia saa saba mchana leo hapo *basement.*

Hivyo Waheshimiwa Wabunge wote tunaombwa tufike eneo hilo ili kuchukua mchele huo wenyewe pasipo kumuagiza mtu ili kuepuka makosa yaliyojitokeza katika kipindi kilichopita ambapo Waheshimiwa Wabunge walikuta mchele wao ulishachukuliwa. Tunawaomba mjitahidi leo na kesho, kuanzia keshokutwa tunawagawia watu wengine tutajua uhitaji. Kwa hiyo, tunaomba kati ya leo na kesho mjitahidi sana muweze kufika pale na kuchkua mchele wenu. *(Makofi)*

Mwisho kabisa katika matangazo kuna nini tena?

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**SPIKA:** Aaaah! Sawa, sawa. Jamani ligi bado inaendelea ligi ya mpira wa miguu, ligi kuu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mbeleko ya chuma.

**SPIKA:** Kwa hiyo wale ambao bado wanautafuta ubingwa, waongeze juhudi...

**MBUNGE FULANI:** Mbeleko ya chuma.

**SPIKA:** Ligi bado haijaisha, ligi bado. Lakini kwa niaba ya Bunge basi tuwapongeze sana *Simba Sports Club* kwa kunyakua ubingwa wa mpira wa miguu wa klabu za Tanzania kwa mwaka 2019/2020. Hongereni sana Simba. *(Kicheko/ Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mbeleko ya chuma.

**SPIKA:** Lakini pia tunawapongeza sana watani wetu Yanga kwa kufanya juhudi za kuongoza ligi kwa muda mrefu. Na leo hapa mtamuona Mheshimiwa *Chief Whip* wa upande

wa Serikali Mheshimiwa Jenista Mhagama jinsi alivyopiga na ua lake lile ameamua kujilipua,. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge sijui kama huwa mnafahamu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, safari hii amepandisha timu ya Jimboni kwake kutoka kule ilikokuwa sasa wameingia katika ligi daraja la kwanza la msimu unaokuja, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakupongeza sana. Ni jambo kubwa, zito na alikuwa ananiambia kwamba timu zinazoingia ligi ijayo wajiandae. Kila watakapokwenda Ruangwa wajipange. Kwa hiyo, tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, na Waheshimiwa Wabunge basi tuunge mkono michezo katika maeneo yetu tuweze kukuza masuala ya michezo kwa sababu michezo inatusaidia sana kujenga Umoja wa Kitaifa pamoja na faida nyingine nyingi. *(Makofi)*

Mwisho niwataarifu kwamba Bunge *Sports Club* wanaendelea kuratibu ule utaratibu ambao Wabunge tutaenda Misri tukiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Spika mwenyewe wakati tumu yetu ya Taifa itakapokwenda kucheza kwenye *AFCON.* Wanaendelea kuandaa utaribu, tutachangia masuala ya nauli na kadhalika, wanajitahidi sana *TFF* na Baraza la Michezo na Wizara wanajitahidi sana kujaribu kuhakikisha kwamba gharama zile zinakuwa *affordable.* Na ni vyema Wabunge tukaonesha mfano, tukajiandikisha wengi na kwa maana hiyo na Watanzania wengine nao wakafanya hivyo inabidi mipango hii iende haraka kwa sababu *booking* za hoteli kule Misri zitajaa *across* mapema.

Kwa hiyo, itabidi tufanye mapema, tujiandikishe mapema wale ambao tunaenda ili *booking* ziweze kufanyika kwa haraka na kwa kweli Wabunge tukijitokeza kuishabikia timu yetu kule Misri tunaamini itawapa moyo sana vijana wetu na wanaweza kufanya vizuri hata kuweza kunyakua kombe.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Katibu!

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mwongozo wa Spika.

**MBUNGE FULANI:** Sisimami bila kanuni.

**SPIKA:** Haya kwanini ila twende haraka haraka. Tuanze na dawati la Upinzani hapo. Tufanye haraka haraka kwa sababu tuna mambo mengi sana.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kutumia Kanuni ya 68(7) kuomba Mwongozo wako. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora wakati anahitimisha bajeti yake hapa aliwaonya sana Wakuu wa Wilaya wasitumie nafasi zao kuwaweka ndani viongozi...

**SPIKA:** Hilo limetokea hapa kwa Waziri wa Utumishi na Utawala?

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana linaweza likavunja amani.

**SPIKA:** Halijatokea leo.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, naomba...

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea, Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba Mwongozo Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, ni mgeni wa Bunge hili lakini toka Awamu ya Kwanza ianze kuna Mbunge mwenzetu anaitwa Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed amekuwa akitupa

sadaka yake ya mchele ambao mimi nikihesabu ni kama milioni 100 na kitu inayokuja kila mwaka na anatupa sisi Wabunge na watumishi wenzetu.

Mheshimiwa Spika, hivi hakuna namna yoyote ya kumuombea au kumpa heshima Mbunge mwenzetu huyu, hata kwa maombi tu. Tunafanyaje jamani mambo kama haya. Hata kwa kumuandalia hiyo nanihii Mullaa, hakuna namna yoyote kweli ya kufanya jambo hili?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Getere, matumaini yetu ni kwamba kila mmoja wetu anafanya maombi kwa wakati wake. Na kwa kuwa wengi wetu tunaomba kabla ya kula basi unaombea na, nakushukuru sana kwa wazo hilo zuri. Mheshimiwa Amina Mollel. *(Makofi)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Ninaomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) Kanuni ya 47(1)(2) na ikikupendeza Kanuni ya 49(1)(2).

Mheshimiwa Spika, Mtanzania mwenzetu Mbwana Samatta anayecheza soka la kulipwa nchini Ubelgiji ameiwezesha timu hiyo kuchukua ubingwa na Mbwana Samatta ameongoza ligi hiyo kwa kufunga magoli 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kazi nzuri aliyofanya Mtanzania mwenzetu na tumeona wakati ambapo wenzake kule na hasa wenyeji wa kule wakishangilia kwa kutumia bendera ya Tanzania, ni dhahiri kabisa kwamba Mbwana Samatta...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** ... Mbwana Samatta ameitangaza vyema nchi hii kwa mara ya kwanza. Kama nilivyosema kwa kupitia Kanuni ya 47(1)(2) na Kanuni ya 49(1)(2) ikikupendeza, ninaomba basi kupata angalau kauli ya Serikali kumpongeza Mtanzania huyu ili basi kutoa motisha

pia kwa Watanzania wengi kwa sababu wanatarajiwa kurudi hivi karibuni hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi *SECO Sports* wameandika kwamba ni raia wa Kenya. Ninaomba pia kwamba kauli hii Serikali iweze kutoa tamko ili basi angalau wenzetu hawa wasipende kudandia dandia kila kizuri kinachofanyika na Watanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Mollel, tutawasiliana na Serikali tutaona namna gani, ushauri tutakaopata kutoka kwa Wizara ya namna ya kushughulika na jambo hli kwa wakati muafaka. Serikali imekusikia Mheshimiwa Amina, ni jambo la msingi.

Mheshimiwa Mlinga!

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba mwongozo kupitia Kanuni ya 68(7) ambapo mwongozo wangu naomba kupitia swali namba 274 kuhusiana na ufaulu wa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, lazima tuwe wakweli, ukiangalia takwimu za kufeli wanafunzi idadi kubwa ya wanafunzi wanaofeli ni wanafunzi wa kike na wengi wanafeli wakitoka maeneo ya kijijini na ukiangalia sababu kubwa inayosababisha ni kitendo chao cha kutohudhuria vizuri masomo kipindi wanapokuwa siku zao (hedhi).

Mheshimiwa Spika, Bunge hili limekuwa likipiga kelele sana Serikali namna gani itawasaidia wanafunzi kwa kuwapa pedi za kike bure. Tumeshuhudia Serikali na utaratibu wa kutoa vifaa tiba kwa makundi mbalimbali ya wananchi wake ili kuwasaidia kuepukana na magonjwa mbalimbali katika kuboresha afya.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano...

**SPIKA:** Haiwezekani yakawa mambo mawili. Ni moja tu...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, mfano tu.

**SPIKA:** Ni katika hilo hilo moja.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo. Kwa mfano tumeshuhudia Serikali inatoa *ARV* bure kwa waathirika wa *HIV,* wagonjwa wa kifafa wanapewa dawa bure, *TB* wanapata dawa bure, hata *ALU* ile pale kwa takwimu ya kawaida ilitakiwa iuzwe 20,000 lakini inauzwa 2,000.

Mheshimiwa Spika, Serikali inagwa mipira ya kiume bure hadi zahanati za vijijini. Kweli Serikali inawapa kipaumbele wazinifu inaacha wanafunzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa nini Serikali isitoe pedi za kike bure kwa wanafunzi wetu. Naomba mwongozo wako. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Hilo nalo pia limefika Serikalini na kwa wakati muafaka Seriakli itaona namna gani ya kuzungumza na Bunge kuhusiana na mambo haya. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nadhani tuendelee.

Katibu!

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea. Tutaanza na Mheshimiwa Catherine Ruge. Mchangiaji wa kwanza.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niwe mchangiaji wa kwanza siku ya leo kwenye bajeti hii iliyoko mezani, Bajeti ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mifugo na uvuvi, kwangu ni sekta ambayo imenilea, imenikuza na imenisomesha. Kwa hiyo, nitachangia kwa *passion* sana kwa sababu, sekta hii ni sehemu ya maisha yangu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo na Uvuvi inaajiri takribani asilimia 50 ya watanzania, lakini inachangia asilimia 6.9 ya pato la TTaifa, kuliko hata Sekta ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa masikitiko makubwa, sekta hii imepuuzwa na Serikali ya Awamu ya Tano. Kama Serikali itaamua kuwekeza kwenye sekta ya mifugo, uvuvi pamoja na kilimo, tutakwenda kwenye uchumi wa kati, kwa sababu sekta hizi ni *inclusive*, ni jumuifu na zinamgusa kila mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachoshangaa ni kwamba, Serikali imeshindwa kuipa sekta hii kipaumbele, imeenda kuwekeza kwenye maeneo ambayo hayana *impacts* kwa wananchi wengi, na nitakwenda kuthibitisha hili baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imerudisha sekta ya mifugo na uvuvi miaka mitano, sita nyuma, wanasema, historia nishahidi mzuri sana, na leo nitakwenda kutumia hisitoria ku-*substantiate* mchango wangu. Hapa nina hotuba za bajeti tatu, nina hotuba ya bajeti ya mwaka 2013/2014 ya Serikali ya Awamu ya Nne, nina hotuba ya mifugo na uvuvi ya mwaka 2018/2019 na nina hotuba ya bajeti pendekezwa ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa mfano tu vitu vichache, kwa mfano maduhuli ambayo yalipangwa kukusanywa kwenye bajeti ya mwaka 2018/2019 na Wizara hii ya bilioni 18.5 yalikusanywa mwaka 2014 na Serikali ya

Awamu ya Nne, halafu tunasema tunatekeleza, hivi tunatekeleza kitu gani! Mauzo ya mazao ya uvuvi mwaka 2014 yalikuwa dola za kimarekani milioni 832 lakini mwaka 2017 yameshuka mpaka dola za kimarekani milioni 182. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuko *serious* kweli? Tunataka kuwekeza kwenye mifugo? kwenye uvuvi! Naomba niende kwenye bajeti ya miaka hii mitatu muone tofauti kubwa na muone jinsi gani tumerudi nyuma kwenye sekta hii ya mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014 bajeti yote iliyopitishwa na hili Bunge lako ilikuwa bilioni 54.5, mwaka 2018/2019 bajeti yote ilikuwa bilioni 35.3, yaani miaka mitano baadaye, bajeti ya sekta ya mifugo na uvuvi, inapungzwa kwa bilioni 19.2, sawa asilimia 35, ndiyo bajeti ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, ilikuwa bilioni 13.8, mwaka 2018/2019, ilikuwa bilioni nukta tano, yaani Serikali kwa miaka mitano, imepunguza bajeti ya wafugaji na wavuvi kwa shilingi bilioni 8.4. Mwaka 2013 bajeti ya maendeleo ilitekelezwa kwa asilimia 40, mwaka 2018/2019 ilitekelezwa kwa asilimia 43. Yaani *within six years, implementation* ya bajeti ya maendeleo ni asilimia tatu, kwa sekta muhimu kama hii ya uvuvi na mifugo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu tuje hapa tuwasifie, tusifie nini? *This is not a praise and worship team,* hili ni Bunge, tunatakiwa kuisimamia na kuiwajibisha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, njoo kwenye bajeti pendekezwa, mwaka 2019/2020, bajeti hii iliyoko mezani, bajeti yote ni shilingi billioni 64.9, baada ya miaka sita Serikali inaongeza *only 10 billion*, kwenye sekta ambayo inaajiri zaidi ya asilimia 50 ya watanzania, lakini kwenye bajeti ya maendeleo ni shilingi bilioni 13.8, wakati mwaka 2013/2014, bajeti ya maendeleo ilikuwa bilioni 14. Yaani ongezeko la milioni 200

kwa miaka sita, *are we real serious,* kweli tunataka kutoka hapa tulipo, sijui tunakwama wapi!

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye sekta ndogo ya maziwa, mwaka 2013/2014, uzalishaji wa maziwa ulikuwa lita bilioni 1.92, mwaka 2018/2019 ulikuwa bilioni 2.4, ongezeko la asilimia 20 ndani ya miaka mitano kwa maana ya aslimia nne kila mwaka, hakuna *efficiency*, tukubali tu, hakuna *efficiency. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twende kwenye usindikaji sasa, mwaka 2013, viwanda vyetu vilikuwa na uwezo wa kusindika lita 135,000 kwa siku, mwaka 2018/2019, viwanda vyetu vina uwezo wa kusindika lita za maziwa 154,000 kwa siku, yaani ongezeko la lita 19,000 kila mwaka, halafu tunasema Serikali ya wanyonge, wanyonge gani tunaowazungumzia? Wakati huo viwanda vilikuwa 67, sasa hivi tuna viwanda 91, hapa hatuzungumzii wingi wa viwanda, tunaongelea uwezo wa uzalishaji wa viwanda vyetu, *operating capacity*, viwanda vya maziwa vina *operate* kwa asilimia mbili. 98% ya viwanda vyetu vya maziwa vina *operate under capacity,* hakuna *efficiency* kwenye viwanda vyetu. Kwa hiyo, siyo hoja kwa na viwanda vingi, hoja ni uwezo wa uzalishaji wa viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukawa na viwanda vichache, lakini tukaweza kuzalisha zaidi na uzalishaji ukawa na tija. Kwa maana hiyo, asilimia 98 ya mazao ya wafugaji wa nchi hii, hayana soko, na hii imepelekea wafugaji wa nchi hii wameendelea kuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye suala la sekta ndogo ya nyama, na hapa ningependa nimnukuu Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mpina, “Tanzania inaagiza tani 2000 za nyama kila mwaka na wakati huo huo inauza nje tani 2000 za nyama” utaona kuwa kiasi cha nyama tunachouza nje kwa bei rahisi kabisa ndicho kiasi hichohicho tunachoagiza kutoka nje kwa bei ya juu. Natamani kuona wawekezaji wengi wakiwekeza katika sekta hii, kwa sababu fursa zilizopo ni kubwa. Mheshimiwa Waziri,

hapa *issue* siyo kuwekeza kwenye viwanda, viwanda tayari tunavyo, *issue* ni kuhakikisha viwanda vinakuwa na tija, vinakuwa na *efficiency* na vonaweza ku-*operate at full capacity.*

Mheshimiwa Spika, na ningependa, *with due respect my brother,* wakati unakuja kuhitimisha hoja yako, utuambie, ni kwa nini viwanda vyetu vimeendelea ku-*operate under capacity,* vyote vya nyama na maziwa! Pia, ni kwa nini kama nchi tumeendelea kuagiza mazao ya mifugo, uvuvi kutoka nje, wakati tuna viwanda katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tuna viwanda 25 vinavyoweza kusindika maziwa katika nchi yetu na uwezo wake kama vingekuwa vinafanya kazi, kwa uwezo halisi kwa maana ya *full operating capacity*, vingekuwa na uwezo wa kuzalisha lita tani 626,000 za nyama, lakini sasa hivi zinazalisha tani 81,220 za nyama. Kwa hiyo, vinazalisha chini ya uwezo wake kwa asilimia 87.3. sasa halafu tunaongelea kuongeza viwanda, *we don't need quantity, we need quality. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna...

**SPIKA:** Ahsante sana ni kengele ya pili.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Shally Raymond, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana sana kwa nafasi hii ya leo, ambayo kwangu ni muhimu sana, hata nimeahirisha kwenda kufanya *checkup* ya afya yangu. Kipekee namshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai, kwetu sote tuliokaa hapa tuweze kuzungumzia mambo ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha nawashukuru wote waliotupatia sadaka zao, akiwemo Mbunge mwenzetu, lakini

pia wako wale watu wa maziwa jana, tumepata maziwa ya *ASAS*, tumepata maziwa ya Tanga Freshi, asiyejua kushukuru hata hatabarikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Leo nimesimama hapa nizungumzie eneo moja tu la mifugo, na ni eneo la kuku na kuku siyo kuku wote, najikita kwenye kuku wa kienyeji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msanii aliyeimba supu ya kuku wa kienyeji ni tamu sana, hakukosea ni kweli kabisa, toka tunakua, ukimuheshimu mgeni nyumbani, unamchinjia angalau kuku wa kienyeji ili apate kukarimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni takribani mwaka wa nne sasa toka nimeingia Bunge hili na kila siku namfuata Waziri wangu wa Mifugo na Uvuvi nikiulizia vifaranga wa kuku wa kienyeji wanapatikana vipi? Niseme kwamba nimekuwa nikijibiwa, napewa namba za simu na kila ninapopiga, ambako amenielekeza sipati simu, lakini hilo haliniondoi kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri huyu kwa kazi zake nzuri ambazo zimeonekana kitaifa yeye pamoja na Manaibu Waziri wake wote, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara mpaka Madereva wao wanaowaendesha kwa usalama Wizara hii itaweza kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa wanawake, na hata dakika hii ukichukua sensa ya walio huku Bungeni, ukiondoa wale waliomsindikiza Mheshimiwa Mbunge aliyeapishwa, wengi ni wanawake. Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni muhimu kwetu sisi kwa sababu bila Wizara hii hatuna kitoweo na sisi wanawake bila kitoweo nyumbani, hakuna chochote kinachokwenda mdomoni. Ukitaja maziwa, ni kitoweo, ukitaja samaki ni kitoweo, ukitaja kuku ni kitoweo, ukitaja ng'ombe ni kitoweo, ukitaja nguruwe ni kitoweo! Ukitaja yule mkuu wa meza ni kiweo, nitaje kipi ambacho siyo kitoweo, ambacho ni muhimu kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwetu wanawake, siyo tu tunataka kile kitoweo, tunataka kitoweo na ziada ya

kutuingizia kipato. Ingekuwa wameweka mkazo kwenye kuku wa kienyeji, na kila mwanamke mtanzania au kila familia ikafuga kuku, na wale vijana wanaomaliza shule ambao hawajapata ajira wakafuga kuku, leo tungekuwa hatuna uhaba kabisa wa mayai, ambayo ni *protein*, tungekuwa hatuna uhaba kabisa *white meat,* kwa wale ambao hawataki kuongeza uzito, na pia tungekuwa hatuna upungufu wa *protein* popote pale.

Mheshimiwa Spika, lakini kundi hilo limeachwa na kuku hawa hawana kazi kubwa sana kuwalea, hawa ni *scavengers,* wanacharukacharuka tu, mtu akitaka kukuonyesha kwamba una harakati nyingine anakwambia wewe acha mambo ya kuku wa kienyeji. Yeye anachakurachakura huku na huku, lakini kuku hao sasa hivi wanafunikwa, wanafutika, utaambiwa kuna *guchi*, sijui kuna *kuroiler* sijui kuna *crossbreed*, ni lini sasa *gene* hii itatafutiwa utalaam wa kuikuza ili watu wengi zaidi wafuge kuku wa kienyeji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni takribani miaka 58 sasa toka tumepata uhuru, lakini tatizo la ugonjwa wa mdondo bado ni usumbufu mkubwa, bila ya ugonjwa wa mdondo, ule wa *new castle* kwa lugha nyingine, kuku wa kienyeji wangezagaa huku. Niwasifu sana wenzetu wa Singida, ambao kwa kweli ukiuliza kuku hii imetoka wapi, Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa najiuliza, niko hapa natamani wanawake wangu wote wa Kilimanjaro wafuge, kila mmoja awe na kuku wake wa kienyeji hata kama atamfugia chini ya uvungu, lakini mbegu haipatikani, napataje mbegu ya kuku wa kienyeji ili nikasambaze Kilimanjaro, kila mwanamke afuge, kila mwanafunzi afuge nikae kwenye geti la shule niwape vifaranga viwili viwili, wafuge kila mtu na shida ya kitoweo iondoke.

Mheshimiwa Spika, utanishangaa na wengine watanishangaa, kwa nini anang'ang'ana kuku wa kienyeji, gharama za kule kuku wa kienyeji ni kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana atakapokuja kujibu Mheshimiwa Waziri, anieleze, kwa nini wanaruhusu hii kutoa chanjo kwa kuku hawa ikawa ni mtu kutaka na isiwe ni *mass vaccination* ili sasa tufute na tutokomeze kabisa, kwenye mambo yake yake ya kipaumbele nimeyasoma, amesema kwamba natarajia kupunguza na hiyo iko kwenye ule ukurasa wa 13, kudhibiti, lakini naomba atokomeze kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia sana hao kuku wa kienyeji na kila mtu kunielewa shida yangu, na wale wanawake wangu wa Kilimanjaro na kokote wanawake wapo, naomba sasa nije kwenye kuwapa miradi vikundi vya akina mama popote walipo.

Mheshimiwa Spika, tukisema mitamba, mtamba mmoja mzuri anakwedna mpaka shilingi milioni moja, hatuwezi wanawake sisi. Nakwenda kwenye ng'ombe sasa, ili ng'ombe tumpate, tumfuge, tupate maziwa, tupate samadi ya kwenye mashamba yetu na kila mahali. Nilikuwa naomba Serikali, kwa vile Serikali yetu ya Awamu ya Tano ni sikivu na inapenda sana pia kutekeleza mambo ya Mwalimu Nyerere, irudi upya, kusambaza mitamba kama Mwalimu Nyerere alivyosambaza mitamba kwenye ile awamu ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, endapo tutafuga vizuri, tukakopeshwa mitamba, kopeshwa ng'ombe lipa ndama, tutaweza tena kuibua mbegu mpya ya mitamba mizuri yenye maziwa mengi, kuliko hii tunayofanya sasa hivi, wamesha *crossbreed* mara nyingi sana wenywe kwa wenyewe, na pia unakuta maziwa yanayopatikana sasa ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo, nimeona, kwenye kitabu tumeelezwa kwamba idadi kubwa imeongezeka kwenye *artificial insemination*, lakini basi ningeomba, hiyo *artificial insemination* ifanyike bure, tuwazalishie watu bure. Mwingine ng'ombe anapata joto anakuta hana hela ya kwenda kulipa, sasa hiyo inapoteza tena, anapoteza muhula mmoja wa kuendeleza au wa kuzalisha ng'ombe. Nilikuwa naomba sana, kama

Mheshimiwa Waziri atanielewa ninalowaombea watu wangu wenye uwezo mdogo, tupate...

**SPIKA:** Malizia Mheshimiwa Shally.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naunga hoja mkono asilimia 100, ahsante sana Spika wangu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango wako mzuri sana kwa mchango wako mzuri sana natumaini Mheshimiwa Waziri atatupa ufafanuzi, hasa mahali gani zinapatikana mbegu za kuku wa kienyeji na chanjo zake, maana yake kwa kweli hata sisi tunawatufuta sana, hiyo mbegu iko wapi. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma nilishakutaja, atafuatia Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye bajeti hii ya mifugo pamoja na uvuvi. Kwanza nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri wanayoifanya, pia na Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Mpina, Mheshimiwa Ulega, Naibu, Katibu Mkuu Prof. Elisante, pamoja na Katibu Mkuu wa Uvuvi, Tamatama.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kuwa, Wizara ya Mifugo, pamoja na Uvuvi, inajitahidi ninapenda kuwapa pongezi kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Licha ya bajeti kupungua pungua au kufanya nini, lakini wanajitahidi sana kwa kazi nzuri wanayoendelea nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwapongeza, naomba niongelee kwenye bajeti ya maendeleo, ni kweli, bajeti ya maendeleo imeshuka, imeshuka kwa asilimia 40. Kwa hiyo, nashauri kuwa, hiyo fedha ndogo mnayoipata na kuwa wasiwasi na hiyo miradi ya maendeleo itatekelezwaje kwa hiyo fedha kidogo bilioni tano, naomba sana, tena sana hiyo fedha itakayotolewa, iweze kutekelezwa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *operations* za uvuvi, *operations* za uvuvi zimekuwa zikiendeshwa hapa nchini, Pwani, Kanda ya Ziwa, Tanga, pia hiyo ni Pwani pia. Lakini tunaweza kukutana na wavuvi, kwa kweli *operation* ni nzuri, naipenda, ni nzuri na Serikali inaipeda, kwa sababu inainua kipato, hao samaki wanaweza kuzalia kwa sababu *operation* hiyo inasaidia samaki waweze kutaga vizuri, kuliko waweze kuvuna samaki wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mpina nilikuwa nashauri elimu endelee; kabla ya kuchoma nyavu za hao wafugaji waweze kupata elimu ya kutosha ya ni saizi gani ya matundu inayotumika kwa samaki, dagaa, kwa samaki sangara, kwa samaki terapia? Ni aina gani na ni wapi wanapatikana? Swali linakuja, je, tukishazichoma hizo nyavu wale wanaoleta nyavu hapa nchini wanafanywaje? Nilikuwa naomba pia waweze kulifuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna migogoro ya ardhi na watumiaji ardhi. Hii migogoro ya ardhi inatokana na; kwa mfano kwa upande wa wafugaji na wakulima, nina mfano kidogo; juzi juzi pale Ulanga mifugo imeingia kwenye shamba la mpunga pale Nakafulu, wamekula mpunga wote wamemaliza. Kwa hiyo nilikuwa nashauri kuwa mikakati iwepo ya kuwaeleza kuwa wafugaji na wakulima waheshimiane ili migogoro iweze kupungua.

Mheshimiwa Spika kuna mikakati inayoendelea ambayo imepangwa na Serikali, naomba hiyo mikakati iweze kutimilika isiwe mikakati tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Malisho.Tatizo hili la migogoro linaletwa na malisho. Nikisema malisho ya mifugo naamanisha mikunde pamoja na nyasi. Mtoe elimu ya jinsi ya kustawisha hayo malisho (shamba darasa).

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri kuwa haya mashamba darasa yawe kwenye kila kata, hasa kwenye mikoa ile ambayo ni ya wafugaji, ili waweze kujua ni malisho gani na jinsi ya kustawisha hayo malisho.

Mheshimiwa Spika, vilevile tatizo lililopo ni mbegu; mbegu za malisho hazipatikani kwa urahisi. Kuna wakulima wafugaji ambao wanatafuta mbegu lakini hazipatikani madukani. Ningeliomba Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri hizi mbegu ziweze kupatika mashambani kusudi Maafisa Ugani waweze kufanya kazi yao ya kuwaelimisha hawa wafugaji jinsi ya kustawisha haya malisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Ufugaji wa Kisasa. Ni kweli mifugo iko mingi, iko hata hapa Dodoma, iko Manyara, iko Mwanza, na iko kila mahala. Hata hivyo ninaishauri Wizara kuwa ule mpango mkakati mliouweka naomba ufuatwe ili tuweze kufuga kwa kisasa na tuweze kupata mazao mema mazuri kutoka kwenye mifugo yetu. Mifugo tukiiendeleza vizuri tunaweza kupata kuinua kipato chetu pamoja na lishe kutokana na mifugo. Kwa hiyo nilikuwa nashauri jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, Vyakula vya Mifugo Hasa Kuku. Ni kweli kuwa tulitoa tozo na ada tulipunguza kwenye vyakula vya kuku hapa Bungeni. Hata hivyo, licha ya kupunguza hizo tozo na ada tatizo bado liko palepale kwenye vyakula vya kuku. Akina mama na vijana wangeweza kweli kufuga kuku, lakini wanapata tatizo kwa sababu vyakula vya kuku bado viko juu. Najua Mheshimiwa Waziri utaweza kuniambia kuwa watumie malighafi inayozalishwa hapa nchini. Ni kweli, nimefanya utafiti, viwanda hivi ni vya hapa nchini, vinazalisha chakula cha kuku na vinatumia malighafi inayozalishwa hapa nchini lakini bado chakula kiko juu. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba ulifanyie kazi kusudi wanawake, vijana, na wakulima wengine waweze kuendelea kwenye tasnia hii ya ufugaji wa kuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tozo kwenye Sekta hii ya Mifugo imekuwa kubwa na nyingi lakini nashukuru na naipongeza Serikali. Kwenye hotuba ya Waziri amesema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kabla sijamaliza naunga mkono hoja, lakini uvuvi wa *aquaculture*, naomba utiliwe mkazo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA**: Ahsante sana Dkt. Christine Ishengoma, nakushukuru sana. Nilishakutaja Mheshimiwa Rhoda Kunchela, utafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf Hussein, na Mheshimiwa Joseph Mkundi ujiandae.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu pia naunga hoja maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tuna mifugo ya takribani zaidi ya milioni 30.5 kwa takwimu zilizotolewa na Wizara ya Uvuvi na Mifugo kwa mwaka 2017/2018; na Tanzania ni nchi ya tatu kwa kuwa na mifugo mingi katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa takwimu hizi hazioneshi uhalisia wa Watanzania kunufaika na wingi wa mifugo. Kwa hiyo changamoto zilizopo kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi; nadhani sasa Waheshimiwa Wabunge wameeza kwa upana wake; changamoto tulizonazo ziko wazi. Tunakosa viwanda kwa ajili uzalishaji; Waheshimiwa Wabunge wameongelea masuala ya uzalishaji wa nyama, maziwa, pia viwanda vya ngozi. Tuna changamoto za kukosa sera na kanuni ambazo zingeweza ku-*support* tukapata ubora wa bidhaa, tukaweza kuuza ndani ya nchi na kupata masoko nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunapata changamoto kwa kutokupata sera na kanuni ambazo zingewezesha wawekezaji kwenye Sekta Binafsi, wangeweza kuwekeza na tukapata viwanda na tukapata bidhaa ambazo zingeweza kulinufaisha taifa.

Mheshimiwa Spika, niongelee kwa kifupi, Mkoa wa Katavi tuna changamoto kubwa ya migogoro ya ardhi, na tangu mwaka 1961 tulikuwa na hifadhi moja tu; lakini kwa

sasa tunahifadhi za kitaifa zaidi ya tano. Sasa unaona tatizo la migogoro ya ardhi, kwa maana ya wafugaji kukosa maeneo ya malisho ni kutokana na Serikali kuendelea kuchukua maeneo tengefu, pia kuendelea kuchukua maeneo kwa ajili ya kutenga maeneo ya hifadhi. Kwa hiyo kama Serikali ikiendeela kutenga maeneo haya, kuchukua maeneo ya wananchi ambao kwa sehemu kubwa walikuwa ni wafugaji wakaweka hizo hifadhi, sasa hawa wafugaji wetu wanakwenda wapi? Ndiyo maana unaona wanasambaa kwenye mikoa mbalimbali, wanaenda kuvamia maeneo ambayo mengine ni maeneo ya wakulima, makazi na maeneo mbalimbali. Kwa hiyo Serikali, kwa sababu tuna eneo kubwa la misitu ione namna ya kuweza kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji, ili kuondoa migogoro hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo kuhusiana na Mkoa wangu wa Katavi. Kumekuwa na mauaji ya kipuuzi kabisa yanayoendelea; na ni nimseme tu kwa kifupi Mkuu wa Wilaya ambaye anajiita ni Muhando katika Wilaya ya Mpanda Vijiji, kwa maana ya Tanganyika, amekuwa anatumia ubabe ambao kimsingi ni unyanyasaji ambao unaendelea kwenye taifa na watu hawana sehemu ya kusemea.

Mheshimiwa Spika, ukihitaji nikupe *CD* ya mauaji ambayo yametokea katika Kijiji cha Lyamgoloka, ni hii hapa. Wananchi wamepigwa risasi, watu wanachomewa nyumba, mifugo inapigwa risasi, watu wanapigwa hawaelewi hatima yao ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa taifa hili mnalosema ni la wanyonge ni kwa nini Serikali hii ya Awamu ya Tano inakaa kimya? Ni kwa nini mnashindw ku-*solve* migogoro ambayo inaendelea katika Jimbo la Mpanda Vijijini? Na hawa askari wa wanyamapori ambao wengine wamekuwa si waaminifu wanapora ng'ombe, ng'ombe wanapigwa risasi. Ni kwa nini Serikali hii inashindwa kutatua migogo hii?

Mheshimiwa Spika, na huyu Mkuu wa Wilaya amekuwa sasa ana kashfa nyingi na wananchi wa Mpanda

Vijiji hawamtaki kutokana na kero na matatizo ambayo yanaendelea kwenye hili. Vijiji ambavyo vimeathirika kutokana na Mkuu huyu wa Wilaya ambaye sasa anajifanya ni Mungu mtu kuna Kaseganyama, Mnyamasi, Karema, Ikole, Isengule, Kapalamsenga pamoja na Vijiji vya Iseganyama.

Mheshimiwa Spika, watu wanaishi kama wako porini, ni kwa nini Mkuu wa Wilaya anafanya matendo ya kinyama, anaamlisha Askari wa wanyamapori pamoja na Polisi kwenda kuwapiga wananchi; leo watu wanaishi kwenye mahema, watu hawaelewi hatima yao ni nini. Hivi leo wafugaji wamekuwa wanaishi katika mazingira ambayo hawaelewi hatima yao ni nini halafu mnasema nchi ni ya amani?

Mheshimiwa Spika, ninaomba Waziri atakapokuja kuhitimisha aeleze ni namna gani atatatua mgogoro na huyu Mkuu wa Wilaya Muhando sisi hatumtaki, wananchi wa Jimbo la Tanganyika hawamtaki kwa sababu tangu ameingia katika Mkoa wa Katavi amekuwa ni kero na hana suluhisho katika migogoro ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, niongele masuala ya tozo; bado iko pale pale. Halmashauri ilitenga kwamba wafugaji wanapoingiza mifugo kwenye maeneo ambalo si sahihi, kwa maana ya hifadhi watozwe shilingi 50,000 kwa mara ya kwanza, kwa pili wanatozwa shilingi 100,000 na kuendelea. Sasa fedha hizi watu wamekuwa wanatozwa zaidi ya 100,000. Ng'ombe mmoja akiingia kwenye chanzo cha maji wanalipishwa mpaka milioni moja; sasa hizi pesa zinakwenda wapi?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rhoda tunakushukuru sana.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, bajeti hii ya mifugo na uvuvi leo imeongozwa uchangiaji na akina mama wanne kwa mfululizo; inaonekana wadau wakubwa wa mifugo na uvuvi ni akina mama. Sasa tuwasikie akina baba kidogo. Mheshimiwa Yussuf utafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mkundi.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kwa kupata nafasi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa masikitiko makubwa, na naomba katika hili utusaidie. Juzi nilimpa tatizo hili kabla ya kuwasilisha hotuba yao jana Mhehsimiwa Naibu Waziri kilio cha Wazanzibar kuhusiana na usafirishaji wa dagaa. Wazanzibar wanasafirisha dagaa kutoka Zanzibar kupeleka Congo, wana vibali vyote kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kusafirisha, lakini wanapofika ndani ya Tanganyika Tunduma wanakamatwa, wakishakamatwa dagaa wao wanazuiliwa wanalipishwa faini ya milioni mbili kila mtu mmoja na gari inapigwa faini ya milioni kumi; *evidence* zote hizo nimempa Mheshimiwa Naibu Waziri kabla ya kuwasilisha hotuba yao jana. Kama hilo halitoshi wanawekwa ndani wanapouliza kwa nini, sisi tuna vibali, hii ni *transit* tu tunapita kwa nini tunakamatwa? Wanawekwa ndani. Kuna msafirishaji anaitwa Ameir maarufu Mchezo amewekwa ndani kwa kuuliza swala hilo, kuna huyu *agent* wao pale Tunduma anaitwa Kibona amewekwa ndani kwa kuuliza swali kama hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaposema sisi Wazanzibar kuhusu masuala haya tunaambiwa tunasema maneno ya uchochezi. Mmetuzuilia sukari tusilete hapa tumenyamaza, mmetuzuilia maziwa yasiletwe hapa tunanyamaza, basi hata kupita? Kwa kweli hili linaumiza sana; na huu ni mwezi wa Ramadhan sitaki kusema sana lakini ni kitu kinachoumiza sana.

Mheshimiwa Spika, mimi nimwambie, na nilisema katika Bunge hili, kwamba Serikali ya Awamu ya Tano hii kuanzia Mheshimiwa Rais na Mawaziri hawa wanafanya kazi

vizuri sana, wanakwenda mbio sana Mawaziri hawa kutatua changamoto hizi, lakini hapa katikati hapa ndipo penye matatizo, mpaangalie. Sasa hata magari yanakamatwa, kwa mfano kuna magari tisa yamekamatwa Mbeya yamepelekwa Tunduma; huko Tunduma kuna nini? Kwamba gari imekamatwa Mbeya, kama ni watu wa *Fisheries* wako pale, kama ni watu wa *TRA* wako pale lakini yapelekwe Tunduma, kuna nini huko?

Mheshimiwa Spika, sasa Wizara inajisifu imekusanya makusanyo mengi sana zaidi ya mpango wao kumbe ni dhuluma, maana hii mimi ninaiona kuwa ni dhuluma; Inauma, inauma, inauma kweli kweli. Tunaomba yale mambo wanayofanya hawa ndugu zangu hawa wa Kinyamwezi, yaani kila mnapotugusa sisi tunanyamaza, tunawaangalia tu; mnatugusa na hapa tunanyamaza tunawaangalia tu, tunataka ushahidi kamili.

Mheshimiwa Spika, naomba hili utusaidie; hawa ni watani wangu; we tulia wewe. Naomba niendelee. Naishauri Serikali katika suala la uvuvi wa bahari kuu. Kuna meli nyingi sana zinazokuja kuvua katika bahari yetu. Niko katika uwekezaji kandokando ya barabara Ukanda ule wa Kaskazini ya Pemba.

Mheshimiwa Spika, meli nyingi sana zinakuja zinafanya *fishing, diving*, na *snorkeling* lakini hakuna kazi yoyote, hakuna utaratibu wowote unaopatikana. Wakati huo huo Zanzibar inataka kusajili meli kwa ajili uvuvi kuna tatizo hili la kodi ambalo wamewekewa inakuwa ni tata.

Mheshimiwa Spika, tunaomba, kama sisi hatuwezi kulinda bahari yetu nani atatulindia? Na shida iliyopo hawa Askari wetu wa *Marline Park,* hawa wanaofanya, hawawezi kuzifikia, zile meli, zile meli ni kubwa vyombo walivyonavyo wao kuwafikia wale ni vyombo vidogo. Kwa mfano iko siku moja watu wa *TRA*, *ZRB* na *KMKM* walienda na *fiber boat*, kuna meli ilikuwa inavua karibu sana na Manta Resort zote wakaenda. Walipokaribia wale waliwaambia tu huko huko mliko ishieni huko, waliwatangazia kwa spika lao kubwa lile

wakafanya ubishi wakaenda. Ile meli ilizungushwa tu wale karibu wazame, kwa sababu kile ni ki-*fiber boat* na lile ni wimbi la kuzungusha meli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuiombe Serikali katika suala hili lazima tujipange. Watu wanatoka huko, wanakuja Tanzania kwenye bahari yetu wanavua wanaondoka na samaki halafu samaki hao hao wanarudi tunakuja kuuziwa tena hapa hapa. Katika hili hatujajipanga; hii bahari ni rasilimali moja moja kubwa sana na ambayo inatuletea tija kubwa sana kama tutajipanga lakini bado hatujawekeza vya kutosha. Niiombe Serikali iwekeze vya kutosha katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, achana na hapo sasa, hiyo ni bahari kwa upande huu wa Magharibi, lakini sasa nenda upande wa Mashariki ya bahari yetu. Kule kwetu sisi kuna upande wa Mashariki wa vile Visiwa, sasa hapo ndipo utaona meli ambazo zinavua haswa. Hizo meli kubwa zinakuja, zinavua kwa mwezi mmoja kisha zinaondoka; hakuna kule kwa sababu hata hizo *fiber bolt* haziwezi kwenda.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

**SPIKA:** Ahsante sana, nilishakutaja Mheshimiwa Mkundi, utafuatiwa na Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata fursa hii ya kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Mchango wangu utakuwa zaidi kwenye eneo la uvuvi, na hii ni kwa sababu ninatoka Ukerewe; na Ukerewe inaundwa na Visiwa. Katika eneo letu *square kilometer* 6,400 zaidi ya asilimia 90 ni maji. Katika idadi ya watu tuliyonayo 400,000 na sehemu zaidi ya

asilimia 95 wanategemea zaidi uvuvi; kwa hiyo mchango wangu utajikita zaidi kwenye eneo la uvuvi.

Mheshimiwa Spika, uvuvi na mifugo unachangia sehemu kubwa ya Pato la Taifa. Ninaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kulinda rasilimali za nchi hii ili ziweze kuwasaidia Watanzania kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na operesheni ambazo zimekuwa zinaendelea kwenye maeneo mbalimbali kwenye uvuvi na mifugo; lakini kwenye eneo la uvuvi operesheni hizi zimekuwa na madhara. Binafsi nimekuwa muumini mkubwa sana wa uvuvi endelevu na nimekuwa ninaunga mkono operesheni hizi kwa dhamira ya kulinda rasilimali zetu; lakini madhara kadhaa ambayo yamekuwa yanasababishwa na operesheni hizi nimekuwa siku zote sikubaliane nazo.

Mheshimiwa Spika, tunafanya mambo haya, tunatengeneza sera, tunatunga sheria, tunafanya operesheni hizi ili kulinda rasilimali lakini wakati huohuo tukihakikisha kwamba maisha ya wananchi wetu kule chini hayaathiriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa zimefanyika operesheni hizi, bahati mbaya sana hapo nyuma tulikuwa na dada mmoja ametajwa jana anaitwa dada Judith, alitusababishia madhara makubwa sana kwenye eneo la Ukerewe, amepelekwa Kigoma kule. Sasa operesheni hizi niombe sana Wizara, kwa mfano kule Ukerewe kwenye Jimbo langu wananchi wengi wameathirika na operesheni hizi. Wamedhulumiwa, wamenyanyaswa, wamechomewa nyavu zao.

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo kubwa linalonisumbua mimi, tunafanya operesheni hizi lakini mbadala wake ni upi? Kwa sababu tukumbuke sehemu Kama Kanda ya Ziwa *specifically* kwa Ukerewe zaidi ya asilimia 95 ya vijana wameajiriwa na kujiajiri kupitia uvuvi. Kwa hiyo unapovuruga mfumo wote wa uvuvi *automatically* unaathiri maisha yao lakini unaathiri vilevile maisha ya ujumla ya kiuchumi ya Visiwa

vya Ukerewe kwa sababu kila kitu kiuchumi kinategemea shughuli za uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna marekebisho ya sheria kwa mfano kwenye nyavu zitakazotumika kuvua dagaa. Nimewahi kusema hapa dagaa hawavuliwi kwa kunyoosha wavu kwamba wale dagaa wanase kwenye wavu ndio uwakusanye hapana, dagaa wanavuliwa maji marefu tena kwa kuchotwa, sasa kule tulikuwa tunatumia nyavu za milimita sita, wameleta milimita nane mpaka milimita kumi inakuwa ni hasara kubwa sana kwa wavuvi wetu wanaoafanya shughuli za uvuvi hususani uvuvi wa dagaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nashauri; la kwanza, badala ya kuweka vikwazo kwenye uvuvi huu kwa ku-*limit* saizi za nyavu jambo ambalo linaathiri sana wavuvi wetu, kwa sababu mvuvi tuchukulie gharama anazoingia kwenda kuvua ni kubwa sana, halafu tuchukulie anatumia mafuta ya taa, anatumia petroli bado kuajiri wale watumishi anatumia zaidi ya shilingi 300,000 au shilingi 400,000 kwa siku halafu kwa kutumia nyavu za milimita kumi anapata dagaa sijui thamani yake shilingi 30,000 au shilingi 40,000 bado kuna kodi nyingi anapaswa alipe tunakuwa hatuwatendei haki wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo badala ya ku-*limit* saizi za nyavu, nishauri Wizara iangalie uwezekano wa kufanya uvuvi wa msimu, kwamba kuanzia mwezi fulani mpaka mwezi fulani kusifanyike uvuvi, baadaye mwezi fulani na kuendelea uvuvi ufanyike. Mbaya zaidi tunaweka *limitation* hizi kwenye maeneo yetu, wenzetu majirani zetu Kenya, Uganda wanaendelea na shughuli za uvuvi, samaki hawako eneo moja, tunapowazuia hapa leo wanahama wanaenda Kenya, wanaenda Uganda na Congo wenzetu kule wanawavua wale samaki. Kwa hiyo tunawasababishia umasikini wananchi wetu kwa faida ya majirani zetu, kwa hiyo ni muhimu sana Wizara iliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiachilia mbali eneo hili la uvuvi wa dagaa sijui na vitu gani, tumeweka saizi za nyavu, tukumbuke kuna *species* nyingi sana za samaki ziwani, kuna samaki wengine ambao ukiweka wavu wa milimita tatu, kuna samaki wengine wadogo ambao hawakui kufikia kiwango hicho, sijui mmefanya *research* kwa kiwango gani. Tukumbuke *ecological disaster* kwenye Ziwa Victoria imesababishwa na upandikizaji wa sangara kwenye ziwa lile. Kwa hiyo katika *species* zilizokuwepo zaidi ya 500 nyingi zimepungua kwa sababu samaki wengi wanatumika kama chakula na wanaliwa na sangara. Sasa tunawalinda sangara, hawa samaki wengine tunatumia mfumo gani kuwalinda, matokeo yake tunawaadhibu wananchi kwamba wasivue samaki wale kwa sababu tu kwamba wanapungua kitu ambacho wanaliwa na sangara, sasa hatuwatendei haki wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Ukerewe kila wakati wananisumbua wananipigia simu bwana tunazuiliwa kuvua ngere kwa sheria ipi, kwa utaratibu upi? Tunazuiliwa kuvua furu kwa utaratibu huu, kwa sheria ipi? Kwa hiyo niombe Wizara itoe tamko la kuruhusu uvuvi wa ngere na furu, kwa sababu kupungua kwao ni kwa sababu wanaliwa na sangara. Ningu kwa mfano tunavua kwa nyavu zipi? Kwa hiyo niombe Wizara iliangalie jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa operesheni hizi kama nilivyosema awali, wananchi wengi sana walinyang'anywa mali zao, wamenyang'anywa mashine, nyavu zimechomwa, mitumbwi imeharibiwa mpaka leo mashine zile za wavuvi ambao wamehangaika kweli kwa jasho na damu kupata mashine zile zimeshikiliwa kwenye vituo mbalimbali. Niombe Mheshimiwa Waziri atoe tamko wananchi wetu vifaa vyao vile waweze kupewa ili waendelee na shughuli zao za uzalishaji mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafanya yote haya lengo ni kulinda rasilimali, lakini tuimarishe uchumi wa wananchi wetu. Tunaweza kuimarisha uchumi wa wananchi wetu tunapochoma nyavu, tunawapa njia mbadala, tumekuwa

tuna- *encourage* uvuvi wa vizimba, je, tunapata faini, tunakusanya mapato, tunarudishaje pesa hizi kuweza kuelimisha vijana wetu kujifunza namna ya uvuvi wa vizimba? Bahati mbaya uvuvi huu wa vizimba ukianza kufuatilia kwa mfano ukitaka kuweka vizimba vyako kuna taratibu nyingi mno, kuna tozo nyingi mno zaidi ya sita, saba, sasa kwa mtu wa kawaida kuvuka vikwazo vyote hivi ni ngumu sana na gharama ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, leo hii kwa mfano nikiuliza kwa Mheshimiwa Waziri hapa leo wanipe kama wana *database* wanipe orodha ya maeneo ambayo yana sifa za kuweka vizimba kwenye maeneo mbalimbali. Kwa mfano, waniambie kwamba Ukerewe ni eneo lipi ambalo wameainisha, wamefanya *research,* wakaona kwamba eneo moja, mbili, tatu yanafaa kwa ajili ya uvuvi. Kwa hiyo, mtu anapotaka kufanya uvuvi huu anaanza kuhangaika hatua moja baada ya nyingine, vikwazo vingi hatimaye sasa hata ile dhamira yake inakuwa imepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana kama nilivyoshauri mambo matatu ambayo ni muhimu sana. La kwanza, Mheshimiwa Waziri kama nilivyosema aruhusu, atoe tamko, vifaa vilivyokamatwa vya wavuvi warudishiwe ili waendelee na shughuli zao, lakini watoe tamko la...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Felister Bura atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ya siku ya leo kwa uhai na baraka tele

katika maisha yetu. Nina mambo machache ya kuchangia; la kwanza, niipongeze Wizara kwa kazi nzuri ambayo tumesoma kwenye bajeti yao na kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nimshukuru kwamba sasa hivi wamekubali kukata vitalu kwa ajili ya wafugaji ambao wanazunguka maeneo ya *ranch*.

Mheshimiwa Spika, kwetu Dodoma tuna *ranch* ya Kongwa na wananchi wanakwenda pale kwenye vitalu vile kwa ajili ya ufugaji, lakini kitu ambacho naona ni kigumu kwa wananchi wangu ni kulipishwa ng'ombe mmoja Sh.10,000 kwa mwezi. Naona gharama hii ni kubwa sana, kwa sababu *ranch* wanapoingia hakuna majani ambayo yamepandwa na watumishi wa *ranch*, hakuna dawa ambayo wanapewa mifugo wanaoingia katika vitalu vile. Kwa hiyo ukisema kwamba mfugaji mmoja ana ng'ombe 50 tu na ng'ombe 50 kwa Dodoma ni ng'ombe wachache sana, ng'ombe 50 kwa mwezi akiingiza kwenye kitalu cha *ranch* ni Sh.500,000 kwa mwezi mmoja.

Mheshimiwa Spika, niiombe Wizara ione namna ya kupunguza bei hii ambayo ni kubwa katika vitalu vyetu ili kuwasaidia wafugaji. Hawana maeneo ya kuchunga ng'ombe, hawana maeneo kabisa na wanapomtoza mfugaji shilingi 10,000 kwa ng'ombe mmoja, akitoka pale hana pa kuuza maziwa, Dodoma hatuna kiwanda cha maziwa mpaka uende Arusha au mpaka mfugaji apeleke maziwa Iringa, kitu ambacho ni kigumu na ni gharama sana kwa mfugaji.

Mheshimiwa Spika, mbali ya hivyo wangetoa elimu wa wale ambao wanafuga katika vitalu vyao, hakuna elimu yoyote inayotolewa kwa wale wafugaji ambao wanafuga kwenye vitalu vya *ranch* na wanashindwa kununua mitamba ile, bora wangeruhusu mitamba ya *ranch* ikapanda ng'ombe za shilingi 1,600,000. Sasa mfugaji achunge ng'ombe kwenye kitalu Sh.10,000 kwa mwezi kwa kila ng'ombe, lakini akitaka mtamba anunue kwa Sh.1,600,000, sio haki. Naomba sasa Wizara iangalie namna ya kusaidia wafugaji wanaoingia kwenye *ranch* ambao wamekodi vitalu kwa bei ndogo, lakini wapate elimu na zaidi ya elimu wakubaliwe mitamba ya

*ranch* iwapande ng'ombe wa wale ambao wako kwenye kitalu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la chuo chetu cha *TARILI* cha Mpwapwa chuo hiki ni cha siku nyingi, ni chuo cha zamani, kinazalisha wataalam wazuri na kimepewa eneo kubwa sana na Serikali ya Wilaya ya Mpwapwa, lakini hawana vifaa, watumishi vibarua wa pale hawalipwi, waliokuwa wanashuhgulika mashambani kulima na kupanda majani kwa ajili ya ng'ombe walikwishaacha kazi, wala haki zao hawajalipwa. Hata hivyo, vibarua waliopo kuna vibarua 70 pale, nadhani wapo zaidi ya 70 hawajawahi kulipwa. Niombe kama kweli chuo kile ni cha thamani kwa Serikali yetu, kama chuo kile kina manufaa kwa nchi yetu, Serikali ione namna sasa ya kukisaidia kile chuo hata vifaa hawana, wanatakiwa kulima na kupanda mazao kwa ajili ya ng'ombe wale wanaowafuga pale na ng'ombe wa Mpwapwa ni wazuri mno ni wazuri sana hata kwa wafugaji wa mmoja mmoja, lakini hawana vifaa. Naomba Serikali sasa iwahudumie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tena juu ya Kiwanda cha SAAFI kilichopo Rukwa, na-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa *PAC* na tumekagua fedha ambazo zilitolewa na Serikali kwa ajili ya kiwanda hiki, ni zaidi ya miaka mitano Serikali haijafaidi kitu chochote na hiki kiwanda na Serikali ilisema inaingia ubia na yule mwekezaji na wakaingiza zaidi ya bilioni 10 kwa ajili ya kiwanda hiki, lakini hakuna manufaa yoyote ambayo Serikali inapata kupitia Kiwanda cha *SAAFI*. Naomba Serikali sasa leo watakapohitimisha watuambie ni nini ambacho kinaendelea juu ya kiwanda hiki maana fedha zile ambazo ziko pale zilizowekezwa ni mali ya umma, ni mali ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee pia machinjio ya Ruvu, Serikali imeweka fedha nyingi sana pale Ruvu fedha nyingi, tulijenga machinjio ya Ruvu kusaidia machinjio ya Dodoma, kusaidia machinjio ya Vingunguti lakini majengo yale yamekaa bure tu hayana kazi. Fedha za Serikali zimeingia mle lakini hakuna kinachoendelea. Tuliambiwa mashine

zilishaletwa pale kwa ajili ya machinjio ya kisasa, hakuna kinachoendelea, je, tunaanzisha miradi ili tuache njiani kweli? Je, tunatumia fedha za umma ili zikae ziharibike bila matumizi, sidhani kama ndio lengo la Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuanzisha mradi na kuona kwamba mradi ule unawafaidisha Watanzania na wako wanaotafuta na wanachinja nyama hapa Dodoma ng'ombe, mbuzi, kondoo kusafirisha nchi za nje, machinjio ya Ruvu yangesaidia hata machinjio ya Dodoma, lakini majengo yale yamekaa pale hayana kazi. Naamini na vifaa vilishakuja lakini hakuna kinachoendelea na sijui kama vile vifaa viko Wizara ya Mifugo au vile vifaa vilishauzwa au bado viko bandarini mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara kwamba wameamua sasa kupitia *Ranch* ya Ruvu kwamba wameingia ubia na *RIDP* kwa ajili ya kujenga kiwanda kikubwa kwa ajili ya kuchinja, kwa ajili ya kupaki nyama na kwa ajili ya mambo kama haya yanayohusu mifugo. Ni jambo jema kabisa, lakini kwa nini tusitumie *ranch* zetu, *ranch* ya Kongwa ina mifugo mingi, nadhani kwamba ni vizuri *ranch* zetu zikasadia kuwa mfano na tukajenga viwanda vya maziwa, vya nyama katika *ranch* zetu kuliko kujenga maeneo ambayo hayana mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Felister Bura. Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, atafutiwa na Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza naunga hoja mkono asilimia mia moja au zaidi ya mia mbili. Namuunga mkono Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Makatibu Wakuu, Katibu Mkuu Wizara ya Uvuvi na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inafanya kazi kubwa sana inasaidia wafugaji na wavuvi, kitu cha kushangaza

kabisa utakuta Wabunge wengi hapa wanachangia kuisema Wizara ya Mifugo kwamba ndio inakamata mifugo ya wananchi. Kitu cha ajabu kabisa, mfugo unaingia *National Park* au *Game Reserve* anausikaje Mheshimiwa Waziri wa Mifugo kukamata ile mifugo, inakamatwa kwa sababu imefanya makosa imeingia kwenye *National Park* au *Game Reserve*. Mheshimiwa Waziri wa Mifugo hausiki, unakuta Mbunge anatoa na povu anasema Wizara ya Mifugo ndio inakamata mifugo, ni kitu cha ajabu kabisa sijaona. Unapochangia changia inapohusika kama huwezi kuchangia kaa kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi kweli Mheshimiwa Waziri, Maafisa Mifugo wanakamata mifugo au mifugo inakamatwa na Wizara ya Maliasili wakati inaingia kwenye *National Park au Game Reserve,* unapochangia changia hoja sio kuchangia *against* Wizara, kama huna uwezo wa kuchangia kaa kimya. Huwezi kuingiza kitu ambacho cha uongo na kuisema mpaka povu zinakutoka kitu cha aibu, kama hujui kaa kimya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naisifu Wizara, nazungumzia habari ya uvuvi. Wizara ya Uvuvi tuzungumze ukweli kila mara nazungumza hapa, tuelimishe wavuvi wetu, sisi Wabunge tuna kazi vilevile ya kuelimisha wavuvi wetu. Mimi mara mbili nimekwenda Kituo cha Kipili wakati wanachoma nyavu nimezuia wasichome wasichome nyavu tukaenda nikapima zile nyavu, unakuta kweli nyavu ziko milimita nane halali, amechanganya na kipande cha milimita sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyavu zinachanganywa, unakuta milimita sita, milimita nne wanachanganya nyavu, sasa utatetea wavuvi kwamba hawavui kiharamu, ndugu zangu tuseme ukweli, Serikali inafanya kazi ya ziada kulinda maliasili ya uvuvi.  Haiwezekani sisi Wabunge tumekaa hapa, tunaisema Wizara ifanye kazi, iache wavuvi wafanye kazi wanavyotaka, wengine tuige mfano tuseme hata Congo kama Congo wanaharibu kule uvuvi wao haramu acha waharibu.

Mheshimiwa Spika, kuna nyavu zinatoka Congo zinakuja kwetu, tuziache? Nyavu zinatoka Burundi zinakuja kwetu, wanaita *free* mayai zinakuja wanavua kwetu, tunazikamata tunazichoma, hatuwezi kuita Serikali ya Congo au Serikali ya Burundi au Serikali ya Zambia haiwezekani! Kama anaharibu Congo na sisi aharibu huku kwetu, haiwezekani, hata kama samaki anatembea, acha atembee lakini haiwezekani na sisi tuingilie uharibu kama wanavyoharibu wenzetu haiwezekani! Kwanza ni dhambi kuvua visamaki vidogo vidogo hata Mwenyezi Mungu hapendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali, juzi tumekutana na Katibu Mkuu, ameruhusu *ring net* wavue, lakini lazima tuwashauri na wavuvi wetu wale wasitumie *ring net* chini ya milimita nane na uvuvi lazima wavue mita 300 toka mwambao wa Ziwa Tanganyika na wavue usiku sio mchana, haiwezekani tuache tu kwa sababu ya kuomba kura kwa wavuvi au kwa wafugaji, tuingie hapa Bungeni tuharibu mali yetu, haiwezekani. Tuwe wa kweli, hawa samaki sio mali yetu peke yetu humu ndani, vizazi na vizazi, mimi nina miaka zaidi ya 70, ingekuwa wanavua tangu zamani kama wanavovua samaki tungewakuta sisi, tungekuta masanamu ya samaki tu, tuwe wakweli bwana, mtu lazima afuate sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tufuate sheria inavyotaka ya kulinda mali yetu, ni mali yetu wote tumepewa na Mwenyezi Mungu, haiwezekani kutetea mvuvi ambaye anavua kiharama unatoa povu zako, haiwezekani kumtetea mfugaji anaharibu mazingira mpaka povu zako zinakutoka, fuata sharia. Unasema wewe anaingia mnyama, kwanza atapata magonjwa kwenye wanyama wale wa asili, tembo mle ndani wamo, mna simba na chui, unapeleka ng'ombe zako wakaharibu mazingira unataka wapeleke magonjwa ya sotoka mle ndani.

Mheshimiwa Spika, Rukwa kule wamegawiwa vitalu Kalambo *Ranch,* vitalu zaidi ya 20 wameuza vile vitalu, lakini ukienda mpaka leo ni miaka 10 wamegawiwa vile vitalu mpaka leo hawana ng'ombe mle ndani, walionunua vile

vitalu mpaka sasa hawana ng'ombe, wanakodishia watu na ng'ombe chache.

Mheshimiwa Spika, juzi wamegawa vitalu vingine kula Kalambo *Ranch* kule wapeleke ng'ombe mle ndani kule kwenye Kalambo *Ranch,* lakini kuchunga hovyo halafu wanaingia *Game Reserve, National Park* wasiwakamate kwa vipi, halafu hilo swali wanapeleka Wizara ya Mifugo inahusika wapi? Haiusiki Wizara ya Mifugo ya Uvuvi, sijaona siku moja Afisa Mifugo akaenda kukamata ng'ombe *National Park* hata siku moja, sijaona mimi, wanaokamata ni watu wa *TANAPA* au watu wa *Game Reserve*, leo unachachamaa na povu linakutoka, unamshambulia na kwa jina, mnamtaja kabisa Mheshimiwa Mpina. Tulitegemea Mheshimiwa Mpina utatusaidia kwa sababu wewe unafuga ng'ombe, aaha imekuwaje! Biashara gani, haiji hata kidogo! Unategemea Mpina kwa kwa sababu ametoka kwenye kufuga asaidie ufugaji haramu. Mimi natoka kwenye uvuvi na ndugu yangu Mheshimiwa Ulega asaidie uvuvi haramu kwa sababu ni mvuvi, haiji! Ni lazima tufuate sheria ndugu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusije hapa unatoa povu zako bure, kuwakashifu Waheshimiwa Mawaziri, kuwakashifu Makatibu Wakuu kwa sababu wewe unataka kura kwa wafugaji haramu na wavuvi haramu, haiji. Waambieni ukweli, waelimisheni wavuvi, haiwezekani mvuvi, nimeona kwa macho yangu kule anavulia chandarua, unategemea sasa utakuta mazalia ya samaki, chandarua!

Mheshimiwa Spika, mimi nimekamata mwenyewe vyandarua, mimi mwenyewe nampigia Bwana Samaki Kipili, naye amekuta vyandarua vinavua samaki. Kwa sababu najua hata kura wasiponipa potelea pote, kwani nimezaliwa kuwa Mbunge mimi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani, sikuzaliwa kuwa Mbunge, lazima tufuate haki. Haiwezekani kokoro likavua Ziwa Tanganyika, makokoro bado yapo na uvuvi haramu bado upo, naomba operesheni ziendelee. Operesheni lazima ziendelee uvuvi haramu bado upo lazima operesheni

ziendelee, lakini operesheni za hekima na busara, lakini tusiache operesheni. Tusitegemee tuache operesheni kabisa samaki watakwisha. Haiwezekani, lazima operesheni ziendelee kwenye maziwa yote na bahari hizi zote, tusikubali.

Mheshimiwa Spika, kuna mabomu yanapigwa, wote mnasikia kuna mabomu yanapigwa. Kule kwangu zamani ilikuwa mabomu mpaka kuna watu wameathirika vidole miaka ya nyuma ya zamani, siku hizi ndiyo hakuna mambo ya mabomu, lakini wako mpaka waliokuwa wanakatika vidole, bomu linachelewa mkononi kwake, samaki unakuta wamelegea wote. Sasa hii ndugu zangu tukianza kutetea, tufuate haki.

Mheshimiwa Spika, hatukuja hapa sisi kwa ajili ya kura za kuombaomba, hapana. Kura zetu tumekuja hapa kutetea Serikali yetu na kutetea wavuvi wetu na wafugaji wetu kuwatetea; lakini wewe una-*base* upande mmoja tu kwa sababu wameletana hapa wanataka kusema aa, yule Mbunge ndiye mzuri tukampe kura katutetea sisi wafugaji na wafugaji na wavuvi, hapana. Lazima tuwawajibishe wavuvi wetu, kama milimita nane itumike milimita nane, lakini kama unachanganya milimita nane na milimita sita, yote umechanganya ni haramu. Huwezi kuweka kwenye sanduku lako umechanganya bangi na sigara, tumbaku, unasema ni halali, utakamatwa tu, yote ni bangi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mchango wagu ndio huu. Lazima tuelimishe wavuvi wetu, tuelimishe wafugaji wetu, tufuge kihekima na busara ili nchi yetu ipate kuendelea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Keissy. Nashukuru Bunge lilikuwa kimywa kwa sababu walikuwa wanapokea ujumbe wako vizuri.

Eeh, ni kweli, Waheshimiwa Wabunge kazima tuwe wakweli. Kama sheria ina shida tulete turekebishe sheria hapa, lakini tusilaumulaumu tu na nini halafu kudanganyadanganya watu; ubunge wa namna hiyo

ulishapitwa na wakati. Lazima uwaambie wananchi ukweli, kwenye *park* usiingize, kwenye *reserve* usiingize sheria inakataa, wewe fuga hapo, wananchi wetu wamiliki maeneo yao wafuge ndani ya maeneo. Kama kuna vitalu basi ingia kwenye kitalu, lakini kwa taratibu zilizowekwa, unatakiwa ulipe lipa, n.k. Kama ng'ombe wako ni wengi kuliko eneo basi utajua nini cha kufanya, na kadhalika, lakini hii ya kudanganyana hii Mheshimiwa Keissy umesema vizuri sana.

Ubunge wa kulambalamba na kusemasema uongo tunasababisha migongano wananchi wanaamini Mbunge kasema kumbe taratibu za Kiserikali ukweli uko hivi, tunakuwa tunawaponza watu wetu. Na upende wa Serikali nao mapungufu yao nao tuwaambie, eeh, maana Serikali ni moja na kadhalika.

Mheshimiwa Frank Mwakajoka, atafuata Mheshimiwa James Ole-Miliya na Mheshimiwa Emmanuel Papian ajiandae.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Wabunge wote ambao wamezungumza ndani ya Bunge asilimia kubwa wamejaribu kuzungumzia hali halisi ambayo inajitokeza kwa wananchi wetu hasa ambao wanajishughulisha na suala la uvuvi na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa sana; kwa mfano, Tunduma pale leo, tangu juzi, jana, leo, pamoja na mimi kukutana na Mheshimiwa Waziri na kujaribu kumweleza, lakini hali kwa kweli Tunduma ni mbaya sana. Sasa hivi Wananchi takribani 20 walikuwa wamekamatwa na wamewekwa ndani, ambao wanajihusisha na biashara ya samaki na dagaa. Vilevile wananchi hawa wanadaiwa dola *1.5,* lakini pia waepigwa faini zaidi ya milioni mbili, milioni moja na nusu, sababu kwa nini wanafanya biashara na wageni ambao wanatoka Congo na wageni ambao wanatika Zambia. Jambo hili kwa kweli limetusikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, na mwaka uliopita tulijaribu kumweleza hata Mheshimiwa Waziri; kwamba sheria hizi ambazo zimeonekana zinaleta unyanyasaji sana kwa wananchi na zinarudisha nyuma juhudi za wananchi ambao wameamua kufanya biashara ya samaki na dagaa tulimwomba azilete Bungeni ziweze kufanyiwa mabadiliko. Kwa kweli sheria hii imekuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, na ukijaribu kusoma hata Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ukisoma Kifungu cha 27 Kifungu Kidogo cha (n), Ilani inasema itawawezesha wavuvi wadogowadogo pamoja na wafanyabiashara kuhakikisha kwamba wanafnya shughuli zao vizuri bila kubughudhiwa na ikapunguza pia tozo mbalimbali ambazo zimekuwa ni kikwazo kikubwa kwa wavuvi hawa pamoja na wafanyabiashara wadogo.

Mheshimiwa Spika, lakini huwezi kuamini, sasahivi imekuwa ni kero Kanda ya Ziwa huko watu wanalia, lakini bado maeneo ambayo wanakwenda kufanya biashara. Kwa mfano Bahari Kuu, ukienda eneo la Pwani pamoja na Zanzibar wanapokuja kufanya biashara hizi imekuwa ni tatizo kubwa, lakini mpaka wawekezaji. Kwa mfano kwenye Mji wa Tunduma kulikuwa na eneo zuri kabisa la uwekezaji watu wanatoka Zambia, Congo, Angola na maeneo mengine walikuwa wananunua samaki pale, lakini leo huwezi kukuta watu wanakuja kununua pale. Sasahivi atu wanakimbiakimbia wanakamatwa, wavuvi wetu pamoja na wanaoleta dagaa pale na samaki, lakini pia wafanyabiashara wa pale wanakamatwa hovyo hovyo. Sasa tunataka kumuinua Mtanzania wa namna gani? Tunataka kumwinua masikini wa Kitanzania wa namna gani?

Mheshimiwa Spika, kama mtu anajiwezesha mwenyewe anakwenda anatafuta mtaji anaamua kufanya biashara ya samaki, anaamua kufanya biashara ya dagaa, lakini anakuwa ananyanyasika katika nchi yake anashindwa kufanya biashara hii; hivi Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ndivyo ilivyojiandaa namna hii?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba sana, kwa kweli jambo lililotokea Tunduma ninaomba Mheshimiwa Waziri alishughulikie haraka iwezekanavyo kwa sababu limeleta tatizo kubwa, limeleta tafrani kubwa. Wananchi wameshindwa kukaa, wananchi wameshindwa kufanya biashara na wageni ambao waliokuja kufanya biashara pale sasa wameamua kuondoka; sasa tunajenga nchi au tunabomoa nchi?

Mheshimiwa Spika, na leo tunakuwa humu ndani ya Bunge tunasema kila wakati kuwa tunahitaji wawekezaji waje katika nchi hii kuja kuwekeza; kama wafanyabiashara wa ndani wananyanyaswa wanashindwa kufanya biashara, hivi wawekezaji kutoka nje wanatoka wapi? Hiki ambacho tunakizungumza hakina uhalisia kabisa. Kwa hiyo, mimi nomba sana wafanyabiashara wangu kwenye Mji wa Tunduma, Mheshimiwa Waziri aweze kutoa maelezo ni namna gani wafanyabiashara hawa wataachiwa kutoka ndani, lakini pia hizi faini ambazo zinapigwa, milioni mbili, milioni tatu, wanapigwa wajasiriamali wadogo kabisa, maana yake nini katika Taifa hili? Kwa kweli, kumekuwa na tatizo kubwa sana kwenye Mji wetu wa Tunduma, lakini pia sheria hizi za uvuvi imekuwa ni unyanyasaji mkubwa sana kwenye Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine, ukisoma kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, waliahidi kwamba mpaka miaka mitano inakwisha watahakikisha kwamba wananunua meli tano za uvuvi, lakini mpaka leo hakuna meli hata moja iliyonunuliwa na bado mwaka mmoja. Sijui tafsiri yake ni nini; kwamba Ilani ya Chama Cha Mapinduzi haitekelezeki au Ilani imeachwa kama ambavyo ilikuwa inadanganya wananchi wapige kura halafu baadaye waachwe? Kwa sababu tulikuwa tumeambiwa katika ilani, ukisoma kulikuwa na meli tano zilitakiwa zinunuliwe, lakini hata meli moja haijanunuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia huwezi kuamini katika taifa hili tuna utajiri mkubwa sana wa samaki, lakini kitu kinachoendelea samaki wanaoagizwa nje kila mwezi wana thamani ya bilioni 56, kila mwezi ambayo ni sawa na dola

milioni 25. Pia kwa mwaka mzima tunatumia fedha bilioni 672 kuagiza samaki nje ilhali tuna maziwa na bahari yetu tunakoweza tukapata samaki kwa wingi. Sasa Serikali lazima ijaribu kuangalia, tunapoteza fedha nyingi kwenda kununua samaki nje, tunanunua China, tunanunua Vietnam, lakini samaki tunao; tuna maziwa, tuna bahari, lakini tunakwenda kununua samaki nje. Jambo hili Serikali iliangalie kwa umakini sana; kwa sababu kama tutaendelea kufanya haya tafsiri yake ni kwamba, tutakuwa hatulitendei taifa hili haki.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumesikia taarifa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tumeona kabisa wanasema kwamba maduhuli yamepanda sana, lakini ukweli maduhuli haya ni mateso makubwa kwa Watanzania ambao walitegemea neema na nuru kutoka kwenye Serikali hii. Hali ni mbaya sana, Kanda ya Ziwa huko kuna watu wamefilisika kabisa, Kanda ya Ziwa huko kuna watu wamekimbia nchi hii kwa sababu tu ya sheria ambazo tumezipitisha ndani ya Bunge hili. Ninaomba sana sheria hizi zibadilishwe kwa sababu sisi ni Wabunge tunatunga sheria, sheria hizi zikibadilishwa ziwe rafiki kwa Watanzania ambao wamejiingiza kwenye sekta ya uvuvi pamoja na ufugaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Frank Mwakajoka. Mheshimiwa James Ole-Miliya atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Spika, nami nimshukuru Mungu kwa nfasi hii, lakini kipekee kwa sababu ndiyo nasimama kwa mara ya kwanza tangu tumpoteze Mheshimiwa Mzee Mengi, marehemu, niendelee kumuombea Mungu ailaze roho yake pema peponi. Alikuwa kiongozi mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze watumishi wa Wizara wamefanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa Mpina alipita juzi Simanjiro na akongea na wafugaji halafu akakagua baadhi ya mabwawa yetu na Mheshimiwa Waziri ukasema utasaidia fedha kwa ajili ya kuboresha yale mabwawa. Mimi

kama Mbunge wa eneo hilo nikushukuru, lakini niishukuru Serikali yangu sana kwa kuwajali wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Katibu Mkuu wa Wizara hii, Profesa Ole-Gabriel. Siku fulani mifugo ya Simanjiro ilikamatwa kwenye Pori Tengefu la Mkungunero, yeye na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ulega, walikuwakilisha vizuri, walitusaidia ng'ombe 540 na punda 10 wakaondoka mikononi mwa hifadhi, kwa *negotiation* za Wizara, na mimi kama Mbunge ambaye napenda kushukuru kwa yale ambayo yamefanywa na Serikali ninawashukuru sana yeye pamoja na viongozi wa *TAMWA* kwa ujumla na viongozi wa Wizara ya Maliasili, wametusaidia na mifugo ile iko huru. Ninawashukuru na wafugaji wa Simanjiro wanawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais, tuendelee kumpa moyo sana kwa kazi kubwa anayowasaidia wafugaji. Wafugaji wengi wako hapa, kwenye hizi *gallery* zote wafugaji wapo. Mheshimiwa Rais ametamka kwamba wakati tunapata uhuru wa nchi yetu taifa lilikuwa na wakazi na Watanzania milioni tisa tu na mifugo ni michache, tumeongezeka kwa takribani milioni 55. Baada ya kuona haja hiyo, ameona yale maeneo ambayo wahifadhi hawayatumii kwa ajili ya mbuga za wanyama amesema kwa upendo mkubwa wa wafugaji yagawiwe, ifanyike timu maalum ya Mawaziri imepita ili wafugaji wapate maeneo hayo. Huu ni upendo gani kwa mkuu wetu wa nchi, anatupenda sana. Mimi kama mfugaji na Mbunge anayetokana na CCM nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, wafugaji wamelipokea hili kwa mikono miwili. Anapenda na wafugaji wako na yeye siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine; kuna ugonjwa unaitwa ugonjwa wa ndigana. *African Union* miaka fulani pale Adis Ababa waliamua kujenga kiwanda cha kuzalisha dawa ya ndigana pale Malawi; lakini hapa nchini mtu aliyepewa tenda hiyo ni mtu anaitwa Dokta Mbwile. Ninapoongea leo mifugo katika Ukanda wote wa Simanjiro, Arusha, Manyara wanakufa kwa sababu dawa hii haipo sokoni. Wizara sijui

mmetumia hekima gani, mnatoa tenda hii kwa mtu mmoja tu nchi nzima. Niiombe Wizara kama ushauri hii tenda igawiwe kwa watu wengine kwa sababu, ule ugonjwa ukimshika ndama au ng'ombe haiwezekani kumtibu tena. Ninawaomba mfikirie namna ya kuongeza wadau wa kuchukua dawa hii kutoka Malawi wailete Tanzania.

Mheshimiwa Spika, la pili; maeneo ya wafugaji ni maeneo makame sana, yanapokea mvua kidogo kila mwaka. Namna pekee ya kuwasaidia wachungaji na wafugaji kwa ujumla nchi hii ni kuanzisha mabwawa makubwa.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uhuru kulikuwa na mabwawa, natoa mifano miwili, Kata ya Narkawo na Kata ya Komolo pale Skuro; mabwawa ambayo Mheshimiwa Waziri wa Mifugo ulitembelea; ni mabwawa makubwa ambayo Mheshimiwa Nyerere, Baba yetu wa Taifa aliyaanzisha kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji. Kwenye maeneo mengi ya wafugaji ardhini hakuna maji, mtusaidie tupate mabwawa makubwa kila eneo ili wafugaji wapate nafuu ya adha ya ufugaji wao.

Mheshimiwa Spika, lingine ni migogoro ya wafugaji. Migogoro hii imekuwa kero. Nimesoma jitihada za Wizara, wamefanya vizuri, maana wametembelea Wilaya za Uvinza, Kasulu, Kibondo, Katavi, Kalambo, Nkasi na Sumbawanga. Niombe, nchi hii migogoro ya wafugaji na wakulima mingi imekithiri eneo la Morogoro; mtusaidie sana Morogoro, muipe kipaumbele Morogoro. Na kwa sababu nimeona mmewashirikisha akina nani, niombe Kanisa la Kilutheri la Kiinjili la Tanzania pale Morogoro mlihusishe. Kuna Askofu mmoja pale anaitwa Askofu Mameo; ni mtu mwema anaweza kuisaidia Serikali kwa ajili ya kutatua tatizo hili la wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Spika, jana nimefarijika sana nimeongea na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na yeye anasema yupo tayari kuingia Morogoro kwa sababu ni mkazi wa Morogoro na kusaidia migogoro hii kwisha. Kwa hiyo,

shirikianeni na Naibu Waziri wa Kilimo yuko tayari kusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, lingine; Ranchi za Taifa kwa awali kabisa zimechukuliwa kutoka kwa wafugaji. Leo hii kwa takwimu Ranchi za Taifa zinamiliki hekta laki mbili kwa mifugo elfu 30 tu. Kwa sababu kuna ranchi nyingine hazitumiki na Serikali wafikirie namna gani ya kuwagawia wafugaji, lakini wangalie, waweke angalizo moja, wasiwape watu wenye nguvu tu, wachukueni wafugaji wa kawaida wagawiani ranchi hizi. Kuna Kilimanjaro kule, kuna hapa Mpwapwa, kuna nyingine Kanda ya Ziwa. Mtusaidie wafugaji ili tuondokane na hizi shida na kumsaidia Mheshimiwa Rais ili hatimaye tusipate shida ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Suala la Maziwa. Ninaipongeza sana Wizara kwa kuamua kulinda viwanda vya ndani. Leo hii pale Arusha ukijaribu kununua *Brookside* au maziwa ya Afrika ya Kusini ni bei ghali sana. Kwa hiyo Wizara nia yake na Serikali ni kukuza viwanda vya ndani. Nimeona maziwa yetu ya Azam, maziwa yetu ya *Tanga Fresh,* kama Mheshimiwa Rais alivyotembelea, yanaanza kupata soko kwenye nchi yetu. Endeleeni hivyo hivyo tuwaunge mkono wazalishaji wa maziwa, nendeni chini muwagundue wengine ambao wanataka kuanzisha biashara hii wapeni *support.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo niombe linguine. Juzi nimeona *clip* moja, na mimi nilisema mara nyingi sitaki kuongelea upinzani sana, lakini mara nyingine wanapoanza kufanya siasa za ajabu inabidi mtu uondoke kwenye mstari ambao hukutaka kuukanyaga. Nimemwona Mwenyekiti wa Taifa wa Chama kinachoitwa CHADEMA. Mheshimiwa Mzee Lowasa alipoondoka na kurudi nyumbani kwake CCM aliwashukuru CHADEMA na akanyamaza; lakini cha ajabu sana Mzee Mbowe juzi anasema Lowasa ameondoka na mke wake peke yake. Ninaomba apate ujumbe mzuri huu, kura za Serikali za Mitaa mwaka huu mtaona jibu lake, kwamba CCM imara ile ambayo tunaijua kuanzia miaka ya elfu mbili, sabini, sasa mtaiona. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ole-Millya. Nakushukuru sana asante.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Spika, na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dokta Mary Nagu, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Papian na Mheshimiwa Hussein Bashe ajiandae.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kunipa nafasi hii. Mimi natoka kwa wafugaji, baba yangu alikuwa daktari wa mifugo kwa hiyo, ninaelewa mambo mengi sana ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kujiweka kabisa kwamba anapenda wafugaji na anapenda mifugo. Nina hakika kuwepo kwake kutasaidia sana kwa wafugaji kuweza kunufaika na kutoa mchango mkubwa kwenye mapato ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mifugo imeongezeka na mazao ya mifugo yameongezeka. Pamoja na hivyo mifugo mazao yake ni *protein* kwa binadamu. Mazao ya chakula na mazao ni malighafi, mazao ya mifugo ni malighafi ya viwanda vyetu. Wakati huohuo nataka niwaambie, kwamba mifugo inaweza ikatoa mapato makubwa kuliko sekta nyingine yoyote kama tutaiangalia vizuri. Hata sasahivi mchango wa mifugo, mazao yake na bidhaa ni kubwa sana kwa Serikali hii. Vilevile nilipokua nikifanya kazi *NDC* kiwanda cha viatu bora cha kilikuwa namba mbili ya kutoa mapato Serikalini; kwa hivyo hii inaonesha kwamba kama tutaisimamia hii sekta vizuri kwa kweli wafugaji watanufaika na taifa nalo na Serikali itanufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na michango hii mikubwa, na sitaki kurudia takwimu kwa sababu Waziri ameweka

takwimu vizuri na waliotangulia wameongea juu ya takwimu vizuri. Nikirudia haitasaidia lakini ni wazi kwamba mchango wa mifugo na mazao yake ni mkubwa sana kwa taifa letu. Hata hivyo, pamoja na mchango wa mifugo katika maeneo mbalimbali sekta hii inakabiliwa na changamoto nyingi ambazo kama tutaziondoa wafugaji watanufaika, Taifa hili litanufaika.

Mheshimiwa Spika, ya kwanza, ni kutokutekeleza matumizi ya ardhi na wanajua kabisa kwamba hakuna mfugaji mmoja mmoja mwenye eneo isipokuwa Serikali yenye ranchi. Wafugaji wanakuwa na ardhi ambayo ni ya pamoja *(communal)* na haiwezekani kuwa ya mmoja mmoja jamani. Kwa hivyo Serikali yetu ikiweza ku-*protect* au kulinda maeneo hayo ambayo ni *communal* ya wafugaji wa jadi na wafugaji wa kisasa, nina hakika wafugaji hawatapata migogoro wanayoipata sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, migogoro hii iko kati ya hifadhi na wafugaji, kati ya wafugaji na wakulima na wengine. Kama maeneo ya wafugaji kwanza yatajulikana na yatalindwa, migogoro hii itapotea bila ya nguvu kubwa jamani na naomba hili lifanyike na tutaondoa migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya pili ni rushwa; kama kuna watu wanaumizwa na rushwa nchi hii ni wafugaji na hasa kwenye hifadhi. Nina mfano mzuri kule kwa Mheshimiwa Millya aliyemaliza kuongea, ng'ombe wa mfugaji wamekwenda kuchukuliwa nyumbani kwa sababu hawapati watu wanaopeleka mifugo kwenye hifadhi. Wamewapeleka kwa kuwadanganya kwamba wanawapeleka mahali pazuri, lakini kumbe wanawapeleka kwenye hifadhi na siyo rahisi kwa mfugaji wa kawaida kujua kwamba mipaka ya hifadhi ni wapi, naomba na hili lionyeshwe. Walipofika kule, wameambiwa mpo kwenye hifadhi, lipeni milioni 10 na wale wakakataa na sasa wapo mahakamani na inawezekana wakashindwa na hii ni laana kwa kila mmoja; kwa yule aliyehusika na hata Serikali yetu itahusika kwa namna fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, suala hili la rushwa liangaliwe na sekta hii iwalinde wafugaji wasiungane kwa sababu nakubali kwamba kuna wachache ambao wanaingiza mifugo kwenye hifadhi, lakini wengi wanaonewa kwa sababu uelewa wao kule porini si mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, nataka niwaambie kwamba bila kuangalia mifugo, wafugaji watapotea na nchi hii itapata hasara kwa sababu nimewaambia kwamba bila kuwatetea hawa wafugaji, hakuna namna. Nataka niwaambie kwamba jamani kuna suala la dawa feki na kuna watu ambao wanataka washikilie wafugaji wawaone kwamba ni wazuri kumbe wanawashikilia wafugaji kwa sababu wanataka kupeleka dawa feki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali na Wizara hii, Waziri naomba wasimdanganye, ataniuliza kwa nini nasema hivyo, wanakuwa karibu na yeye halafu wafugaji wanapelekewa dawa feki na ng'ombe na wafugaji wanaumia. Namwomba sana Waziri namwamini lakini si rahisi kuwajua watu ambao wanataka kunufaika kwa kuonekana ni wazuri lakini kumbe ni ubinafsi wao wenyewe. Naomba dawa hizi feki ziangaliwe, chanjo za ng'ombe ziwe na uhakika na dawa za tiba ziwe na uhakika, nina hakika Sekta hii itakuwa na mchango mkubwa sana kwenye uchumi wa nchi hii, itawanufaisha wafugaji, umaskini utapungua; tuwasaidie wafugaji na Mungu atawabariki nyie wote. Ahsanteni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Kila siku nasahau kutoa hoja, lakini naunga masuala yote ya Serikali. Naunga kwa mikono yote miwili bajeti hii na mimi nipo pamoja na wao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Emmanuel Papian, atafuatiwa na Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Oscar Mukasa ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza naunga mkono hoja ili nisije nikasahau mwisho.

Mheshimiwa Spika, nipongeze Wizara na Waziri kwa bajeti nzuri ambayo wametuletea, lakini pia nipongeze na Kamati yangu kwa kazi kubwa ambayo tumeifanya inayoongozwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Mgimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo jambo moja ambalo naomba niseme, naipongeza Wizara kwa kazi moja ambayo wameifanya ya kupunguza migogoro ya wafugaji kwenye maeneo ya malisho, wamechukua maeneo makubwa kwenye ranchi za Taifa, wamekodishwa wafugaji, ng'ombe wamehamia mle kwa hiyo kero imepungua kwenye maeneo mengi; Kagera, Ruvu, Kalambo na mikoa mingine ambayo ina ranchi za Taifa ambazo wale wafugaji walikuwa wanazunguka na kuhangaika kwa ajili ya kutafuta malisho. Nawapongeza na nampongeza Mkurugenzi wa *NARCO* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba hili jambo linafanyika na mifugo inapata maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; niombe kuzungumzia suala la uvuvi haramu na stori nyingi ambazo zimeendelea kwa nchi nzima juu ya uvuvi haramu. Nikushukuru kwa sababu tulikwenda Mwanza kama Kamati, tukakutana na wadau wote; tulikutana na wadau wa viwanda, tukakutana na wavuvi wenyewe na wale madalali ambao wanauza samaki kwenye viwanda.

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa kule Mwanza kila mtu tumempa dozi yake; Waziri amepata dozi juu ya watendaji wake ambao hawatimizi wajibu wao sawasawa, lakini na wale madalali tumewapa dozi yao kwa sababu wanafanya udalali kwa kupunguza bei ya wanaokwenda kununua samaki kwa wavuvi na ku-*collude* pamoja na wenye viwanda. Suala hili ni suala pana, lakini tunaamini sasa tunapokwenda kwa dozi tuliyoacha kule ndiyo maana unaona kidogo sasa hivi hakuna malalamiko kumetulia,

isipokuwa yale madogo madogo tunaendelea kuyakamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya kazi kubwa, haya mambo mengi yatakwenda yanapungua pole pole na tutafika mahali ambapo tunaitendea Wizara hii haki. Tunalo tatizo kubwa, wavuvi hawasemi ukweli kwenye baadhi ya maeneo mengi na ndiyo maana kuna eneo la uharamu ambao unafanyika. Leo, tunapozungumza Wilaya ya Muleba kwa Mheshimiwa Mwijage pale, uvuvi kwenye vile Visiwa vyote vya Bumbire na wapi kote, leo wana-*enjoy* samaki wapo, wakienda ziwani wanarudi na samaki wa kutosha ambao wao wanaendelea ku-*enjoy*.

Mheshimiwa Spika, pia Halmashauri yetu ile ya Muleba nampongeza yule Mkurugenzi alikuwa anakusanya milioni nne kwa mwezi, leo anakusanya milioni 50. Kwa hiyo, Halmashauri inaendelea ku-*grow,* hiyo ni TAMISEMI ina-*earn* kutokana na *effort* za Wizara ya Mifugo. Haya yote twende tunayaona, ukizungumza na wale wavuvi wadogo wadogo wana-*enjoy* samaki wapo, wamekuwa wanavua kwa muda mfupi na wanapata samaki kuliko kushinda ziwani siku mbili, tatu.

Mheshimiwa Spika, wenye viwanda; wenye viwanda wanakwenda wana-*determine price* bila kushirikisha Serikali, wanashusha bei, wanadili na madalali wetu, wahuni, matapeli ambao siyo waajiriwa wa Wizara wala siyo watendaji wa Halmashauri. Wanashusha bei ya wavuvi, samaki wao wanawaingiza viwandani, wakishamaliza wale samaki wanawachakata, wakimaliza wanamwambia samaki wako bwana, hawa samaki hawako kwenye *size* na zile milimita zilizopangwa kwa hiyo ondoka na samaki wako, wameshawachakata mvuvi anapata hasara. Naomba hili suala sasa Wizara iliangalie kwa ukaribu sana na iweze kuona hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa inabeba lawama nyingi hizi za uvuvi, lakini *on the way* mvuvi analeta samaki kwenye kiwanda, anakamatwa na watu wengine na watu

wa ushuru ambao ni wa TAMISEMI, Polisi na watu wengine ambao ni Wizara tofauti kabisa na Wizara husika, wanapopigwa faini na kudaiwa ushuru huu mzigo unaenda unatupwa kwenye Wizara husika. Ushauri wangu juu ya hili, tunaomba hizi Wizara ziweze ku-*interrupt* zione *solution* ya pamoja juu ya kutatua huu mgogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo jambo la mwisho kwenye uvuvi, tulitengeneza kanuni na sheria hapa juu ya uvuvi, tunaomba hizi sheria na kanuni kandamizi Mheshimiwa Waziri azilete hapa tuzifumue, tupange upya suala la utaratibu wa wavuvi uweze kukaa salama na nchi iweze kubaki salama tupunguze suala la lawama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo suala la viwanda juu ya uzalishaji wa maziwa ya *UHT, long life milk.* Wameongeza kodi ya maziwa kwa ajili ya ku-*reduce importation* ya maziwa, lakini wakati huo tumepunguza hiyo, ilikuwa ni ku-*promote* viwanda vyetu vya ndani, kwa hiyo, viwanda vyetu vinavyozalisha kama *Tanga Fresh* na *Asas* wameshafunga mitambo ya *UHT*, sasa hivi wanajaribu ku-*push* kuona namna gani wanaweza kupanda wakitegemea wale wazalishaji wa maziwa wadogo, tukitegemea *growth* yao, Benki ya Kilimo na benki zote *(commercial banks)* zi-*support* hawa wakulima waweze ku-*grow.*

Mheshimiwa Spika, leo Waziri amekuja na suala la kupunguza tozo ya maziwa yanayokuwa *imported* ya unga, ukipunguza kilo moja ya maziwa ya unga yana-*produce* lita nane. Ukimpunguzia Azam leo, ukapunguza kwa *level* hii ya *eighty something percent it means* unakwenda kusababisha hivi viwanda vya Asas na *Tanga Fresh* vife asubuhi kwenye hii *UHT*. Wamekopa kwenye mabenki ya ndani, wana-*promote* wazalishaji wa maziwa wadogo *which means* unga unaendelea kuongezeka, maziwa ya unga yanaongezeka, una-*import* hiyo una *impose* unapunguza kodi, unasababisha watu wetu kufilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikueleze kwa hili na itatokea na utaiona, kwa hili Mheshimiwa Mpina akae chini

atafute *cash flow* na *projections* za namna ya *importation* ya maziwa ku-*protect* viwanda vyetu vya ndani vya *UHT* kama programu ilivyokuwa. Hiyo ndiyo inayokwamisha Sekta ya Maziwa nchini kwa sababu *investment* ya maziwa, mradi kwenye *plant* ya *UHT* ni zaidi ya dola milioni nne au tano, sasa anapo-*invest* amekopa hapa, uka-*import* hayo ni kwamba hawezi kushindana kwenye soko, mwisho wa siku kinachotokea ni nini? Anaweza kuuza lita ya maziwa Sh.2,600, huyu mwingine ni lazima akiweka zile *cost* zote vyovyote vile inatozwa 18% lazima atatokea kwenye Sh.3,000. Mwisho wa siku, hakuna uwiano kwenye hili. Niombe Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa haraka sana hili ili kuokoa na ku-*allow* ushindani wa ndani, tuwe kwenye *balancing point,* asiwepo bora na mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala lingine; kwangu kumeanzisha Hifadhi ya Olengapa, nyanda za malisho, lakini kumekuwa na migogoro mingi, watu wanalalamika. Nimefanya ziara, kipofu mmoja akanyoosha mkono anasema mimi shamba langu limekwenda, nilikuwa nalima, ni kipofu, sasa naenda kufa. Alipozungumza kwenye mkutano wenzake wakamwambia ale udongo. Mheshimiwa Waziri aje, tukae tuone hao watu wanaolalamika kwa nini Olengapi wamechukua eneo wasingeacha wale wakulima 300 na eneo lao, ime-*incorporate* lile eneo ikalichukua ikaacha hawa watu ikiwemo hao vipofu wanaolalamika kwamba wameambiwa na wenzao wakale udongo. Niombe kwamba sasa hilo suala Waziri atakapokuja, basi atusaidie ni namna gani ya kutatua hilo... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Emmanuel Papian.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Bashe atafuatiwa na Mheshimiwa Kuntu Majala.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii. Nitumie nafasi hii kwanza nimpongeze Waziri Mheshimiwa Mpina na Naibu wake kwa angalau kuleta *awareness* ya Sekta ya Mifugo na jitihada wanazofanya. Mchango wangu utakuwa ni kushauri zaidi kwenye eneo la mifugo kwa maana ya ng'ombe lakini vilevile maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhana nzima ya ufugaji ni dhana ya *input* na *output* kwa maana ya kwamba unachokiingiza ndicho unachotarajia kukipata. Kwa hiyo, ukifanya *wrong investment* na *wrong input,* utarajie matokeo dhaifu. Ili viwanda vya maziwa viweze kufanya kazi vizuri, hatua ya kwanza ni kuhakikisha kwamba malighafi ya maziwa yanapatikana kwa urahisi, *at a competitive rate* ili yule mzalishaji wa maziwa aweze kuyanunua na mkulima apate faida.

Mheshimiwa Spika, nitatolea mfano, mfugaji anayezalisha ng'ombe wa maziwa, ng'ombe mmoja anayetoa lita 10 anahitaji kula majani makavu yenye uzito wa kilo 19. Ng'ombe huyu ili aweze kupata ile *hay, hay* moja inauzwa Sh.2,500 mpaka Sh.3,000, kwa hiyo, kwa siku majani yake ni Sh.3,000; tunamzungumzia mfugaji anayefuga kwa ajili ya kuuza maziwa *commercially.* Anahitaji kumpa *supplement* kilo mbili asubuhi na akilo mbili jioni, ina maana kilo nne ya *supplement.* Kilo nne ya *supplement* kwa bei ya sasa hivi iliyopo sokoni ni kati ya Sh.470 mpaka Sh.500. Kwa hiyo, kama atampa kilo nne maana yake ni Sh.2,000. Kwa hiyo, kampa majani yenye thamani ya Sh.3,000 halafu kamlisha *supplement* ya Sh.2,000, gharama yake ni Sh.5,000.

Mheshimiwa Spika, mifugo yetu yote iliyopo katika nchi hii wastani wake wa uzalishaji ni lita 10 *maximum,* hatuna ng'ombe wanaozalisha lita 20 au lita 30, ni wachache sana na wafugaji wetu katika *household* wengi *capacity* ya ng'ombe wao wengi ni *ten litres at the best.* Kwa hiyo, maziwa anayauza shilingi ngapi, anayauza Sh.900 mpaka Sh.100; kwa hiyo kapata Sh.9,000 wakati yeye kagharamikia Sh.5,000 mpaka Sh.6,000; hizi ni gharama za moja kwa moja. Bado

kuna gharama za madawa na maji, matokeo yake ni kwamba bei ya uzalishaji wa maziwa *per litre compared* na bei ya ununuzi kiwandani, wafugaji hawapati faida yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mfugaji ana-*opt* kufanya nini? Ana-*opt* kufanya uchungaji wa kawaida, hata hapa Dodoma ukipita barabarani unaona ng'ombe wa kisasa wanachungwa barabarani kwa sababu hawana uwezo wa kupata *input* ya kumlisha ng'ombe, kwa hiyo tunaingia kwenye tatizo la *feeding.* Kinachotokea kwa kuwa ng'ombe hajalishwa vizuri, hawezi kuzalisha vizuri, kwa hiyo viwanda haviwezi kupata maziwa ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nini ushauri wangu kwa Serikali? Ushauri wangu wa kwanza, ni lazima Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Ardhi, Wizara ya TAMISEMI wakae chini pamoja kuja na *master plan.* Ukisoma *Tanzania Livestock Master Plan* iliyozinduliwa na Waziri, *it is centered* kwenye Wizara moja na suala la ufugaji ni *crosscutting,* siyo la Wizara ya Mheshimiwa Mpina peke yake. Leo tuna shamba la Serikali la kuzalisha malisho lipo Dar es Salaam, ni *under capacity*, haliwezi kuzalisha chakula cha mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimeona hapa Mheshimiwa Waziri amesema anafanya uhilimishaji wa ng'ombe wa kienyeji milioni tatu kupata mitamba milioni moja. Ni hivi, ukimchukua ng'ombe wa kienyeji Mheshimiwa Mpina anafahamu Tarime ya kule kwetu Tabora na Shinyanga, ukampandisha dume wa *Fraiesian* atapatikana *F1, F1* huyu *capacity* yake ya uzalishaji wa maziwa *is maximum of three and four litres.* Ukimpelekea mfugaji akamfanye *zero grazing is an economical,* haiwezekani, hawezi kumzalisha na kupata mazao. Ili aweze kupata ng'ombe wa kumpatia maziwa mazuri anayetokana na ng'ombe wa kienyeji ni *third generation*, apatikane *F1, F2, F3* ndiyo huyu F3 atafika *at least 10 litres* kwa sababu *genetically* ni 25, 50 and 75 yaani *generation* ya tatu ndiyo tutapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ambao nataka niishauri Serikali, hawawezi kufanya *mass insemination* nchi nzima, lazima tufanye *clustering* ni wapi tunazalisha ng'ombe wa maziwa, wapi tunazalisha ng'ombe wa nyama, huu ni ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili kwenye maziwa, leo kiwanda cha maziwa kinahitaji kuzalisha maziwa na wao Wizarani wanajua, walikuja watu wa *Tanga Fresh* kwenye Kamati ya Bajeti eti waliomba kibali na mimi niwapongeze Wizara ya Mifugo waligoma, wanaomba kibali wa-*import* maziwa *raw* kutoka Rwanda.

Sasa *what is the success story* ya Rwanda? *Success story* ya Rwanda ilikuwa ni moja, kila kaya ilipewa programu ya ng'ombe mmoja wa maziwa lakini kwenye vijiji zikaanzishwa *collection center* kwamba wafugaji wote wanaleta maziwa yao kwenye *center* moja, pale kwenye *center,* kiwanda kinakuja kuyachukua yale maziwa. Sasa hivi wafugaji wetu wapo *scattered,* hawezi kusafirisha maziwa yake kuyaleta kwenye *center* au kumfikishia mtu wa kiwandani kwa sababu gharama ni kubwa na kwa hali hii hatuwezi ku-*break through. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, *Asas* yupo nyanda za juu, *it's better* kukaa chini na Wizara ya Fedha kuangalia *incentive* za kikodi na kumtengenezea *clustering centers* kwenye Mikoa ya Mbeya na Iringa, yeye ajenge *cooling centers* ambazo wafugaji watapeleka maziwa yao pale, yeye ataenda kuyachukulia pale ili gharama zake za uzalishaji ziwe ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka niongelee, nataka nimshauri Waziri, ukienda *NAIC* pale Arusha wana ngo'mbe anaitwa *Friesian,* wana ng'ombe labda anaitwa Borani, wana ng'ombe anaitwa *Ayrshire.* Kwenye *breeding* ya ng'ombe wa nyama *the best breed* ni aina mbili; ni Borani na *Sahiwal,* lakini kwa *insemination* hatuwezi kubadilisha ng'ombe wetu wa Kisukuma na Kigogo na Kimasai.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu; Serikali ianzishe programu, mnunue madume ya Borani; wakati wa Mwalimu Nyerere kulikuwa kuna *holding grounds* zilikuwa zinatumika kwa ajili ya *breeding;* kwa hiyo yale madume ya Borani mnayapeleka Nzega, halmashauri inakabidhiwa, katika kila kijiji kunakuwa na *centers* au kata halafu mnaenda kuhasi madume ya kienyeji, mnaanzisha programu ya kupandisha ng'ombe wa Borani kwenye ng'ombe wa kienyeji, tutabadilisha *breed* namna hii.

Mheshimiwa Spika, lakini ziki-*run parallel* ng'ombe wa kienyeji na Borani ambao wanauzwa milioni moja na nusu, milioni mbili, wafugaji hawawezi ku-*afford.* Ili anunue dume mmoja wa Borani inabidi auze ng'ombe zaidi ya sita wa kienyeji, *he cannot afford* kwa sababu ana ng'ombe wake kumi anaona anaingia umaskini. Kwa hiyo mimi nashauri Serikali tafakarini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante, malizia.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Spika, namalizia la mwisho, dakika moja tu nakuomba.

Mheshimiwa Spika, ngozi; rudisheni utaratibu wa zamani, zamani kulikuwa kuna kitu kinaitwa *Tanzania Hides and Skin,* ngozi zinauzwa kwenye mnada kwenye machinjio. Bila kufanya namna hiyo mazao ya ngozi hamuwezi kuya-*control. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa kunti Majala, kama yupo. Atafuatiwa na Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mheshimiwa Stanslaus Mabula ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi niweze kusema machache kwenye Wizara yetu hii ambayo imebeba Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, mimi nitaomba nizungumzie suala zima la wagani (maafisa mifugo), lakini pili migogoro na tatu ni ushuru kwenye minada yetu na ntagusia kidogo suala zima la nyavu haramu.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wetu wengi walioko vijijini wana changamoto kubwa sana ya wagani ama maafisa mifugo. Kwanza maafisa mifugo hawajitoshelezi, lakini pili hao waliopo hawafanyi kazi ipasavyo kwa mujibu wa maadili yao ya kazi. Leo afisa ugani aliyeko kijijini yeye amekuwa ni mchuuzi. Analipwa mshahara na Serikali lakini bado anapohitajika kwenda kutimiza wajibu na majukumu yake mtu huyu ukimfuata atakwambia kwanzasina usafiri, hilo ni kweli hawana usafiri, lakini pili, akienda kufanya hiyo kazi atakwambia sasa unanipa shilingi ngapi; mtumishi huyu analipwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hawa watu, maafisa ugani waliopo tunaomba Wizara iweze kuwafuatilia mmoja baada ya mwingine kwa sababu wamekuwa ni kero na changamoto inayosababisha wakulima ama wafugaji wetu kuacha kuwatumia kutokana na biashara yao ya kutoa huduma, badala ya kutoa huduma kwa jamii, wanalipwa mishahara na kodi hizohizo za Watanzania, wanaacha kufanya hiyo kazi wanataka walipwe fedha nyingine ili waweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maafisa ugani hawa bado wana shida ya vitendeakazi. Afisa ugani huyu uliyempeleka kwenye kata pale ana vijiji vitatu ama vinne; kutoka makao makuu ya kata mpaka kwenda Kijiji A unaweza ukakuta kuna kilometa 20 mpaka 30; vijiji vyetu hata vya Mkoa wa Dodoma unavijua jinsi vilivyo; mtu huyu hana usafiri, hana pikipiki wala baiskele. Hivi Serikali hii ya uchumi wa kati, Serikali ya viwanda tunaifikiaje hiyo ndoto bila kuwaboreshea maisha

vitendeakazi vya hawa maafisa ugani wetu ili waweze kufikisha huduma kwa wakulima wetu?

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la migogoro ya ardhi; limesemwa na Wabunge wengi lakini suala hili ni kama vile limetulia kidogo, limepoa, lakini linafanyika chini kwa chini, kuna mambo yanayoendelea huko huwezi kuamini. Naibu Waziri alifika Wilaya ya Chemba na Wilaya ya Kondoa, kwenye Pori la Swagaswaga pamoja na Mkungunero. Kuna watu walikamatiwa ng'ombe wao wakiwa wanachunga, si kwenye hifadhi, ni mpakani na hifadhi, wale watu wa hifadhi wakaenda wakawasukumia wale ng'ombe kwenye hifadhi wakawakamata.

Mheshimiwa Spika, walivyowakata wakaenda wakawaambia kila ng'ombe mmoja alipiwe shilingi laki moja. Watu wale wakasema hizo hela kwa sasa hatuna, wakawaambia nendeni mkatafute mrudi. Walivyorudi wakahojiwa kila mfugaji mmoja wewe ulikuwa na ng'ombe wangapi, mfugaji anasema nilikuwa na ng'ombe 200 anaambiwa ng'ombe hawa 200 mara 1000 tujumlishe. Lakini watu hawa walikuwa wakilipa hizo faini, wanapokabidhiwa ng'ombe hawafiki ng'ombe 200, mtu atapewa ng'ombe 150, atapewa ng'ombe 80. Wakiuliza ng'ombe wetu wengine wako wapi wanaambiwa ng'ombe wamepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo haya yanasononesha, mambo haya yanasikitisha, mambo haya yanahuzunisha na yanatia simanzi sana ndani ya taifa letu la Tanzania. Taifa hili, wakulima hawa, wafugaji hawa, huyu mfugaji anatakiwa alipe ada ya mwanafunzi, anatakiwa ale, anatakiwa afanye mahitaji yake yote kulingana na hawa ng'ombe wake. Umeenda umemchukulia ng'ombe wale, umemlipisha faini, unamtaka nini huyu mfugaji? Tanzania ya wanyonge ipi katika taifa letu leo la Serikali ya Awamu ya Tano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa na Wizara bado hazina dhamira ya dhati ya kwenda kupambana na watu hawa ambao wameendelea kuwadhalilisha Watanzania walio wengi katika taifa hili ambao ndio walipa

kodi na wao ndio wanalipwa mishahara na haohao walipakodi wanaowanyanyasa. Naomba watu wale ambao ng'ombe wao hawakurudishwa, Mheshimiwa Waziri ukija naomba uniambie watu wa Mkungunero na Swagaswaga waliokuwa wamekamatiwa ng'ombe wao, hawakurudi, naomba uniambie watu wale mnawachukulia hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Suala Zima la Ushuru wa Minada. Tunafahamu minada haipo kwenye vijiji vyote wala kwenye kata zote, tuna minada ambayo tumeiteua. Lakini ni kwamba katika minada hii, kumekuwa na ushuru wa usafirishaji na kwenda kuuza, mfano mwananchi anayetoka Kijiji cha Mlongia kwenda kuuza ng'ombe Mnada wa Soya, huyu mtu anatakiwa kukata ushuru...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kuniti, nakushukuru.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oscar Mukasa atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kutoa mchango wangu. Lakini kwa namna ya juu kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufaya kazi hii; na ninawapongeza Wizara, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na timu yenu nzima, hongereni kwa kazi mnayofanya.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano ilivyoingia madarakani, miongoni mwa mambo ambayo iliyafanya kwa nguvu kubwa kabisa ni kuweka amri ambazo zilisaidia kwenye utekelezaji wa sheria kwenye mambo ya hifadhi ambayo ilihusiana na mifugo, kwa sababu ilikuwa

inaingia kule, lakini pia na habari ya uvuvi. Ni jambo zuri, kwa sababu sheria ni namna tu mlivyokubaliana namna ya kuishi na namna ya kuhusiana lakini amri ndiyo lile karipio linalotoka kwenda kuhakikisha watu wanafuata sharia; kwa hiyo hilo nalipongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, mimi ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba sasa tumepata muda wa kutosha wa kuweka amri ili sheria zitekelezwe na ushahidi uko wazi, kwamba sasa amri zinaanza kuzaa matunda. Nitatoa mfano wa Biharamulo; Biharamulo ni Wilaya ambayo asilimia 46 ya eneo lake ni eneo lililohifadhiwa; kwa maana ya Burigi, Biharamulo na Kimisi; kwa hiyo asilimia 54 ya eneo iliyobaki ndiyo kwa ajili ya shughuli nyingine za uchumi, nasema nyingine kwa sababu uhifadhi nao ni shughuli ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, na kwa sababu hiyo, kwa sababu ya kitovu hicho cha hizo hifadhi tatu, wakati wa zile vurugu za kuondoa mifugo kutoka kwenye hifadhi ili habari ya uhifadhi iende vizuri Biharamulo ilikuwa ni kitovu cha mapambano kati ya hifadhi na wafugaji, ilikuwa vurugu kubwa sana. Lakini sasa mimi ni mmoja wa mashahidi kwamba ni kweli kuondoa wale ng'ombe hifadhini kumeanza kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, juzi hapa mmeona kuna picha ilikuwa inatembea kwenye mitandao, kuna ndovu mmoja amegongwa na gari barabarani, nafikiri ni upande wa Karagwe, hiyo ni ishara kwamba wanyama hawa tunaowahifadhi wameanza sasa kuwa wengi na sasa wanaanza kuonekana hata kwa ngazi hiyo. Lakini faida hiyo tunayoipata upande wa hifadhi hebu twende na upande wa pili, upande wa wafugaji nako tutafute sasa kwenda hatua ya zaidi baada ya amri sasa tuanze kuwekeza kwenye mambo ambayo yataongeza tija.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kabla ya zile vurugu za hifadhi na wafugaji mimi nilikuwa nimepata fursa ya kuongea na mfuko mmoja wa hifadhi ya jamii; walikuwa

tayari kuja kukaa na Chama cha Wafugaji Ukanda ule wa Wilaya za Biharamulo, Ngara, Karagwe, Chato, Muleba, ili kuona ni namna gani eneo dogo tulilonalo la asilimia 54; kwa sababu tunafanana wilaya hizo; litatumika kwa tija.

Mheshimiwa Spika, unakuta mkulima ana eka kumi, analima tatu, eka saba hazitumii lakini anasema hizi ni za kwangu. Lakini hapo kuna fursa ya kuweka uwekezaji ambapo utapata zile nyasi nzuri za ng'ombe kutumia, kwa hiyo kwanza ukaongeza mahusiano mazuri kati ya mfugaji na mkulima, lakini ukaweka namna ambapo hata wote wawili wanaweza kushiriki kwenye ushuru na kodi kwa mfumo ambao ni rasmi.

Mheshimiwa Spika, wakati mifugo ipo hifadhini ilikuwa ni kukimbizana tu, wanakimbizana, wanatoa rushwa, wanaleta kesi na nini. Mimi nimezungumza sana na hiki chama cha wafugaji; pesa iliyokuwa inazunguka kwenye kesi na rushwa, hiyohiyo ukiigeuza ikawa kodi ni uchumi mkubwa sana. Sasa nakuomba Mheshimiwa Mpina, hebu tuanze na ukanda ule kama mfano, njoo tukuelekeze, tunaongea vizuri na chama cha wafugaji. Bahati nzuri wakishakuwa na chama ni fursa kwamba wana sauti moja, njoo tuzungumze tuondoke kwenye hiyo hatua, tumeshafanya vizuri kwenye hatua ya sheria na amri, sasa twende kwenye hatua ya tija ya hizo sheria na amri zianze kuchangia kwenye uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimefurahi, kwenye hotuba yako, sikumbuki ni ukurasa wa ngapi, umezungumzia namna ambavyo sasa nyama tunayoleta kutoka nje ya nchi imeanza kupungua, na ninadhani huo ndiyo uwe mwelekeo. Juzi mimi nimemsikia Mheshimiwa Rais anatoa maelekezo kwamba baadhi ya watu, hasa viongozi wa Serikali, pamoja na kuwa na laini nyingine za simu;nataka nitumie kama mfano; lakini lazima wawe na laini za *TTCL* kwa sababu wao ndiyo wadau wakubwa wa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuna mtu mmoja akawa anaona kwamba ni jambo limekaa vibaya, lakini mimi nikajiuliza; nina ndugu yangu aliwahi kufanya kazi *Airtel,* alikuwa ananiambia

wao kwa mwezi *Airtel* wanawapa *airtime* kwa ajili ya mawasiliano. Na jana nikamuuliza hivi ilitokea siku moja *Airtel* wakakupa *airtime* ya Tigo wakati wewe unafanya kazi *Airtel?* Akasema hapana. Kwa hiyo hiki kinachofanyika mimi nafikiri ndio mwelekeo. Hebu tutafute kuinua mambo ambayo kwanza ni ya Umma halafu twende upande wa pili, siyo kwamba *Private Sector* tuiue.

Mheshimiwa Spika, sasa niilete kwenye muktadha wa ufugaji. Ukiangalia viatu, mikanda, mabegi tunayotumia hapa Watanzania ni uchumi mkubwa sana unazunguka. Jana nimemsikia Mheshimiwa Mbunge mmoja anasema tutafute soko nje, lakini mimi nasema tuanze na soko la hapa, hebu *starve* yale mambo ya nje weka nje huko, tuhakikishe hapa mikanda, viatu, mabegi tunatumia hapa. Tuki-*starve supply* kutoka nje, hapa soko liki-*starve* wawekezaji watafanya kazi nzuri, na muwape *support,* itafikia hatua hata ng'ombe wako akipotea unakuta ameshachunwa watu wanakwenda kutengeneza mikanda kwa sababu mikanda haitoshi, utakuwa umetengeneza soko la hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini tuwasaidie na wafugaji sasa; jambo lingine katika ile niliyosema kuongeza ubora; hebu tuondoke kwenye habari ya ng'ombe, kuna mtaalam mmoja alikuwa ananiambia hapa kwamba sio kila ng'ombe ambaye nyama yake itakuwa nzuri, nyama inawekwa inavutwa hivi kama mkanda, ng'ombe anafugwa miezi 18, 16 ni nyama. Sasa sisi hapa unakuta ng'ombe ana miaka tisa, yaani tangu azaliwe anakuja kuchinjwa siku ya *graduation* ya *Form Four* ya binti au kijana aliyezaliwa wakati ng'ombe ananunuliwa. Kwa hiyo tutafute namna ya kuanza ku-*transform* ili habari ya nyama iwe ya kiwango hicho. Utaacha kununua nyama kutoka nje kuleta Serena na kwingine na mambo mengine kama hayo.

Mheshimiwa Spika, nimeskia hapa, kwenye ukurasa fulani hapa, sikumbuki, tutaona, inasema asilimia 20 ya wafugaji wa nchi hii ndio wana *access* na *extension services* (huduma za ugani); lakini hata miongoni mwa hao asilimia 20 ni tija ndogo sana inayopatikana pamoja na huduma za

ugani. Na hii inaashiria kwamba mambo aliyokuwa anasema Mheshimiwa Dkt. Nagu kama mfano, kwamba mara kuna dawa feki na vitu kama hivyo, inawezekana kweli yapo. Kwa sababu hata katika hiyo asilimia 20 ambayo wanapata huduma za ugani bado tija haipatikani, na hii nimeipata kwenye ripoti ambayo ni ya Serikali inaitwa *Tanzania Livestock Modernization Initiative.*

Mheshimiwa Spika, tumeona idadi ya ng'ombe inaongezeka, kwenye hotuba wanasema milioni 30 mpaka 32; mbuzi milioni 18, nadhani ni milioni, nafikiri niko sahihi; kondoo wanaongezeka. Lakini twende hatua ya zaidi, kutoka kwenye idadi kwenda sasa kwenye tija ya hiyo idadi. Namna gani sasa; hebu tuingize wawekezaji waende watengeneze ranchi ndogondogo kwenye maeneo ambayo wakulima...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Oscar Mukasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:...** nakushukuru sana. Mheshimiwa Stanslaus Mabura, tafadhali.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia walau machache kwenye hii Wizara muhimu kabisa, Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nijikite kwenye mambo machache ambayo kwa kweli nadhani yananipa deni sana kama sitayazungumza. Jambo la kwanza, wiki chache zilizopita nilizungumza juu ya masuala ya minada. Tunafahamu, kuna minada ya upili na minada ya msingi. Sasa miaka michache iliyopita Wizara iliamua kwa kukaa tu na kufikiria bila kuwa na sheria ambayo ingeweza kutuongoza vizuri, kwamba kwa sababu yako baadhi ya maeneo yana

minada iliyokuwa inaendelea ilikuwa imejaa sana, sasa wakaamua kuhamisha ile minada kupeleka kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana watu wa Nyamagana na Ilemela kule minada yao ya msingi ikaondolewa na kupelekwa Misungwi ambapo wakaenda kuanzisha mnada wa upili. Matokeo yake ni nini; kuhamishwa huku kwa minada kulitokana na sababu za msingi tu kwamba maeneo ya awali yaliyokuwa yanatumiwa kwa minada, kama pale Nyamagana tulikuwa na eneo pale Igoma, kwamba eneo hili limekuwa finyu sana kwa hiyo ni lazima tuhamishe mnada. Hii imefanyika pia Pugu kwenda Ruvu na sisi tukatoka Nyamagana kwenda Misungwi.

Mheshimiwa Spika, lakini hoja yangu hapa ni nini; kulikuwa na sababu gani ya kuuhamisha mnada Nyamagana ukaenda Misungwi ilihali ule mnada ungeweza kutoka eneo ulilokuepo awali ukapelekwa kwenye eneo lingine. Nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri; sisi Nayamagana tuna eneo mbadala la zaidi ya ekari 35 mpaka 50, linatosha kwa ajili ya kupata mnada mpya wa msingi ambao utakuwa Nyamagana ili tuondoe hizi kero na changamoto tunazoziweka kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, nilisema hapa mfugaji au mchinjaji anakwenda kununua ng'ombe Magu, analipa 7,500 anapewa kibali kwenda Misungwi, anatoka Magu anapitiliza mpaka Misungwi, anafika Misungwi analipa 7,500 ndipo anapewa kibali kutoka Misungwi kuja kuchinja ng'ombe Nyamagana, hii siyo sawa. Tunaongeza mzigo kwa wavuvi, tunaongeza mzigo kwa wachinjaji na hatutawasaidia sana. Kwa hiyo niombe sana Wizara kwa sababu mlishaanza kulifanyia kazi, tunaomba mnada wetu uliokuwa unatakiwa urudi Nyamagana urudi ili tuweze kuendelea na shughuli za uchinjaji na mapato ambayo yaliyokuwa yanapotea kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, la pili; tuna kiwanda cha ngozi pale Mwanza kinaitwa *Mwanza Tanneries,* imekuwa ni muda

mrefu sasa tunakipiga kelele. Viko vyuo vya ngozi lakini watu hao hata wakimaliza mafunzo hawana sehemu za kwenda kujifunza. Mimi niombe Waziri ulichukue hili, *Mwanza Tanneries* ipo, majengo yapo, mitambo yote ilishaondolewa, hebu mliangalie na hili kama ni kutafuta wawekezaji watafuteni wawekezaji waje haraka tuendelee kunufaika na huyu mnyama anayeitwa ng'ombe na kadhalika kwa ajili ya ngozi hizi ambazo kwa kweli zitaweza kutuletea pato kubwa sana kwenye taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie habari ya biashara ya mabondo; biashara hii ni kubwa sana, na Wachina wamejaa Mwanza wananunua mabondo. Bahati mbaya sana ni biashara ambayo haina bei elekezi. Mheshimiwa Waziri, inawezekana Wizara na Serikali inapoteza fedha nyingi sana. Mchina mabondo yakiwa mengi kabisa; maana hawa samaki Sangara wakati mwingine wanakufa tu na kiferezi huko kwenye maji, mabondo yanongezeka, akija Mchina haulizi bei, matokeo yake anashusha bei inakuwa ya kutupa kwa sababu mabondo yamekuwa mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hii haiwezi kuwa sahihi sana. Ni lazima tufike sehemu tuweke bei elekezi ili huyu anayechuuza na yeye kupata biashara hii asinyanyasike kwa sababu tu Serikali haijawawekea mwongozo lakini inataka kodi ya yale mabondo. Kwa hiyo lazima tuangalie maeneo yote mawili ili tuweze kumsaidia mvuvi, tuweze kumsaidia mtu anayefanya biashara ya mabondo, lakini tumuwekee mkakati huyu mfanyabiashara anayekuja kununua ajue msingi wa Serikali unataka nini kwenye biashara ya mabondo.

Mheshimiwa Spika, liko lingine, hili nafikiri baada ya Wizara kuwasilisha hii bajeti nitamwona Mheshimiwa Waziri nimletee na hawa watu, walinyanyasika sana na mzigo wao mkubwa wamedhulumiwa, lakini kila wakifuatilia baada ya maamuzi ya Mahakama wanachukuliwa hatua, inakuwa kama ni kazi ya uhasama. Sidhani kama ni vyema kulisema hapa, lakini nalisema kama *brief,* halafu nitamtafuta Waziri na hawa watu ili aweze kuzungumza nao.

Mheshimiwa Spika, lingine, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwenye suala la uvuvi wa samaki, kiukweli wamefanya kazi kubwa. Jambo lililopo sasa la uamuzi wa kutoka kwenye sentimita 50 kwenda 85 kwa kuamua kuiruhusu 85 hata kama itafika sentimita 200, huu ndiyo uamuzi mzuri na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Tunataka kama hivi jambo limetokea wamechukua hatua wamekaa wamefikiria wakaamua kwa ajili ya maslahi ya watu, hongera sana, samaki huyu mwenye sentimita 85 na kuendelea ndiyo mwenye soko na ndiye anayelipa kuliko Waziri anavyofikiria.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la nyavu, sote tunafahamu kwenye suala la nyavu, nyavu za dagaa pamoja na nyavu za sangara ambazo ni milimita nane mpaka milimita sita. Kwenye nyavu za sangara Waziri ameshafanya utafiti zaidi ya mara mbili na jambo moja kubwa tunaona kwamba nyavu za *single,* maana kuna *double* na *single,* nyavu za *single* ni ukweli kwamba pamoja na tafiti mbili alizozifanya Waziri, inaonekana bado haziwasaidii wavuvi kufikia malengo waliyoyakusudia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri turudi pale kwenye *double* wala asikate tama, arudi pale kwenye *double* ili wavuvi kulingana na mawazo wanayoyatoa kwa sababu ndiyo wako kwenye *field,* ataona matokeo yake, Serikali itapata fedha, samaki anazozitaka zitapatikana, vipimo vilivyokadiriwa vitapatikana na tutakuwa hatuna tatizo kabisa.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya yote nafahamu sasa hivi Mheshimiwa Waziri anafikiria kuwa na *pie* kati ya sita au saba, hebu nimwombe tusimame kwenye *six pie* au turudi chini kuliko kwenda kwenye...

**SPIKA:** Malizia Mheshimiwa Mabula, dakika moja.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, hizi zinaweza zikatusumbua sana kwa sababu mzigo utaenda kwa wavuvi na sio kwa watu wengine.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, nafikiri kwa leo hayo machache yanatosha, naunga mkono hoja kwa asilimia mia na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana.

Kwenye *Gallery* ya Spika, tulikuwa na mgeni maalum Mheshimiwa Waziri wa Mifugo mstaafu, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Titus, karibu Dodoma, alikuwa Mbunge mwenzetu wa Busega kipindi kilichopita na alikuwa Waziri wa Wizara hii na alifanya kazi nzuri sana hapa Bungeni.

Nakushukuru sana Daktari, karibu sana tunafurahi kuwa pamoja nawe.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara hii kusheheni mipango bado tuna changamoto za kibajeti kuminywa na huku wafugaji wakiendelea kuteseka na kero za majosho, ukosefu wa viwanda vya kuchakata bidhaa za ngozi, changamoto za malisho, upungufu wa watumishi katika sekta hii, migogoro mikubwa na tozo holela kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo; nashauri kuweka mazingira bora ya kisera na kisheria kwa Sekta Binafsi kujenga viwanda kwenye Sekta ndogo ya Ngozi na kuzalisha bidhaa za ngozi kwa wingi. Tanzania ina mifugo zaidi ya milioni 17.7 inayoweza kutoa bidhaa za ngozi isipokuwa bidhaa za ngozi zinazozalishwa ni milioni 2.6 kwa mwaka. Sehemu kubwa ya ngozi inauzwa nje bila kuchakatwa, ni 10% pekee ndiyo huchakatwa nchini. Napendekeza Serikali iweke mazingira bora ya kisera na kisheria kwa sekta binafsi kujenga viwanda vya nyama na maziwa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo inachangia asilimia 29.1 ya Pato la Taifa. Endapo tutaongeza juhudi katika uzalishaji huenda Sekta ya Kilimo ndiyo ikaleta mageuzi

makubwa nchini. Changamoto tuliyonayo ni kufeli kwa mipango ya Serikali yetu, kufungamanisha miradi mikubwa ya kiuchumi na Sekta ya Kilimo sambamba na mikakati ya kuongeza thamani kwenye uzalishaji wa Sekta ya Kilimo. Mwenendo wa takwimu za hifadhi ya chakula nchini tangu 2015 mpaka 2019 zinaonesha kiwango cha uzalishaji wa chakula kimeshuka kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia takwimu zilizotumiwa na Benki Kuu April 2019 – Hifadhi ya chakula imeshuka kwa 82.7 kutoka mwezi Machi, 2015 mpaka kufika 17.3 Machi, 2019. Ukiangalia takwimu hizo utaona Machi, 2015 hifadhi ya chakula ilikuwa tani 452,054.0, lakini kufika Machi 2019 hifadhi ya chakula imeshuka mpaka 78,336.0.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya ardhi kuongeza uzalishaji. 53.3 ya ardhi yetu ni misitu na 15.4 iliyobaki ni ardhi yenye rutuba. Sehemu kubwa ya ardhi yetu hapa nchini inafaa kwa kilimo ila uzalishaji wetu umeendelea kushuka siku kwa siku. Kumekuwa hakuna utoshelevu wa kutosha wa chakula ilhali tuna ardhi yenye rutuba isipokuwa tu na maarifa duni ya kuongeza kiwango cha uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, endapo tungekuwa na utoshelevu wa kutosha wa chakula basi hata ujenzi wa reli *(standard gauge)* unapaswa kutumika kusafirisha chakula Afrika Mashariki (Kongo DRC, Burundi, Uganda na Rwanda).

Mheshimiwa Spika, takwimu za uagizaji chakula nje ya nchi na bei za vyakula; bei zimeshuka na kuumiza wakulima, uagizaji umeongezeka kutoka dola milioni 13.3 mwezi Machi, 2018 mpaka kufikia dola milioni 15 Machi, 2019. Katika mazao sita makuu bei zimeshuka Machi, 2018 gunia la mchele 185.735.4 na sasa 168,520.5 kwa 9.3. Maharage ilikuwa 170,140 na zaidi, sasa imefikia 165,300 na zaidi kwa 2.81. Uwele gunia kutoka 76,712.1, sasa ni 75,677.4 kwa asilimia 1.3. Gunia la viazi 69,033.8 imeshuka kwa 1.0 mpaka 68,302.9. Mtama 148,8371 mpaka sasa ni 134,724.3. Hatujafanya juhudi za kutosha kutumia sehemu ya ardhi yenye rutuba.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu; ifanyike juhudi ya kuongeza thamani ya mazao kama matunda kwa kufanya *(packaging)* na *processing* ya matunda *(juice)* kuweka mazingira bora ya kisheria na kisera kwa Sekta Binafsi kujenga viwanda na kuchakata korosho. Kuweka mazingira bora ya kisera na kisheria kwa Sekta Binafsi ili kujenga viwanda vya kukamua mbegu za mazao kama alizeti. Kuweka mazingira bora ya kisera na kisheria kwa Sekta Binafsi kujenga viwanda vya utengenezaji wa nguo *(textile industries)* pamba inayozalishwa nchini ni nyingi (20) pekee huchakatwa nchini.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai kwetu sote na utashi wa kujadili maendeleo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa juhudi nyingi za kuendeleza sekta hii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Mifugo, Katibu Mkuu Uvuvi na wakuu wote wa Idara na vyuo husika kwa kazi nzuri. Natoa shukrani kwa kampuni ya *Asas,* Iringa na Tanga *Fresh,* Tanga kwa ukarimu wa kutunywesha maziwa yao leo.

Mheshimiwa Spika, leo nitazungumzia ufugaji wa kuku wa kienyeji. Awali ya yote naomba ufafanuzi wa takwimu za mifugo ya nchi hii, iliyotolewa ukurasa wa nne aya ya 10. Hivi takwimu hizi zinapatikana vipi au ni za kwenye mashamba ya Serikali tu? Mimi ni mfugaji mdogo lakini sijawahi kutembelewa na afisa yeyote anayefanya sensa ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwenye ukurasa wa sita mwanzo tunaelezwa kuwa kuku wa asili wameongezeka kutoka milioni 38.2 hadi milioni 38.5, hii ina maana kwa mwaka mzima ni kuku 300,000 tu wameongezeka. Tatizo ongezeko ni asilimia ndogo sana na ukizingatia kuwa kuku hawa wa asili ni rahisi sana kufuga kwani wao wana *scavenge in their own* na ni msaada kwa akinamama wa vijijini na vijana wetu wanaomaliza shule ambao hawana ajira. Mfano hai tumeona kwenye mradi wa *TASAF.* Swali, Serikali ina mpango gani kuwa na *local chicken gene bank?*

Mheshimiwa Spika, toka nimeingia Bunge hili la 11, kila mara namsumbua Waziri na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi,

jinsi ya kupata vifaranga hao wa kienyeji kwa ajili ya wanawake wa Kilimanjaro, lakini wananipa namba za simu ambazo hziajibiwi, ni lini sasa nitapatiwa vifaranga hao?

Mheshimiwa Spika, tatizo uchanjaji wa mifugo; ni takriban miaka 58 tangu tupate uhuru, lakini ugonjwa wa mdondo ukurasa wa sita, aya ya 16 inayosomeka mpaka ukurasa wa saba imeelezwa vizuri sana. Ni kwa nini Serikali haifanyi *mass vaccination?* Naona kwamba ni vyema chanjo hiyo na chanjo nyingine zote zikatolewa bure.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya vipaumbele katika mpango na bajeti 2018/2019 ni pamoja na kudhibiti magonjwa ya mlipuko na magonjwa ya kipaumbele (page 13:iii) ni kwa nini isiwe kuondoa kabisa magonjwa hayo ili watu wa hali ya chini wafuge kuku wa kienyeji bila hofu?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja. Pili, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayofanya ya kuleta mapinduzi ya kiuchumi katika Sekta ya Mifugo. Sekta hii ya Mifugo ilikuwa imedorora kwa miaka mingi pamoja na kuwa ni sekta muhimu kwa uchumi wa Taifa letu. Sera ya Mifugo ya mwaka 2006 na Sheria ya Nyanda za Malisho ya Mwaka 2010 zinasisitiza kwamba uchumi wa mifugo una nafasi muhimu na ya kipekee katika kujenga uchumi imara wa Taifa letu. Ili mifugo iwanufaishe wafugaji na kuliletea mapato makubwa Taifa ni lazima mifugo ipate maeneo ya malisho, maji, tiba na masoko sambamba na miundombinu ya barabara, viwanda vya nyama na mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hotuba ya Waziri imeagiza haya yote naomba atekeleze aliyoyasema kwa kuhakikisha kuwa wafugaji hasa wa asili wanapimiwa na kutengewa maeneo yao mahsusi ya kufugia. Kwa mfano, katika Jimbo langu la Longido, sisi tuna nyanda za malisho

zaidi ya 20 ambazo zikiendelezwa kwa kuchimba mabwawa na visima virefu vitawezesha ufugaji wenye tija ili viwanda vya nyama vinavyoendelea kujengwa nchini ipite rasilimali ya kutosha na yenye ubora unaohitajika. Baadhi ya maeneo yetu ya malisho yanayohitaji kuendelezwa ni pamoja na Loorboro, Oldenja na Engasurai.

Mheshimiwa Spika, tiba, chanjo na uogeshaji izingatiwe. Tatu, masoko mpaka masoko ya ndani ya uhakika yapatikane, masharti na tozo za kuuza mifugo na bidhaa zake nje zilegezwe ili wafugaji wasiendelee kuumia. Mwisho naomba Wizara izingatie na kuongeza suala la jinsi ya kukab iliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kwenye suala zima la uendelezaji wa Sekta ya Mifugo hususan nyanda za malisho na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi ya kuchangia na naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua fursa hii kwa kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia katika hotuba ya Wizara hii. Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuitayarisha na kuiwakilisha hotuba hii katika Bunge lako kwa ufasaha mkubwa. Katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Elimu na Mafunzo ya Uvuvi; nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kuweka mpango huu mzuri katika nchi yetu ambao una manufaa kwa wavuvi wetu. Katika Hotuba ya Waziri, Ukurasa wa 89 – 90 imeeleza namna ya *FETA* kwa kushirikiana na *NORGEES VEL* ya Norway iliyofadhili kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya pamoja na mambo mengine lakini zaidi kufundisha stadi za ufugaji na biashara katika maeneo kadhaa ya nchi yetu. Hili ni jambo zuri ambalo linapaswa kushukuriwa na kupongezwa. Ushauri wangu katika jambo hili ni kwamba, Wizara ipanue wigo wa kueneza jambo hili katika maeneo mengi zaidi, hasa yale ya vijijini ambako kuna wavuvi ambao uwezo wao ni mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, Migogoro Kati ya Wafugaji na Wakulima; tatizo la migogoro ya ardhi kati ya makundi haya makubwa katika nchi yetu bado ni kubwa. Ni vyema Wizara ikalichukulia jambo hili kwa uzito unaostahili ili kulitafutia ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, Mabadiliko ya Sheria milimita 10 mpaka milimita nane (8) nyavu za dagaa. Ni jambo jema kwa mabadiliko haya, lakini tatizo ni kubwa zaidi kwenye Ziwa Victoria kuliko bahari. Dagaa wanaopatikana katika Ziwa Victoria wana *size* ndogo kiasi kwamba, kuvuliwa kwa nyavu za milimita10 si sahihi na ni uonevu kwa wananchi wanaofanya kazi katika Ziwa Victoria. Ikumbukwe dagaa wanavuliwa kwa kuchotwa, kwa hiyo, mabadiliko haya yaguse pia, dagaa wanaovuliwa katika Ziwa Victoria ili pia, iruhusiwe kuvua dagaa kwa kutumia nyavu za milimita nane.

Mheshimiwa Spika, Samaki Wadogo Wasiokua zaidi ya *Size* iliyowekwa; naomba Kauli ya Serikali kuhusu uvuvi wa samaki kama furu, ngere na kadhalika. Samaki aina hii ni maalum sana kwa maeneo kama Ukerewe. Ikumbukwe kwamba, samaki hawa walianza kupungua baada ya kupandikizwa kwa sangara kwenye Ziwa Victoria, lakini badala yake wananchi ndio wanaadhibiwa kwa kuzuiliwa kuvua samaki hawa. Wananchi wa Ukerewe na maeneo mengine yanayozunguka Ziwa Victoria waruhusiwe kuvua samaki aina ya ngere, furu na wengineo ambao hawawezi kukua kufikia *size* inayowekwa na sheria.

Mheshimiwa Spika, Uvuvi wa Vizimba; urasimu ni mkubwa sana kwa watu wanaotaka kuwekeza kwenye vizimba na mchakato unagubikwa na rushwa. Kuna tozo nyingi sana mpaka kupata kibali, jambo linalokatisha tamaa. Hakuna uwekezaji wowote kwa watu hasa, vijana wanaoishi maeneo ya pembezoni mwa ziwa kama njia mbadala ya kuimarisha uchumi wa watu wetu.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, mifugo itasaidia Watanzania zaidi iwapo uchumi wa viwanda utashika kasi. Cha kushangaza ni kuwa hata viwanda vilivyopo sasa havitumiki kabisa. Nikitolea mfano, Kiwanda cha Nyama cha *SAAFI* kilichopo Sumbawanga kinasemekana ni miongoni mwa viwanda bora kabisa vya nyama, lakini baada ya uwezo wa mwekezaji mzawa kutetereka Serikali imeshindwa kabisa kuweka mipango ya kukiendeleza, badala yake ng'ombe wanasafirishwa toka Sumbawanga mpaka Dar-es-Salaam na wakati mwingine ng'ombe hupelekwa Zambia kwenye viwanda vya nyama.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara ione namna ya kukitumia kiwanda hiki. Nilipata nafasi ya kutembelea kiwanda, ni kiwanda kizuri kina miundombinu ya kisasa mingi inayowezesha mifugo wote na masalia yake yote kuongezewa thamani, ikiwemo damu, ngozi, kwato, mifupa na kadhalika. Serikali iliweza kutaka kushirikiana na mwekezaji ili aweze pia kulipa deni la Serikali na kutafuta masoko duniani. Masoko ya nyama yalipatikana sehemu mbalimbali ikiwemo Comoro, Shelisheli, Uarabuni na kadhalika, hata hivyo Serikali imekaa kimya bila kutoa uamuzi. Naomba watusaidie kiwanda kile kikifanya kazi ng'ombe wa wafugaji wa Rukwa, Katavi, wangepata soko na kuvutia ufugaji. Naomba sana Serikali isaidie kiwanda hiki kipate mtaji wa kazi na ikiwezekana isimamie yenyewe na mwekezaji yuko tayari sasa *PPP* na Sera ya Viwanda tunaitekeleza kweli namna hii.

Mheshimiwa Spika, wavuvi wananyanyasika kupita kiasi; Maafisa hawajengi mahusiano baina yao na wavuvi, mahusiano ni ya paka na panya. Nashauri Serikali ifanye mabadiliko katika kusimamia sekta ya uvuvi iwe rafiki kwa wadau wote.

**MHE. DKT. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuleta hotuba nzuri. Napenda

kuchangia maeneo mawili ya migogoro baina ya wafugaji na makundi mengine hususan wakulima na soko la samaki.

Mheshimiwa Spika, migogoro kati ya wakulima na wafugaji *(pastoralists)* imegharimu maisha ya watu, mifugo na uharibifu wa mazao. Wafugaji wanaohamahama kwa sehemu kubwa wanatafuta malisho na maji. Haya ndiyo maeneo yanayosababisha wafugaji kuchunga katika mashamba ya wakulima na wakati mwingine wanaingia katika maeneo yasiyoruhusiwa kama Hifadhi za Taifa. Hata mifugo wanaposafirishwa wakati mwingine wanaswagwa kupitia barabara kuu, wanaharibu barabara na kadhalika. Kwa nini usafirishaji wa mifugo usiwe na vyombo rasmi na inapobidi watumie *National Stock Routes*? Kama zimefifia, kwa nini zisifufuliwe?

Mheshimiwa Spika, suluhu ya migogoro ya wakulima na wafugaji kwa upande mmoja ni maandalizi ya matumizi bora ya ardhi, lakini kwa upande mwingine ni usimamizi wa sheria, sheria ndogo na kanuni zinazotawala matumizi ya ardhi. Aidha, ni muhimu Serikali ikajenga mabwawa maalum kwa ajili ya kunywesha mifugo na inapowezekana mifugo ijengewe mabirika ya kunywea maji *(cattle troughs)*. Zamani Wizara ya Mifugo ilikuwa na kitengo cha kujenga mabwawa ya mifugo, kwa sasa ni vema watumie *DDCA.*

Mheshimiwa Spika, Soko la samaki (*tuner fish);* mwaka 2017 nilifanya ziara nchini Spain kutafuta soko la samaki aina ya *tuner.* Nilichokikuta huko ni kwamba, viwanda vya kusindika samaki hao vilikuwa vinaagiza samaki kutoka China. Sina uhakika kama samaki wote wanaotoka China kweli wanatoka huko. Hata hivyo, nilipofika Spain, walinipa ripoti iliyoandaliwa na wataalam kutoka Denmark inayoonesha kwamba *tuner fish* wanapatikana kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu kwa mwaka hapa Tanzania. Naleta swali hili Wizara ilifanyie kazi; je, ni kweli upatikanaji wa *tuner fish* hapa Tanzania ni mdogo na *seasonal* kiasi kwamba wawekezaji hawavutiwi kuanzisha kiwanda? (Mheshimiwa Waziri apeleleze).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja. Pili, niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. Wamebadili sana hali ya utendaji kwa watumishi waliokuwa wanafanya kazi kwa mazoea.

Mheshimiwa Spika, haja yangu, Mheshimiwa Waziri naomba kufahamu mpango wa Wizara juu ya eneo la mafunzo kwa vijana wanaosoma Chuo cha Ngozi, Mwanza. Kiwanda cha Ngozi ambacho kilikuwa kinachukua wanafunzi na kuwapa mafunzo katika Kiwanda cha Ngozi maarufu kama Mwana *Tanneries*. Niombe kiwanda hiki kifufuliwe upya, mwekezaji apatikane ili tuongeze ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, pili, nimepokea malalamiko toka kwa wananchi wakilalamikia wafanyabiashara toka nje ya nchi wanaingia moja kwa moja viwandani na maeneo ya uvuvi ili kununua bidhaa ya samaki badala ya kununua katika soko la Mwaloni, soko ambalo liko rasmi kwa biashara ya mazao ya samaki katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, tatu, niombe Idara ya Uvuvi wafike Jimboni kutoa elimu ya ufugaji samaki wa vizimba, ukizingatia kuwa zaidi ya 80% ya eneo katika Jimbo ni eneo la maji. Naomba tutumie maeneo ya fukwe za ziwa ambayo hayatumiki kama *beach* yatumike kufanya ufugaji wa vizimba *(cape fishing)*.

Mheshimiwa Spika, nne, tunao vijana katika vikundi vya ufugaji walipata mafunzo ya awali ya ufugaji kuku, sungura na kadhalika. Niombe Wizara iwezeshe katika kuwapa mtaji ikiwemo vitendea kazi na namna bora ya ujenzi wa mabanda ya sungura, kuku na kadhalika yenye kuzingatia viwango vinavyokubalika.

Mheshimiwa Spika, tano, kuna Chama cha Ushirika cha Wavuvi ambao wameshajiunga wanasubiri uzinduzi

rasmi. Niombe Mheshimiwa Waziri awazindulie ili kufungua milango kwa wafanyabiashara wengine wa samaki na wafugaji pia.

Mheshimiwa Spika, sita, ombi maalum; naomba vifaa vya uvuvi ili kuwezesha vijana waliopo katika sekta hii ya uvuvi wavue kwa tija.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, Pongezi kwa Serikali na Wizara hii, *VAT* kwa bidhaa za maziwa hususani *(UHT Milk)* tunaomba itolewe.

Mheshimiwa Spika, Serikali iwekeze kwenye taaluma ya maziwa Vyuoni kama Shahada na Stashahada ili tupatiwe Wataalamu na kuongeza ujuzi katika Sekta hii ya maziwa.

Mheshimiwa Spika, Kwa sasa Afrika ya Mashariki Chuo pekee kinachotoa taaluma hii ya maziwa ni Egerton University ya nchini Kenya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika Sekta ya Mifugo na Uvuvi inaajiri takribani 50% ya Watanzania ambao ni zaidi ya milioni 25 na inachangia zaidi ya 6% kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uvuvi; Operesheni Jodari imeacha madhara mengi hasi kuliko chanya, Wavuvi wamepigwa, wamechomewa nyavu, vibali vimekuwa vingi, wamenyang'anywa mitumbwi na kadhalika. Naomba Serikali ifuatilie na kuona madhara yanayotokana na operesheni hii na nini kauli ya Wizara kwa Watendaji waliokiuka sheria na taratibu katika kufanya zoezi hilo na Serikali (Wizara) iko tayari kuwarejeshea wale wote walionyang'anywa vyombo vyao kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa kitoweo cha samaki; kumekuwa na changamoto na uhaba mkubwa wa

kitoweo cha samaki hasa wanaotoka maji chumvi (baharini) na ukiwauliza wavuvi, wanasema kuna makatazo kutoka Serikalini, ukiwauliza wafanyabiashara na wenye mabucha, wanasema baada ya samaki kutoka nje kukatazwa na wavuvi wetu wa ndani kuvua kwa kificho baada ya Serikali kutoa katazo na kunyanyasa wavuvi hivyo kama mfanyabiashara atabahatika kuwapata samaki wa maji chumvi basi bei huwa juu sana na hivyo hawapati wateja.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atuambie kwa nini samaki wa maji chumvi wameadimika na nini mkakati wa Wizara kuhakikisha samaki wanapatikana?

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED:** Mheshimiwa Spika, Awali ya yote inapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutupatia uhai na uzima na kuwa tunaendelea na harakati zetu kama kawaida. Pia kwa namna ya pekee napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia mada iliyopo hewani. Katika mchango wangu naomba nizungumzie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kupigwa nyavu moto, Wavuvi kunyang'anywa zana zao za uvuvi na kupigwa Wavuvi na JWTZ; kumekuwa na utaratibu kwa kipindi kirefu, wavuvi wetu kunyang'anywa nyavu zao na kutiwa moto. Ni vyema watu hawa wakapelekwa Mahakamani, Mahakama ikaamua kuliko kuamuliwa maamuzi ya aina kama hii.

Mheshimiwa Spika, niongee vipigo wanavyopata Wavuvi; kumekuwa na utaratibu mbaya sana wa kupiga wavuvi kwa visingizio mbalimbali. JWTZ Kitengo cha *Navy* kimekuwa kikipiga wavuvi, hatari sana kabisa inatisha, inaumiza lakini pia inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, niombe kwa heshima zote, Serikali ione umuhimu wa kutatua hili kwani linazidi kuleta changamoto kwa wavuvi na kwa Taifa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuchangia kuhusiana na kunyang'anya wavuvi zana zao; kumekuwa na tatizo hili

kwa kipindi kirefu sana, wavuvi wetu wamekuwa wakinyang'anywa zana zao kama nyavu, mashine, mitungi ya gesi. Kwa nini baada ya kunyang'anywa vifaa hivyo hawapelekwi kwenye sheria Mahakamani, matokeo yake vifaa hivyo vinabaki kwa wale waliokamata hadi lini? Tunaweza kusema wananyang'anywa na hawapewi vifaa vyao?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri na Naibu Waziri, pamoja na Wataalam kwa hotuba na pia kwa kazi nzuri ya kusimamia Wizara hii muhimu. Pamoja na mikakati mizuri ya Wizara iliyoonyeshwa kwenye bajeti hii, kuna changamoto nyingi ambazo nashauri Wizara ichukue hatua za kutatua. Napendekeza, Wizara kujenga mabwawa ya maji kwa wafugaji wa Kata ya Mjelena Mshewe, katika Wilaya ya Mbeya ili kukabiliana na ukame.

Mheshimiwa Spika, napendekeza hatua zichukuliwe za kulinda hali ya mazingira ya Ziwa Rukwa ambalo kwa kiasi kikubwa linazidiwa na mchanga unaotokana na mmomomyoko wa mito inayoingiza maji katika Ziwa Rukwa. Pia hatua za makusudi zichukuliwe za kuhamasisha vijana kuanzisha miradi ya ufugaji samaki katika Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara iangalie uwezekano wa kuanzisha shamba ka kisasa la mifugo ya ng'ombe wa nyama na pia ujenzi wa kiwanda cha nyama katika eneo jipya lililotengwa na halmashauri kwa kunenepesha mifugo na kiwanda cha nyama. Halmashauri imetenga zaidi ya eka 6,000 katika Kata ya Mjeta ili kubadilishana na eneo la iliyokuwa *Tanganyika Packers* ambayo kwa sasa limezungukwa na Mji Mdogo wa Mbalizi. Eneo hili jipya litawezesha Wilaya ya Mbeya kuzalisha ng'ombe wa kiwango kizuri sana na kuweza kukidhi ushindani wa soko la Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inapaswa kushirikiana na Wizara ya Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhakikisha kwamba mipango kabambe *(master plan)* za kila Jiji, Manispaa na Wilaya zinalenga maeneo ambayo ufugaji na uvuvi unaweza kufanyika ili kuepusha migogoro na kuhakikisha uendelevu. Katika muktadha huo niombe katika majumuisho Wizara ieleze iwapo ilipewa nakala ya *master plan* ya Jiji la Dar es Salam na iwapo imeshatoa maoni ya kuboresha *master plan* ya Jiji mintarafu masuala na mipango ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salam ni mtaji mkuu wa uvuvi kwa upande wa nchi yetu ya Tanzania, hata hivyo yamekuwepo malalamiko ya kuletwa kwa samaki wa sato na aina nyingine kutoka nje ya nchi ambao wamekuwa chini ya kiwango. Aidha, hata kwa samaki ambao wamekuwa wakifugwa kwenye mabwawa wamekuwa wakipewa muda wa wengi na kuwa baadhi ya kuku aina ya *broilers*. Hivyo, Wizara iwe na mikakati thabiti ya kudhibiti ubora wa samaki kutoka nje ya nchi na ubora wa samaki wanaofugwa katika mabwawa.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri yametolewa maelezo kuhusu utatuzi wa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ambayo yanaonyesha bado Serikali haijawezesha utatuzi kamili na endelevu wa migogoro hiyo. Hivyo, katika majumuisho ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi iwasilishe Bungeni taarifa juu ya utatuzi wa migogoro yenye kuorodhesha migogoro iliyopo na kwa maeneo ambayo migogoro haijatatuliwa bado iwekewe *road map* ya utatuzi wa migogoro hiyo ambayo pamoja na mambo mengine itaeleza ni lini migogoro hiyo ikatatuliwa. Pia Wizara ya Fedha kwa kuwa suala hili ni mtambuka ieleze ni lini itaongeza fedha kwa Wizara zote zenye mipango ya upimaji wa ardhi ili kuwezesha ardhi ya nchi yetu kupimwa na kupangwa kwa ajili ya maendeleo endelevu ikiwemo ya mifugo na uvuvi nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine naomba kupitia mchango huu Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)*

itenge eneo katika ardhi yake ya Mkoa wa Pwani kwa ajili ya vijana wa Jimbo la Kibamba kulitumia kwa ajili ya ufugaji ikiwa ni sehemu ya mchango wake katika kuongeza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, suala lingine muhimu kupewa kipaumbele ni nafasi ya Bodi ya Maziwa katika kuhamasisha unywaji wa maziwa ikiwemo kwa wanafunzi wa shule mbalimbali. Hivyo, naomba Bodi itekeleze kampeni maalum katika Shule za umma za msingi na sekondari katika Jimbo la Kibamba ya kuhamasisha wanafunzi kunywa maziwa kwa kushirikiana na wasindikaji mbalimbali wa maziwa.

**MHE. LUCIA M. MLOWE**: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ufugaji wa samaki; kwa kuwa kuna umuhimu sana wa wananchi kupata lishe ya samaki ambapo samaki hawana madhara kama nyama, naiomba Serikali itoe elimu kwa wananchi namna ya kufuga samaki. Pia samaki hao watawapatia wananchi kipato.

Mheshimiwa Spika, nyavu za uvuvi kumekuwa na uchomaji wa nyavu holela kwa wavuvi. Hii siyo sawa, naomba kuishauri Serikali nyavu zinazochomwa basi zirudi kiwandani zikarekebishwe.

Mheshimiwa Spika, wataalam; kwa kuwa sekta ya ufugaji na uvuvi haina wataalam wa kutosha, naomba Serikali iajiri wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE**: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipanga na imepanga kuendelea kujenga Mabwawa na malambo kwa ajili ya kunyweshea wanyama (Mifugo). Je, ni lini sasa mabwawa

na malambo hayo yatajengwa katika Jimbo la Kavuu Halmashauri ya Mpimbwe Mkoa wa Katavi?

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kuhamisha ufugaji wa kuku wa kienyeji katika maeneo ya kijijini hasa katika maeneo ya vijijini kama maeneo ya Jimbo la Kavuu?

Mheshimiwa Spika, kupitia Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Wanyamapori iainishe mipaka kati ya hifadhi na matumizi ya mifugo.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kuwapongeza Mawaziri husika. Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mheshimiwa Ulega, pamoja na Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Hotuba yao nzuri ya bajeti iliyowasilishwa hapa Bungeni. Sasa naomba kutoa maoni yangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya malisho kutokana na kutokuwa na Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi, hivyo kusababisha migogoro kati ya Wakulima na Wafugaji.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wilaya katika Mkoa wetu wa Kagera wana maeneo maalum ya malisho hasa yale yaliyokuwa *Ranch* za Taifa lakini kwa Jimbo la Ngara hakuna maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine tuliyonayo ni ya masoko ya mazao ya mifugo, mfano ngozi, maziwa, nyama pamoja na mayai ya kuku.

Mheshimiwa Spika, sababu zinazofanya ngozi nyingi kuwa na ubora wa chini ni pamoja na upigaji wa chapa ovyo hususan katika maeneo muhimu ya ngozi, hali mbaya ya miundombinu ya machinjio, makaro, mabanda ya kukaushia na kuhifadhia ngozi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina utajiri mkubwa wa mifugo ambayo ingezalisha ngozi kama malighafi za viwandani na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, shughuli za ufugaji wa samaki nchini unafanywa na wafugaji wadogo wadogo kwa asilimia kubwa. Ufugaji wa samaki hukabiliwa na matatizo na changamoto nyingi, kama ukosefu wa teknolojia bora, upungufu wa vifaranga bora na miundombinu ya usafiri kuwa duni.

Mheshimiwa Spika, changamoto katika sekta ya uvuvi inakabiliwa na upungufu katika sera na sheria, elimu duni juu ya shughuli za uvuvi katika jamii, uvuvi uliopitiliza na hivyo kuathiri rasilimali za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mwendelezo wa wavuvi kuchomewa nyavu zao za kuvulia kila mara na kumekuwa na matamko kutoka Wizara husika juu ya matumizi ya nyavu sahihi za kuvulia.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, ushauri wangu; tafiti zinaonesha Ranchi za Taifa ni takribani hekta 200,000, lakini ng'ombe wa Serikali ni chini ya 30,000 na hivyo ranchi hazitumiki ipasavyo. Nashauri tujifunze kutoka Botswana, Serikali ikodishe kwa unenepeshaji na wafugaji walipe kodi.

Mheshimiwa Spika, ranchi zote zinazomilikiwa na wakubwa zifanyiwe *auditing* ili zile zinazo-*operate under performance* zirejeshwe kwa wafugaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, mashamba makubwa ya *NAFCO* ambayo hayajaendelezwa huko Simanjiro, Monduli Juu, *West Kilimanjaro,* yarejeshwe kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, nashauri tozo ya 30,000 kwa ng'ombe *export tax* ipunguzwe iwe 15,000.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ifuatilie ng'ombe walioshikiliwa na maliasili maana wanakuta na wamekaa muda mrefu, hata baada ya kushinda kesi.

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia upande wa uvuvi. Wavuvi wa Mkoa wa Tanga wana malalamiko makubwa sana juu ya nyavu zao ambazo tamko lililotoka warudishiwe lakini mpaka leo hawajarudishiwa ukizingatia wanategemea shughuli za uvuvi kusomesha watoto na kuendesha shughuli zao za familia kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tozo na faini zimekuwa nyingi, lakini kwa nini Serikali isijikite kutoa zaidi elimu kwa watu hawa ili kupunguza matatizo yanayosababisha tozo hizo?

Mheshimiwa Spika, tunaomba tupatiwe kiwanda cha kusindika samaki, Tanga samaki ni wengi ila masoko na sehemu ya kutunzia ni tatizo. Hivyo, tusaidiwe kiwanda Mkoa wa Tanga kitakachosaidia hata kwa upande wa ajira. Pia mitaji hasa kwa vijana ambao wanajua uvuvi lakini wanazagaa tu kwa kukosa vitendeakazi. Vile vile iwasaidie hata kuboresha mazingira yao ya kuvulia, ikibidi hata wakopeshwe.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo tuna migogoro mingi sana kati ya wafugaji na wakulima, hasa Wilaya ya Handeni Kata za Misima, Sindeni, Kwamatuku, Mkata na Ndolwa. Tatizo la ni malisho ya mifugo, kesi ni nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote niiombe Wizara ione umuhimu wa kutoa zaidi elimu kwa wafugaji na hata wavuvi ili kuboresha shughuli zao. Mfano mdogo ni Tanzania kuwa *termed* chini ya kiwango cha kutumia maziwa kilichowekwa na *FAO* huku tukiwa na mifugo ya kutosha. Hapa tatizo ni elimu, wapewe elimu na mazingira bora ili wapate matokeo yaliyo bora zaidi. Pia wahamasishwe kujiunga katika vikundi ambavyo vitawasaidia sana katika kupata matokeo yaliyo bora na kulinda pamoja na kutunza

mazingira ya kazi zao wakati huohuo kufuata sheria na taratibu za nchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja iliyo mezani ambayo tukiamua kama nchi kuwekeza kwenye sekta ya kilimo na uvuvi tutapata faida kubwa kwa kukuza uchumi wa wananchi wetu na pia Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa bajeti zinazotengwa kwenye Wizara hii ni ndogo sana na haziendi zote na kwa wakati. Leo tunaona idadi ya kupeleka nyama nje ya nchi ni sawa na kiwango ambacho tunaingiza nyama kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, hapa ni kwamba sisi tunapoteza maana tuna mifugo mingi; hivyo ili tukawe mosi tuanzishe viwanda vingi vya kusindika nyama na kuchakata *byproducts* nyingine kama vile ngozi, kwato, pembe *etc*. Ili sasa tuweze kumudu kuhudumia soko la ndani na kuondoa uingizwaji wa nyama kutoka nje ya nchi. Pia tunaongeza idadi ya kupeleka nyama na mazao (*By-products*) nyingine za mifugo nje ya nchi. Hii itakuza sana uchumi wa nchi maana tunakuwa na *foreign currencies* nyingi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba kunakuwa na mazingira mazuri kwa wawekezaji kwenye sekta ya mifugo na uvuvi. Kwa mfano kwa kutafuta masoko, kuondoa tozo, ushuru kwenye bidhaa hizi hasa zile ambazo hazitoshi na nchi wananchama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa mfano *export levy* kwenye ngozi.

Mheshimiwa Spika, hii inachangia sana kuua soko la ngozi na Watanazania wengi wameathirika na hapa Tanzania hamna viwanva vya kutosha ku- *absorb* ngozi zote. Tozo hii iwe *discouraged* kabisa kwenye uwekezaji kwenye ngozi; na sasa ngozi nyingi zinaharibika kwenye maghala.

Ngozi mwaka 2015 ilikuwa imeanza shilingi 20,000 lakini sasa ni shilingi 1,000, tena wanakubembeleza ununue.

Mheshimiwa Spika, wakati awali ilikuwa unaweka *booking* na *payment* in *advance*, hii ni mbaya sana, inabidi Serikali ijue kuwa siku hizi kuna teknolojia ambayo mataifa kama China wana uwezo wa kutengeneza *products equivalent* na ngozi bila kutumia ngozi za wanyama *(Artificial leather)*. Sasa *with artificial leather* na bado kuna hizo tozo za *export levy* ni dhahiri hizo ngozi zetu zitaendelea kuoza kwenye maghala. Hivyo naishauri Serikali waone umuhimu wa kuondoa hii tozo ya kusafisha.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa uvuvi pia mazao yetu kama samaki na dagaa pamoja *byproducts* za daa (vyakula vya kuku) haviuziki kwenye masoko ya nchi jirani kama vile Kenya, Uganda, Congo n. k. Kuna *export levy* ya 80.16 kwa kila kilo moja ya dagaa, hii inasababisha bidhaa za dagaa zinazotoka Tanzania kuwa ghali sana na hivyo kusababisha bidhaa zetu kutouzika kabisa. kwa mfano mfanyabiashara wa Tanzania tozo na ushuru mbalimbali kwa tani 10 inagharimu takribani shilingi 4,800,000 lakini yule wa Uganda anagharimu shilingi 800,000. Sasa hapa utaona ni jinsi gani bidhaa zetu hazina thamani hata soko nyuma. Maana ni ghali sana hivyo hujikuta hawauzi bidhaa/dagaa zao.

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi Serikali inatoza hii tozo hata kwenye dagaa/chakula cha kuku kwenda miji ya pembezoni; mfano Mbeya, Tunduru, Sirari, Ruvuma etc; nao wanalipa nao *export levy*. Hii si sawa maana hawa ni Watanzania na hili linasababisha dagaa kuuzwa kwa bei kubwa sana. Nashauri Serikali kuondoa hii tozo ili bidhaa zetu ziwe sindanishi. Hii ni muhimu sana katika kukuza sekta ya uchumi na kuwapa unafuu wafanyabishara wa dagaa.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu kufunguliwa kwa Mnada wa Magena ambao umekuwa ukiuliza maswali hapa na kueleza umuhimu wa mnada ule ambao ungetoa fursa

kwa wananchi wa Tarime na kukuza uchumi wa nchi yetu na ule Tarime.

Mheshimiwa Spika, upande wa pili, Kenya, wana Mnada wa Maabera ambao ambao upo mpakanikabisa, chini ya kilometa tatu. Hawa wanapata faida na tunakuza uchumi wao. Mheshimiwa Mwigulu alipokuwa Waziri mwaka 2016 yeye na watendaji walifika na kutembelea Mnada wa Kirumi na ule wa Magena ambao miundombinu ipo. Huu mnada tulikubaliana ufunguliwe siku moja baada ya ule wa Kirumi ili tuweze pata faida.

Pili, ilivyo sasa mifugo ya Rorya, Serengeti na Tarime inaenda maabera Kenya moja kwa moja; na ilivyo sasa kuna mianya mingi ya rushwa na upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Spika, mnada ule ulifungwa kwa sababu ya wizi mwaka 1997. Hata hivyo wote ni mashahili, hali Tarime sasa ni shwari, mifugo inapita kutoka mikoa mingine kwenda Kenya badala ya kuuziwa pale Magena. Hii ni fursa tunayoichezea Watanzania. Ijulikane tu kuwa Kenya wanategemea ng'ombe kutoka Tanzania; inashangaza tunapoteza fursa kwa mambo ya kisiasa na si. Kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pia alikuja Mheshimiwa Waziri Tizeba na watendaji wakaahidi kuufungua lakini nashangaa kuna nini nyuma ya pazia.

Mheshimiwa Spika, hata alivyokuja Mheshimiwa Rais Julai 2018 alielekezwa mnada wa Magena aufunguliwe. Nashangaa hata amri ya Mheshimiwa Rais inapuuzwa! Wananchi wa Tarime tungependa kujua kwa nini miradi hii inapotezewa? Hata jengo la mazao ya kimataifa la Remegwe limetelekezwa. Naomba tujulishwe hatua ya mnada wa Magena maana muhtasari upo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza sana

Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho zuri na lenye kuleta matumaini.

Mheshimiwa Spika, suala la bandari ya uvuvi limekuwa linasuasua kwa muda mrefu sana. Mwaka wa fedha 2013/2014 zilitengwa fedha kwa ajili ya *pre-feasibility study* na kiasi cha shilingi milioni 500 na mshauri elekezi alilipwa na kazi ilifanyika na mpaka sasa hatujui matokeo ya kazi ile. Baadaye fedha zimekuwa zikitengwa kila mwaka kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, hata bajeti hii tunayoitekeleza 2018/2019 zimetengwa fedha kwa ajili ya bandari hiyo ya uvuvi lakini hatuoni matokeo yeyote; na mpaka sasa hata eneo la kujenga bandari hiyo bado halijapatikana. Kwenye bajeti ijayo kupitia kitabu chake Mheshimiwa Waziri anaomba aidhinishiwe shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya kazi ileile ya ushauri elekezi.

Mheshimiwa Spika, faida za bandari ya uvuvi ni nyingi ikiwemo utoaji wa ajira kwa vijana wetu nimuombe Mheshimiwa Waziri kuwa sasa fedha hizi bilioni 1.4 ziende na kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, uvuvi katika bahari ni fursa ambayo nchi inatakiwa iitumie vema. Kwa sasa uvuvi katika Bahari Kuu umedumaa na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu. *Deep Sea Fishing Authority (DSFA)* kwa sasa ipo katika hali mbaya sana. Mamlaka hii haipati bajeti yeyote kutoka Serikalini na inaendeshwa kwa mapato ya meli za uvuvi za kimataifa zinapokata leseni ya kuja kuvua katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilianzisha tozo ya dola 0.4 kwa kilo ya samaki itakayovuliwa. Baada ya kuanzishwa kwa tozo hii nchini wamegoma kuleta meli zao katika eneo letu hili la *EEZ (Exclusive Economic Zone)*. Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri na Serikali Kuu kwa ujumla waifute tozo hii ili kuokoa mamlaka yetu hii.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikifuta tozo hiyo Serikali ianze kujipanga kwa kununua meli zake zenyewe za uvuvi wa Bahari Kuu sambamba na ujenzi wa bandari ya uvuvi kama nilivyoandika hapo awali. Nimeona kwenye hotuba kuwa Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kufufua Shirika la Uvuvi (TAFICO) pamoja na mipango ya kununua meli mbili za uvuvi; hili ni jambo jema. Niiombe Serikali sasa iongeze kasi ya kutekeleza malengo haya.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Kuhusu Hifadhi ya Bahari Mafia (MPRU) Taasisi hii imepewa Mamlaka ya kuwekeza katika visiwa vidogo vya uvuvi. Mwekezaji huyu amekumbwa na changamoto za kutoshirikisha Mamlaka za Halmashauri ya Wilaya kwenye kutoa vibali stahiki kama vibali vya ujenzi. Nikuombe Mheshimiwa Waziri Mamlaka hii ya MPRU ampe maagizo ya kufuata sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni hili linalohusu vifaa vinavyotumia *FAD'S (Fishing Aggregating Devices);* tunaomba viletwe Mafia kwani kwa sasa wavuvi wanatumia njia za kutosa magari mabovu baharini na kuchafua mazingira.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Spika, Fungu 99 Sekta ya Mifugo. Changamoto kubwa ni migogoro inayowahusisha wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi pamoja na sheria kandamizi kwa wafugaji ambayo hutumiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, ng'ombe wakiingia kwenye hifadhi wanakamatwa na kutaifishwa, kutozwa *fine* kila ng'ombe mmoja Shs. 100,000; mchungaji hutozwa *fine* ya laki 300,000/= na mwenye ng'ombe kufungwa.

Mheshimiwa Spika, kwafano mfugaji Wambura wa Serengeti alipigwa *fine* ya shs. 5,000,000/=, kifungo miaka mitano na ng'ombe 294 kutaifishwa. Hiyo siyo halali kwa kuwa ukisha muadhibu si vema kutaifishiwa ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri naomba kuwe na mpango mkakati wa kuwasaidia wafugaji na kuwatembelea kwenye maeneo yao na kuwasikiliza.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Kero ya Usafirishaji wa Mifugo kwa Kutumia Malori. Kuna utozaji wa ushuru wa *SUMATRA* na *TANROADS*. Tunaomba ifuatilie kujua uhalali huo.

Mheshimiwa Spika, Ushindani Usio Sawa Hususan Bidhaa Mpya ya UHT. Sasa hivi ni viwanda vinne tu ndivyo vinazalisha maziwa kwa kutumia *product* ya ndani. Viwanda hivi vinanunua maziwa kwa wafugaji wetu na kutengeneza UHF. Cha kusikitisha hivi viwanda vinne vinavyonunua maziwa kwa wafugaji wa ndani hawakupewa punguzo la kodi. Ila Azam anayesindika maziwa ya unga kutoka nje ya nchi na kutengeneza UHT amepewa punguzo la kodi kwa asilimia 87.5

Mheshimiwa Spika, natoa ushauri kwa kuweza kulinda watu wetu wawekezaji wanaonunua maziwa kwa wafugaji kupewa punguzo.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Uvuvi. Mheshimiwa Waziri nachangia kuhusu maziwa madogo, kati na mabwawa. Ninatambua lengo la kuimarisha usimamizi, uendelezaji, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na utunzaji wa mazingira.

1. Unyanyasaji, kwa wavuvi, wachuuzi na watumiaji wengine wa samaki.

2. Kufunga maziwa kwa muda wa miezi sita wakati huo mvuvi amelipa leseni ya mwaka moja.

3. Kufunga maziwa kunasababisha wachuuzi wanaotegemea mboga kukosa huduma hiyo kwa miezi sita.

4. Hawa wote kushindwa kujikimu kwa maisha yao kwa kuwa hawana pato lingine ni kuwatia umaskini.

Mheshimiwa Spika, nashauri maeneo yote ya mazalio ya samaki yasivuliwe kwa muda wote na mwaka mzima ili wavuvi nao wavue kwa muda wote kwa kuwa hiyo ndiyo sehemu ya kipato.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuwepo mahali hapa nami niweze kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Mwaka 2019/2020. Halikadhalika nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri. Hotuba hii inakwenda kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa kuhakikisha sekta nzima ya mifugo na uvuvi inaendelea kuimarika kama ilivyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuanza kwa kutoa pongezi kubwa kwa Serikali kwa kuendelea kuimarisha sekta ya mifugo na uvuvi kwa kushirikiana na sekta binafsi. Aidha, katika mwaka 2018/2019, Serikali imetuambia ilianzisha dawati la sekta binafsi kwa ajili ya kutatua changamoto zinazowakabili wawekezaji katika sekta za mifugo na uvuvi. Lengo la Serikali ni kuongeza uwekezaji wenye tija utakaowezesha wafugaji na wavuvi kuongeza kipato, kuzalisha malighafi za kutosha za viwanda na kuongeza mchango kwenye Pato la Taifa. Hatua hiyo ni muhimu sana kwa maendeleo chanya ya sekta hii.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba sekta ya mifugo na uvuvi inakua na mnyororo mpana wa ongezeko la thamani kwa kutoa kipaumbele katika ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na uvuvi, hatua ambayo inakwenda moja kwa moja kuazimia ile hoja ya kuwa na Tanzania ya Viwanda. Hadi sasa viwanda 99 vya kusindika mazao ya mifugo vimeanzishwa vikiwemo viwanda 17 vya nyama, 76 vya maziwa na sita vya ngozi, hatua ambayo itawasaidia wafugaji na wavuvi hasa kupandisha thamani ya bidhaa zao. Vilevile katika mwaka 2019/2020 Serikali imeendelea kuweka msisitizo katika kuwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu

katika uwekezaji kwenye viwanda, kuimarisha usimamizi wa rasilimali katika ukanda wa uchumi wa bahari na bahari kuu; na kuimarisha miundombinu na kukuza biashara ya mazao ya uvuvi. Aidha naishauri Serikali kutoa elimu kwa wavuvi wetu hasa katika Nyanja ya uvuaji wa Bahari Kuu ili sasa na wao waweze kushiriki kwa namna moja katika kukuza uchumi wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Sasa Naomba Nizungumzie Changamoto Zinazotukabili Kibaha Vijijini. Katika Jimbo letu tumeendelea kuwa na migogoro ya wafugaji na wakulima, migogoro hiyo inasababisha kuzorotesha hali ya kiuzalishaji wa kiuchumi kwani muda mwingi wananchi wamekuwa katika migogoro hiyo. Ninaishauri Serikali kuchukua hatua kadhaa zitakazowezesha kupunguza migogoro hiyo, hasa kwa kufanya upimaji wa maeneo yote ya ufugaji wa Kibaha Vijijini ili yajulikane kwa kuweka alama maalum ili kuepusha mwingiliano kati ya wafugaji na wakulima. Aidha Kata ya Kwala kujengwe Ranchi ya kufugia ili wafugaji wakafugie mifugo yao huko. Kufanya hivyo kutapunguza migogoro iliyopo kati ya wafugaji na wakulima ambayo imeendelea kudumu kwa muda mrefu bila kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya kwenye Wizara hii katika kusimamia majukumu yao ya kila siku ili kuhakikisha masuala yahusuyo mifugo na uvuvi yanatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Maoni; fedha zinazotengwa katika Wizara hii hazitoshi kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Naishauri Serikali itenge fedha za kutosha na pia fedha hizo zitolewe kwa wakati ili miradi iliyopangwa iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuondoa gharama za leseni katika vyombo vya uvuvi kama ilivyo katika trekta. Naishauri Serikali kutokana na wingi wa ngozi

zinazotokana mara baada ya kuchinja mifugo yetu kwa ajili ya nyama. Vijengwe viwanda vya kutosha hapa nchini mwetu vya uchakataji wa ngozi ili kuweza kupata ajira pia kuongeza Pata la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iboreshe majosho yote nchini kwa ajili ya mifugo; na majosho hayo yatumike kwa mifugo tu na si shughuli zingine za kibinadamu. Naishauri Serikali itenge maeneo maalum ya malisho ya mifugo mifugo ili kuondoa kabisa migogoro iliyopo sasa baina ya wakulima na wafugaji ya kugombania maeneo kwa ajili ya kilimo kwa wakulima na kwa ajili ya malisho kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuzingatia sheria na kanuni zilizopo pindi mifugo ikikamatwa. Kuna baadhi ya watendaji wa Wizara hawafuati sheria na taratibu zilizopo; hutaifisha mifugo hiyo ambapo ni kinyume cha sheria na kuanza kuipiga mnada na hivyo kuendelea kuleta mahusiano mabaya baina ya watendaji na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ipunguze tozo katika maziwa. Kwa mfano katika usindikaji wa maziwa, ladha ya maziwa, vifungashio na leseni za usafiri. Naishauri Serikali Ranchi zote walizopewa wawekezaji na kushindwa kuziendeleza zirudishwe Serikalini ili Serikali iweze kuziendeleza kwa kuziboresha na hatimaye zitumike kama maeneo ya malisho kwa wafugaji waishio pembezoni mwa ranchi hizo. Pia ranchi hizo zitumike kama shamba darasa kwa wafugaji wetu ili kuepuka kutohamahama kwenda kutafuta malisho.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iboreshe vyombo vya uvuvi katika bahari kuu. Pia kuwepo na meli kubwa za uvuvi. Ili viwanda viweze kupata malighafi za kutosha pia itapunguza uingizwaji wa samaki kutoka nje ambapo wakati mwingine samaki hao si bora kwa mlaji au kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, pia naishauri Serikali ijenge viwanda vya kuchakata samaki katika mikoa iliyopo pembezoni mwa Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Spika, mwisho nawatakia Waziri na Naibu Waziri afya njema na umri mrefu katika kuyatekeleza majukumu yao ya kila siku.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza wote ndani ya Wizara katika utendaji wao wa kazi nzito kutokana na wengi wao ambao ni wafugaji na wavuvi ni wananchi wa kawaida, ambao wanahitaji kupewa elimu ya kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa ufanisi na tija kwa mapato yao. Hivyo hazina waone umuhimu wa kuongeza ukomo wa bajeti na fungu la miradi ya maendeleo kuweza kutolewa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuona umuhimu wa vikundi vya akina mama wanaojikita kwenye ufugaji wa kuku kama miradi ya kuwapatia uchumi kwa kupambana na umasikini. Akina mama wamekuwa na uwezo mdogo wa kufuatilia vifaranga na utunzaji wa vifaranga hivyo hadi kufikia kutoa mazao tarajiwa ya mayai au nyama, kuwa na gharama kubwa. Tunaomba Wizara/Serikali kuona utaratibu bora wa kuboresha utunzaji wa kuku wa kienyeji ili kuweza kuzalisha mayai na kutoa nyama kwa mahitaji makubwa kwa wananchi wetu, na kwa kuwa hawana gharama kubwa na wanastahimili madhara stahili kwa wastani mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wamekuwa wanasafiri sana maeneo mbalimbali ili kutafuta malisho. Hivi kwanini Serikali isiweke utaratibu wa mashamba ya malisho na yakafahamika na kuwaelimisha wafugaji kulima mashamba hayo kwa idadi ya mifugo yao? Pia tuone utaratibu wa kuboresha mifugo ya asili kulika kupandikiza wa kutupatia mifugo chotara na kusababisha kupotea kwa mbegu ya asili ya mifugo yetu.

Mheshimiwa Spika, jitihaa ya Wizara kutuwezesha kupata samaki wakubwa na wenye tija wa kuwapatia mapato ya kutosha wananchi wetu. Kikubwa tutoe elimu kwa wahusika na uvuvi na ufugaji kwa maendeleo na kukuza uvuvi na ufugaji bora nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziro Mpina, Naibu Waziri Mheshimiwa Ulega, Makatibu Wakuu na Watendaji wa Wizara ya Mifugo kwa hotuba yao nzuri ya bajeti iliyowasirishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nitoe mchango wangu kwa mambo yafuatayo;

Mheshimiwa Spika, Makusanyo ya Maduhuli. Niipongeze Wizara kwa juhudi kubwa sana ya ukusanyaji maduhuli ya zaidi ya asilimia 183. Hii imeonesha jinsi mlivyo makini sana. Yapo malalamiko kwa baadhi ya wavuvi ambao wamekuwa wakilalamikia watendaji wa Wizara kuwatoza faini kama kuna kosa lakini risiti wanayopatiwa inaandikwa kiwango kidogo cha fedha. Je, Serikali inatambua hilo? na je, hatua gani zinachukuliwa kwa watendaji kama hawa wanaoiibia Serikali na kuwanyanyasa wafugaji na wavuvi?

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya Halmashauri watendaji wa Serikali wamekuwa wakiwanyanyasa wafugaji. Je, Wizara imejipangaje kuona utaratibu wa sheria na kanuni zinafuatwa kumlinda mfugaji?

Mheshimiwa Spika, Maeneo ya Malisho na Migogoro ya Wafugaji. Serikali inaweka mkakati gani wa kuhakikisha inamaliza mgongano wa wafugaji baina ya wakulima na dhidi ya hifadhi za taifa kutokana na upungufu wa maeneo ya malisho?

Mheshimiwa Spika, wafugaji wamekuwa wakinyang'anywa mifugo yao na askari wa wanyamapori na kusababisha unyanyasaji mkubwa sana na wananchi kufilisiwa. Je, huwa wanatumia sheria gani?

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Sekta ya Maziwa. Serikali imejipangaje kusaidia viwanda vya maziwa nchini kwa kuondoa tozo nyingi? (ukurasa wa 28) kulinda viwanda vyetu

na kuvutia wawekezaji wa nje na ndani ikiwa ni pamoja na kuongeza ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, pia changamoto nyingine ni wingi wa taasisi za kudhibiti na ukaguzi zipatazo 11 ikiwa ni pamoja na kutoza kila *flavor* katika maziwa.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Serikali itupatie mkakati wa kukuza sekta hii ya maziwa. Naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Makatibu Wakuu na timu yote.

Mheshimiwa Spika, nilishaongea juu ya josho eneo la Linga (Keta), suala la samaki wadogo (vituwi) lifanyiwe utafiti ili Wananchi wanufaike na samako hao, kuboresha mialo, mazingira ya uvuvi, pamoja na umuhimu wa boti.

Mheshimiwa Spika, ukopeshaji/ruzuku ya *engine* za boti isiwe lazima kwa vikundi kwani katika vikundi wakati mwingine uwajibikaji huwa ni dogo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hata kama atanunua mmoja bado hawezi kuvua pake yake na ajira zitakuwa nyingi na uvuvi utaimarika. Ubinafsi ndiyo zana kuu ya kumhamasisha mjasiriamali, 'kwamba ninanufaika vipi?'

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, Madaktari wa Mifugo. Kumekuwepo na upungufu mkubwa sana wa madaktari wa mifugo na kupelekea mifugo kufariki bila ugonjwa kutambulika na kueneza magonjwa hovyo. Pia kumekuwepo na kutopatikana kwa dawa za mifugo. Kwa mfano, unakuta kuna ugonjwa wa kichaa cha mbwa na chanjo hazipo na madaktari wa mifugo hawapo. Je, Serikali ina mikakati gani

ya kuhakikisha madaktari wa mifugo na dawa zinapatikana? Siku za nyuma, madaktari walikuwa wanatembelea wafugaji na kutoa chanjo. Je, ni lini utaratibu huu utarudi?

Mheshimiwa Spika, sekta ya mifugo; wafugaji wengi wanajitahidi sana kufuga kisasa na kuzalisha maziwa mengi ambayo yangeweza hata kuuzwa nje, kutengeneza *cheese*, siagi na kupata nyama; lakini tatizo bado Serikali haijaweza kushirikiana kati ya Wizara na Wizara. Kwa mfano Wizara ya Mifugo kujenga viwanda vya maziwa ili kuweza kuwapatia wafugaji masoko. Je, nchi kama Tanzania kuna sababu ya kununua maziwa, siagi, *cheese* kutoka nchi za nje? Ardhi tunayo, mifugo tunayo, wafugaji wapo shida ni nini?

Mheshimiwa Spika, Ushauri; Serikali ijitahidi kila sehemu yenye wafugaji ihakikishe inajenga majosho ya kutosha ili wakati wa kiangazi mifugo isife kwa kiu; na ni vizuri kufanya hili katika kila Wilaya.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, nyavu za kuvulia dagaa milimita sita zimezuiliwa Tanzania lakini Kenya na Uganda zinatumika bila kuhojiwa na Ziwa Victoria ni lile lile. Jambo hili si sawa, litazamwe upya.

Mheshimiwa Spika, *operations* zinazofanyika hazipati maelekezo ya awali ya *AG.* Ni vyema Mwanasheria Mkuu wa Serikali akatoa maelekezo mahsusi kwa watendaji hawa ili utekelezaji wa sheria ufanyike bila kuonea wananchi. Kwa mfano, makosa ya uvuvi kutolewa adhabu za mazingira, rushwa na wizi wa waziwazi unafanyika.

Mheshimiwa Spika, ufugaji wa samaki kwa vizimba umegubikwa bado na urasimu mkubwa. Leseni ni nyingi, masharti ni magumu sana kwa wananchi wa kawaida. Hivi kwanini zana za kutengenezea vizimba hazipo/haziruhusiwi hapa nchini? Wizara inaniapa vibali kuagiza toka Kenya mara kwa mara, hii ni aibu. Utaratibu ufanyike, wawepo wauzaji maalum wa zana hizi.

Mheshimiwa Spika, Soko la Samaki la Nyakarilo hadi leo halijafunguliwa. Naomba katika kuhitimisha hoja itangazwe kufunguliwa kwa soko hilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango kwa njia ya kuzungumza, naongeza kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nishauri juu ya uvuvi wa bahari kuu. Baada ya kuanzisha Shirika la Uvuvi *(TAFICO),* hakuna haja ya kusubiri kununua meli zinazomilikiwa na Serikali, waalike wawekezaji walio tayari kufanya kazi kwa kushirikiana na *TAFICO.* Walete meli zao, *TAFICO* ishirikiane nao tupate japo kidogo hicho tunachokosa. Serikali ipitie upya sekta ya uvuvi wa bahari kuu na kufanya maamuzi kwa mwongozo ulio sahihi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweza kudhibiti uvuvi haramu. Mafanikio ni kuwa samaki wameongezeka, wale wenye ubora unaotakiwa. Ushauri kwa Serikali ni kuwa Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa uvuvi haramu haurejei tena. Eneo lenye mapungufu ni watendaji wa Wizara na idara za uvuvi, hawa ndio wanaohamasisha uvuvi haramu. Katika Mkoa wa Kagera maeneo ya visiwani, *compliance* iko juu sana ila sehemu za karibu na nchi kavu uvuvi haramu umeanza kurejea tena.

Mheshimiwa Spika, Niishauri Serikali Juu ya Sekta ya Maziwa. Sekta hii ni moja ya sekta zenye fursa kubwa ya kujenga uchumi jumuishi. Taarifa za wataalam wa sekta ya maziwa nchini Uganda wanasema Tanzania kwa uchache tuna fursa ya kuzalisha na kuchakata lita milioni nne kwa siku. Uganda kwa sasa wanazalisha na kuchakata lita milioni mbili kwa siku ukilinganisha na lita 150,000 kwa siku kwa nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ili Tanzania iweze kufikia kiwango hicho kwa kuazima uzoefu wa Uganda tunapaswa kufanya

yafuatayo; moja, Serikali itenge maeneo sehemu za wafugaji nchi nzima kwa kuanzisha *semi free range animal keeping.* Wafugaji wasaidiwe kuendeleza maeneo hayo kupewa mitamba huku Serikali ikitegemea kupata uwekezaji wake kwenye maziwa yatakayouzwa.

Mheshimiwa Spika, pili, soko la maziwa ni kiwanda, viwanda vyote vya maziwa vipewe vivutio kadiri inavyowezekana. Punguzo/upotevu wa ushuru/tozo kwenye viwanda vitarejeshwa kutoka kwenye kipato cha wananchi na sekta za kuzalisha maziwa zitakazoshamiri.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia *NARCO* inaendesha zoezi la kugawa vitalu vya ufugaji Mkoani Kagera. Tatizo langu kwa zoezi hili *NARCO* na Wizara wanarudia makosa yaliyofanyika miaka ya 2005. Maamuzi ya Serikali ya mwaka 2005 juu ya ranchi za Mkoa wa Kagera tume nyingi ikiwemo ile ya makatibu wakuu sita ziliikataa. Tume ya makatibu wakuu sita iliundwa na Mheshimiwa Dkt. Magufuli akiwa Waziri wa Mifugo na hata akiwa Mkoani Kagera amekuwa akilaani ugawaji huu wa maeneo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali katika zoezi hili izingatie yafuatayo:-

(a) Imalize migogoro ya ugawaji wa mwaka 2006, kwetu Muleba. Tunashauri vijiji vyetu vinne na vitongoji virudishwe kwa wananchi.

(b) Kabla ya kugawa maeneo, lazima wazingatie mahitaji ya vijiji jirani ambavyo hutegemea mbuga hizo kuchunga ng'ombe wao.

(c) Mkoa wa Kagera unahitaji na kutegemea sekta ya maziwa. Yatengwe maeneo mahususi kwa ajili ya wawekezaji waliotayari kujenga viwanda. Wawekezaji hao wapewe vivutio vya ziada kwani sekta hii inajenga uchumi jumuishi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Uvuvi; nishauri Serikali kuhakikisha kunakuwepo na meli za uvuvi kwa ajili ya kuvua katika vina virefu. Ilitokea wakati ambapo meli za kigeni zilivua samaki wakubwa katika kina kirefu na kupata samaki wengi na wakubwa. Hii inaonesha tulivyo na utajiri mkubwa katika bahari yetu inayotuzunguka.

Mheshimiwa Spika, nishauri Serikali kuongeza vifaa vya doria kwani maharamia baharini wako wengi hivyo kutushia uhai wa wavuvi katika bahari yetu.

Mheshimiwa Spika, Uhaba wa Viwanda vya Kuchakata Mazao ya Baharini. Ninaishauri Serikali kuhakikisha inawekeza katika viwanda vya kuchakata mazao ya baharini.

Mheshimiwa Spika, Mabwawa ya Kufugia Samaki. Wananchi wengi wanahitaji elimu ya ufugaji samaki katika mabwawa. Watu wengi wamehamasika sana juu ya ufugaji samaki lakini elimu hawana ya jinsi ya kutengeneza mabwawa na jinsi ya kuzalisha wa samaki.

Mheshimiwa Spika, Mifugo. Nipende kuishauri Serikali kuondoa uchapaji ng'ombe ambao unasababisha uharibifu wa ngozi, pia kupunguza thamani ya ngozi hizo na kukosa soko la kimataifa.

Mheshimiwa Spika, nishauri Serikali sehemu zilizo na mifugo kujengwa viwanda ili kuondoa adha hii ambayo inawapata wafugaji kupata masoko bora na rafiki. Usafirishaji kupeleka mbali imekuwa ni shida na ghali, hivyo kuwakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kuhakikisha inasimamia thamani ya nyama inayoliwa; mabucha mengi yanatoa huduma ya nyama isiyo salama kuanzia uchunaji hadi ukataji buchani.

**SPIKA:** Baada ya hayo, sasa naomba nimwite kwa sababu ya hali ilivyo nina majina kadhaa lakini sasa muda haupo upande wetu, naomba moja kwa moja nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri sasa aanze kutupitisha kwenye hoja zetu nyingi ambazo tumekuwa tukizitoa tangu jana mpaka leo. Karibu sana Mheshimiwa Abdallah Ulega.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi naomba nichukue fursa hii kumshukuru kwanza Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuweza kushiriki vyema katika shughuli hii ya bajeti ya Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi. Pili, nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuzungumza hapa na tatu, kwa namna ya kipekee kabisa, nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuhakikisha kuwa wakati wote anaendelea kutusimamia na kuhakikisha kuwa nchi yetu inasonga mbele kwa yale yaliyokusudiwa katika Taifa letu ya kuwaletea maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo mazuri anayotupatia wakati wote na kutusimamia katika kuhakikisha tunamsaidia vyema Mheshimiwa Rais wetu. Kwa namna ya kipekee pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri wangu Luhaga Joelson Mpina, Makatibu Wakuu wetu wote wawili wa Mifugo na Uvuvi Profesa Elisante Ole Gabriel na Dkt Rashid Tamatamah kwa namna tunavyoshirikiana na watendaji wote pale Wizarani katika kusukuma mbele gurudumu hili la Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi ambayo ni Wizara yenye tija kubwa na inayogusa Watanzania walio wengi na hapa leo Waheshimiwa Wabunge wamethibitisha jambo hilo pia.

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kuwashukuru Kamati yetu ya Bunge na Wabunge wote waliochangia katika hoja hii inayotuhusu ya Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi kwa sababu tumepata wachangiaji wengi sana. Hii imetupa moyo mpana sana na kwa niaba ya Waziri wangu ni lazima nitoe shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa sababu hatukuamini kwamba tungeweza kupata

wachangiaji wa namna hii wa kutushauri na kutuelekeza pia vile vile ya namna bora zaidi ya kwenda mbele hatimaye kuyapata matokeo tarajiwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze katika hoja. Hoja zimesemwa nyingi sana na Waheshimiwa Wabunge katika upande wa Mifugo, lakini vilevile katika kupande wa Uvuvi. Nijielekeze kidogo katika upande wa Uvuvi; jana katika miongoni mwa wachangiaji waliochangia na mmoja leo amerudia kuonesha kuwa katika kipindi chote tulichohudumu Serikali ya Awamu ya Tano, haijafanya jambo lolote katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika sekta hii ya Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba watembee kifua mbele, yako mambo ya msingi tuliyoyafanya na mimi ninayo Ilani ya Uchaguzi hapa na nitaeleza baadhi ya mambo ambayo Serikali ya Awamu ya Tano imeyafanya. Wabunge waliopata nafasi na kusema kwamba hakuna kilichofanyika, kwanza nianze na ibara hii ya 27 ya Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, eneo la (p); kuendelea kupambana na uvuvi haramu ili uvuvi uwe endelevu na wenye tija. Jambo hili Waheshimiwa Wabunge wengi wanaweza kuwa wasijue kuwa limeandikwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Mapinduzi kinataka samaki tulionao leo tuendelee kuwa nao kesho na hata vizazi vyetu vikute samaki hawa na ndiyo maana kikaelekeza Serikali yake kwamba tulinde rasilimali zetu hizi. Sisi tumeifanya kazi hii kama ni kazi ya kipaumbele katika kulinda rasilimali za nchi yetu ziinufaishe nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie wewe mwenyewe na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, jambo hili limeleta tija kubwa sana. Uvuvi haramu kwa upande wa bahari ya hindi ulikuwa umekithiri, ulikuwa ni uvuvi wa mabomu, leo katika upande wa bahari ya hindi hauwezi kusikia bomu linapigwa kuanzia Tanga MOA, hadi Mtwara

kule Msanga Mkuu hakuna bomu linalopigwa. Tumedhibiti kwa zaidi ya asilimia 99, hakuna bomu linalopigwa na Watanzania wa upande wa huko pwani wameanza kusahau habari ya bomu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni mafanikio makubwa bomu liliua watu, bomu lilitishia hata usalama wa baadhi ya miundombinu yetu ikiwemo hata bomba letu la gesi linalotoka Songosongo kuja Somanga kwa ajili ya gesi inayoenda kuzalisha umeme pale Kinyerezi, sisi tumeweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine mmoja kati ya wachangiaji jana alikuwa anazungumzia juu ya ujenzi wa bandari ya uvuvi. Katika kazi tuliyoifanya kipindi hiki ni kufufua shirika letu la *TAFICO,* hii ni hesabu nyepesi sana tu. Tumenunua ndege, tusingeenda kununua ndege, isipokuwa kwanza tuwe na shirika imara la kuzisimamia zile ndege, ndiyo maana tukaimarisha *ATC,* hatuwezi kwenda kununua meli, nani atakayezisimamia zile meli, ndiyo maana tukasema ni lazima tufufue *TAFICO*. Ufufuaji wa TAFICO ndiyo utakaokwenda kusimamia zile meli tunazozitegemea kuzinunua.

Mheshimiwa Spika, nataka niwapeni habari njema *TAFICO* imefufuka tena mwanamama mmoja mahiri tumempa kazi ya kuhakikisha *TAFICO* inafanya vyema. Tumetambua mali zote za *TAFICO* na *TAFICO* sasa ipo na imeanza kazi na tayari tuna uhakika wa kupata takriban kiasi cha shilingi bilioni nne kununua meli, meli ambazo zitafanya kazi ya kuvua katika maji yetu ya ndani kwanza, tunafanya hivyo kwa nini?

Mheshimiwa Spika, tunafanya kwa sababu tunataka tuioneshe dunia kwamba tunazo rasilimali, tuwavute wawekezaji, watu walikata tama, hawawezi kuamini kwamba hapa katika maji yetu sisi wako samaki, mwekezaji wa kuweka kiwanda au mwekezaji wa kuleta meli haji tu bila ya kuwa na uhakika wa kuweza kufanya *investment* ile ambayo anaweza kwenda kuifanya pale.

Mheshimiwa Spika, sisi tumetengeneza mkakati na hivi leo *TAFICO* inatengeneza *business plan* ya kisasa ambayo itakwenda kuhakikisha kuwa inaingia hata mikataba. Tunao Wakorea, wameonesha nia ya kushirikiana na *TAFICO* na tutakwenda kujenga bandari ya uvuvi. Hao Wajapan pia vile vile wameonesha nia ya kushirikiana na *TAFICO* ambayo itaenda kutuletea tija katika shughuli hizi za uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Ilani pia ya Uchaguzi imetuelekeza juu ya kuhakikisha kuwa tunalinda matumbawe yetu, maeneo ya mazalia ya samaki kwa upande wa kule pwani, hili tumefanikiwa. Kwa nini tumefanikiwa? Upande wa kule pwani tumedhibiti, watu wa Kilwa hapa kama wapo wananisikia na watahakikisha kwamba jambo hili ni la ukweli wa kiasi gani. Pale Kilwa tumedhibiti miamba yetu. Pweza walikuwa wakipatikana kwa uchache sana, pweza ni biashara ambayo inauzwa ndani, lakini tuna-*export* pia vile vile kwa kupitia mradi maarufu wa *SWIOFISH,* tumefanikiwa kudhibiti na sasa wanapata mazao ya kutosha watu wa kule pwani kwa ajili ya kuweza kuinua maisha yao, hiyo ni kazi yetu sisi.

Mheshimiwa Spika, Ilani imetuelekeza pia vile vile tutengeneze matumbawe yasiyokuwa ya asili ambayo tumeyatengeneza pale Bagamoyo na kule Nungwi, tumepeleka ya kutosha, hizi zote ni kazi tulizozifanya.

Mheshimiwa Spika, Ilani katika eneo (d) linatuelekeza sisi kuimarisha Masoko yetu ya Feri na kuimarisha Masoko yetu ya Kirumba. Katika jambo tulilofanikiwa ni hilo, tumeimarisha Soko letu la Feri na tumeimarisha Soko letu la Kirumba. Kirumba kabla sisi hatujaingia katika kupewa dhamana hii na Mheshimiwa Rais, nataka niwahakikishie ni eneo ambalo lilikuwa linakwenda vizuri, lakini sivyo kama tunavyokwenda hivi leo. Kirumba sasa inakusanya kwa mwezi mmoja milioni 600, eneo ambalo tulikuwa tunakusanya milioni 30; kutoka milioni 30 mpaka milioni 600 kwa mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hi kuwashukuru na kuwapongeza sana watendaji wote,

Mheshimiwa Mbunge wa Ilemela Dkt. Angelina Mabula na wengine wote pale Mwanza kwa namna walivyotuunga mkono katika kuhakikisha Soko la Kirumba linafanya vizuri. Soko la Kirumba limetengenezewa mzani wa kisasa, unapima mazao yetu yote yanayoingia pale. Tulikuwa tunapoteza pesa nyingi sana kama Serikali, hivi leo tunafanya vizuri. Pale feri tunafanya ukarabati mkubwa sana, tunapeleka zaidi ya bilioni 1.5 pale kulifanya Soko la Feri liwe soko la kisasa, nani anasema Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi haijatekelezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nilimtaka awepo hapa ili nimwoneshe kwa namna gani, kazi kubwa tuliyoifanya. Wabunge wa Chama cha Mapinduzi litakapokuja suala la Uvuvi, nawaomba watembee kifua mbele, Serikali ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imefanya kazi kubwa na itaendelea kufanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa mifugo, nataka nikuhakikishie kwamba tumefanya kazi kubwa. Jambo moja amelisema jana Mheshimiwa Mbunge Jackline Msongozi, naomba niende na hilo tu, mwaka 2016/2017, wakati Mheshimiwa Rais anakwenda kutembelea pale Tanga alipita katika Kiwanda cha Tanga *Fresh* akaona liko tatizo la ardhi na mtaji wao ni mdogo, akawawezesha. Wale watu wa Tanga *Fresh* hawakuwa wanazalisha maziwa ya *long life*, hivi leo wanazalisha maziwa ya *long life,* tunajivunia, hata maziwa ya kutoka nje yasipokuwepo Tanga *Fresh* na *ASAS* wote tumewawezesha sisi. *ASAS* wamewezeshwa kupitia ubunifu, ubunifu uliofanywa na Waziri wangu Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, tumeanzisha dawati la sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dawati la sekta binafsi tumelizindua sisi wenyewe mwaka jana mwezi wa 10, limeleta tija kubwa, limesaidia viwanda vya nchi hii, limesaidia wavuvi wa nchi hii, tuna ushirika leo. Ushirika unajibu Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ushirika pale Kikumba Itare tumewapelekea milioni tano, nimekwenda kukabidhi mimi mwenyewe. Pale Igombe, Mwanza tunawapelekea milioni

tano, anakwenda kukabidhi Mheshimiwa Waziri. Tumepeleka kila mahali, tunainua ushirika na kama haitoshi tumepeleka hata pembezoni ambako wanakwenda kufanya mabwawa, pale Peramiho kwa Mheshimiwa Jenista tumekwenda kuwasaidia waweze kuanzisha mabwawa ya ufugaji wa samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeanzisha Chama Kikuu cha Ushirika katika nchi ambacho kinawaunganisha wavuvi wote kwa lengo na nia tuwakopeshe zana za uvuvi, tuwasaidie wakopeshwe pesa na mabenki waweze kupata tija ya kazi yao wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote kazi inaendelea na sisi hatutakata tamaa katika kuhakikisha kazi hii tuliyopewa ya kulisogeza Taifa letu mbele, ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais, hatutarudi nyuma, tutaendelea kusonga mbele, upungufu ule mliotueleza sisi kama wanadamu tutaufanyia kazi katika kuhakikisha kuwa Taifa letu linasonga mbele katika rasilimali zake hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa muda huu wa kuweza kuchangia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega kwa maelezo mazuri sana, japo muda ulikuwa ni mdogo sana, lakini umeutumia vizuri. Tunakushukuru sana, niliona hata Mheshimiwa Selasini akipiga makofi, nikaona Mheshimiwa Gimbi Masaba akitabasamu kabisa mtani wangu huyo, natumaini mambo ni mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, tutakapoanza jioni Mheshimiwa Waziri atapitia sasa baadhi ya hoja hizi na kuweka sawasawa kwa lengo la kuweka uelewa wa Waheshimiwa Wabunge vizuri zaidi. Mheshimiwa Waziri wa Fedha msaidie bwana meli ya uvuvi ili tupunguze ngebe kidogo, tutenge pesa tupate meli za uvuvi ili hii *TAFICO* hii inayofufuka sasa ifanye vitu vyake.

Tutaendelea jioni saa 10.00 kamili na mjadala wetu wa Mifugo na Uvuvi ambapo mtoa hoja atakuwa anahitimisha. Naomba sasa niwaombe muwahi kurudi ili tufanye kazi yetu vizuri na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 10.00 kamili jioni.

*(Saa 6.54 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10:00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu!

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea Waheshimiwa Wabunge, na kwa hiyo sasa nimwite mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina ili aje haitimishe na kujaribu kutoa ufafanuzi kwa hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Waziri karibu sana, unayo saa moja ya kufanya hivyo, karibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru sana Mwenyenzi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele hapa ili niweze kuhitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru sana wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge

kwa uwezo na umahili mkubwa mnaounesha katika kuliendesha Bunge letu Tukufu. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana kwa dhati Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umakini wake wa kusimamia shughuli za Serikali hapa Bungeni. Aidha, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia hoja yangu niliyoiwasilisha hapa Bungeni kwa michango yao mizuri na ya kina yenye lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingi zimetolewa, na hii ni dalili ya dhati kwamba upo mwamko mkubwa sana upande wa kuendeleza sekta ya mifugo na uvuvi ili ziweze kupiga hatua zaidi katika maendeleo. Aidha, katika michango hiyo imedhihilisha wazi kuwa kuna mahitaji makubwa ya kusimamia sekta ya mifugo na uvuvi kupitia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali inayoongoza Wizara yangu. Ni dhahili kuwa masuala ya kuendeleza utafiti wa mifugo na malisho ikiwa ni pamoja na kuendeleza kosafu bora za mifugo ili kuongeza tija katika uzalishaji wa maziwa, nyama, mayai na ngozi kuendana na mnyonyoro wa thamani wa uchumi na viwanda. Aidha, tafiti mbalimbali zinahitaji kuendelea kufanyika kwa nyakati tofauti zenye lengo la kujua rasilimali za uvuvi ikiwa ni tafiti katika ukanda wa bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja mbalimbali katika Wizara yangu ambapo wapo jumla 46**.** Sitawaja majina yao lakini walichangia kwa kusimama 29 na ambao wamechangia kwa maandishi ni 17. Michango ya Waheshimiwa Wabunge wote niliowataja ilikuwa mizuri sana na iliyosheheni busara na heshima na hekima na changamoto. Aidha, si rahisi kujibu kwa kina na kutosheleza hoja zote za Waheshimiwa Wabunge kwa muda huu mfupi. Naahidi kwamba hoja zote tutazijibu kwa maandihsi na Waheshimiwa Wabunge wote watapewa.

Mheshimiwa Spika, ushauri na maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji umezingatiwa.

Pia maombi ya Kambi ya Upinzani vilevile yamezingatiwa isipokuwa moja tu. Mchango wa kambi ya upinzani safari hii ulikuwa mzuri sana, isipokuwa pendekezo moja tu lililosema kwamba Wizara itumie sera za CHADEMA. Wizara haitatumia sera za CHADEMA kwa sababu sera za CCM ni nzuri na hazina mfano kwa hiyo hakuna sababu yoyote ya kutumia sera za CHADEMA, zinajitoshereza. Kwa hiyo sera hapa ni za CCM na ilani hapa itatumika ya CCM.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumze kuhusu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Hoja zilizozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ni nyingi mno, kama nilivyosema. Kwa hiyo nitajaribu ambazo nitaweza kuzifikia ili kuweza kutoa ufafanuzi huo kwa Wabunge. Moja ni hili la Mheshimiwa Mzee wangu Lubeleje Mbunge wa Mpwapwa la kuhusu kituo cha tariri. Kilichofanyika pale hatuja hamisha kituo cha utafiti cha tariri tulichohamisha ni Makao Makuu. Makao makuu ni Mkurugenzi ni mambo ya utawala si mambo ya kiutafiti tena. Kwa maana ya kituo cha utafiti bado kipo pale, kwa hiyo mzee wangu Lubeleje hana sababu yoyote ile ya kukamata shilingi kwa hoja hiyo, kwa sababu kama wananchi wa mpwapwa kituo chao hatujakiondoa cha utafiti. Walioondoka ni hao wakurugenzi ambao wanawajibika kwa mambo ya kiutawala ndio tuliowaleta hapa.

Mheshimiwa Spika, la pili Waheshimiwa Wabunge mmezungumzia hoja mbalimbali za uvuvi na mifugo. Sasa katika hoja za uvuvi baadhi yake ikiwa mmesisitiza sana kwamba sheria kuharakisha mchakato wa kuboresha sera na sheria za uvuvi. Awali niliwaambia kwenye hotuba kwamba tumeamua kwa dhati kuhakikisha kwamba sheria ya uvuvi namba 22 ya mwaka 2003 pamoja na kanuni zake za mwaka 2009 tumekubaliana kama wizara tumezifumua na tumetembea kwa wadau kanda zote kutaka mawazo yao. Tayari sasa hivi mchakato Serikalini unaendelea.

Mheshimiwa Spika, na kama tulivyowaahidi Waheshimiwa Wabunge sheria hizi zitafika mikononi mwenu Ili muweze kutushauri kadri matakavyoweza ili tuweze kutengeza kanuni au sheria zitakazoendana wakati wa sasa

na kuondoa changamoto zilizopo. Sasa sioni tatizo tena la lawama juu ya Wizara kwa sababu maamuzi ya Wizara ni maamuzi makubwa, kuamua kufumua sheria yote ili tuweze kupata maoni mengi. Lakini vilevile kuamua kufumua mpaka kanuni ili tuweze kupata maoni mengi. Kakini vilevele hata katika kufumua kanuni hiyo ndiyo maana tukaamua kwamba yapo mambo ya dharura ambayo inapaswa yafanyike sasa hivi kwa haraka sana kwa sababu yalikuwa yanakwaza sana wavuvi. Kwa hiyo nilitegemea kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi mngeyashangilia.

Mheshimiwa Spika, Moja uvuvi wa ukanda wa bahari kuu ambao unalazimisha watu kuvua kwa kutumia nyavu za mm 10 ilikwepo kwa mijibu wa sharia; kuvua kwa tumia mm 10. Wananchi wakalalamika, Waheshimiwa Wabunge mkalalamika, Serikali ikakubali kurekebisha sheria na kanuni zimesainiwa na *GN* ipo tayari na leo mnondoka na *GN* hiyo. Wananchi wa ukanda wa pwani hawawezi tena kukamtwa kuzuiwa kuvua kwa kutumia mm nane. Sasa hizo ni *achievement* zenu wala si za Wizara, mliishauri Wizara, Wizara hii ya Serikali ya Awamu ya Tano ambayo ni nyenyekevu sana na sikivu imetekeleza.

Mheshimiwa Spika, lakini ukanda wa Ziwa Victoria, ukomo wa kuvua samaki wa sentimita 85; kwamba huruhusi kuvua samaki wa sentimita 85 napo Serikali imesikia. Katika kufanya hiyo tumekubali tumerekebisha, tumeondoa ukomo huo ambapo sasa wananchi wa ukanda wa ziwa victoria watavua bila ukomo. Tunahakikisha kwamba hairuhusiwi kuvua chini ya sentimita 50. Lakini huku na kuendelea kwa maana ya samaki sangara mtaendelea kuvua samaki wa urefu wowote ule. Hii ni *mileage* kubwa upande wetu kwa sababu viwanda vingi vitapata malighafi nyingi lakini vilevile uzalishaji wa bidhaa kama mabondo utazalishwa kwa wingi sana. Hata hivyo hili nalo ni la kwenu Wabunge mlilalamikia na kuomba Serikali ifanye na tumetekeleza, tatizo nini tena?

Mheshimiwa Spika, mmesema kwamba wananchi wanahangaika kupata leseni kila wilaya; na ninataka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja hii

mmsifikie mahala mkajisahau kwamba maji yalipo kwenye eneo lako kama ni ziwa lipo pale Sengerema eti lile ziwa ni la Sengerema, msijisahau hivyo. Kama bahari ipo rufiji usijisahau ukasema hiyo bahari ni ya rufiji, hiyo bahari ni rasilimali ya taifa, ya wananchi wote, mkatushauri kama Serikali kwamba kwa nini mwananchi akate leseni kila wilaya?Wakati mwingine uko ndani ya maji, unavua hujui kama umefika chato, hujui kama umefika Sengerema. Unavua, unavua tu unaenda. Hujui kama umefika Tanga hujui kama umefika Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kila unafika unakamatwa unaambiwa kata leseni nyingine, tukakubali tuka-*amend* sheria. Sasa mnataka Serikali yenye usikivu wa aina gani? Tume-*amend,* tumekubali tumrekebisha sheria wananchi sasa hivi watavua maji yote. Uikata leseni ya Bahari ya Hindi ukanda wa pwani utavua kote. Ukikata leseni ya kuvua ziwa victoria utavua ziwa lote. Ukikata leseni ziwa Tanganyika utavua ziwa lote; sasa hiyo ndio Serikali sikivu.

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge sisi tuko vizuri kuwasiliza sana tu. Mmezungumzia wala kukosekana wa uwiano wa sheria za uvuvi katika nchi za Afrika Mashariki. Mimi nataka kwanza Waheshimiwa Wabunge mjivunie sana na haya mafanikio, kwa sababu haya mafanikio sisi tungewafuata wenzetu. Tulipokwenda kufanya Oparesheni Sangara Ukanda wa Ziwa Victoria watu wote walisema kwamba Kenya wenyewe hawana masharti hayo na hawana sheria hizo Tanzania sisi tuna sheria hizo; sasa kama tunakwenda maana yake sisi tutakuwa *looser*. Nataka niwahakikishie, sisi ndio tuna maji mengi, kama ni *looser* sisi tungekuwa ni *looser* namba moja. Ziwa victoria sisi tuna asilimia 51. Hatuweze tukawa tunawafuata watu, kwamba Kenya wapo hivi lazima na sisi tuwe hivyo. Wakibadilisha leo, wanabadilisha kesho tunabalisha tena kwa sababu Kenya wamebadilisha?

Mheshimiwa Spika, lakini sisi tuka-*stick* tukasema lazima oparesheni ziendelee. Leo baada ya taasisi za kiutafiti za nchi zote tatu wote wanaipongeza Tanzania. Tatifi ambazo

zimefanywa na *TAFIRI* pamoja na taasisi zingine za kitafiti za Kenya na Uganda baada ya samaki kuongezeka kwa muda mfupi sana katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hilo mwaka 2016/2017 kwa samaki waliokuwepo Ziwa Victoria; uvunaji wa samaki katika ziwa victoria ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati tunaanza oparasheni samaki wachanga ziwa victoria walikuwa asilimia 96.6 samaki wachanga, yaani lile ziwa lilikuwa na samaki wachanga wote. Baada ya oparasheni asilimia ya samaki wachanga imefikia asilimia 62.8, imeshuka. Vilevile samaki waliofaa kuvuliwa wakati tunaanza oparesheni Ziwa Victoria ilikuwa ni asilimia 3.3. Sasa kama ni asilimia 3.3 ndio samaki wanaofaa kuvuliwa; leo samaki wanaofaa kuliwa ziwa wamefikia asilimia 32. Sasa walikuwa wanazidi asilimia 85 ambao ndio samaki wazazi Ziwa victoria walikuwa 0.4, na leo wapo asilimia 5.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urefu wa samaki sangara wastani ulikuwa 16 leo urefu umefikia urefu umefikia wastani wa sentimita 25.2; haya ni mafanikio makubwa. Nchi zote zinajivuni kwa hatua ambazo zimechukuliwa na Tanzania, na wanaendelea kuwekeza viwanda mbalimbali na sisi tutaenda kuwekeza viwanda, na ndiyo maana tukakubali kurekebisha hata kuruhusu kuvua samaki wa zaidi wa sentimita 85 kwa sababu moja kwamba samaki wazazi sasa hivi tunaona wengi. Sasa una 0.4 Waheshimiwa Wabunge unataka uvue kwa utaratibu unataka, una samaki wazazi 0.4 lile ziwa victoria tungefunga uvuvi isingewezekana uvuvi kufanyika, 0.4 za samaki wazazi tulikuwa tunaenda kumaliza lile ziwa. Sasa tuna asilimia 5.2, ni samaki wengi. Kwa hiyo sasahivi tunafunga uvuvi hii viwanda vingi vitajengwa na wananchi wengi watanufaika sana na uwekezaji huu.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Kuwepo kwa Faini ya Gandamizi Sisizozinga Sheria. Waheshimiwa Wabunge hakuna namna yoyote Serikali hii ya Awamu ya Tano na Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi ninayoingoza ambayo inaweza kuwavamia wananchi kwenda kuwaongea bila sababu;

hakuna namna yoyote ile na hatuwezi kufanya hivyo na hatuna sababu ya kufanya hivyo. Waheshimiwa Wabunge hili jambo ni vizuri likaeenda case by case. Kwa sababu mnapolileta hapa kwa ujumla wamepigwa wananchi wameumizwa bila hata kueleza ni wapi walipoumizwa na wapi walipopigwa imekuwa ikituleta changamoto sana. Mara nyingine tumekuwa tukifuatilia ukweli tunaokuta kule sio ule. Sheria za Serikali zilizopo Serikali ndizo itakazo zifuata. Sheria hizi zimetungwa na Mbunge, hili hakuna namna yoyote ya Bunge hili kuzikana hizi sheria.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya Mwaka 2003 imetungwa na Bunge hili. Kanuni za mwaka 2009 ziliinidhishwa kutumika kulingana na sheria iliyokuwepo; kwahiyo hakuna namna yoyote ya Bunge kujitoa katika utungaji wa sheria. Kwa hiyo tunafika kwenye jambo hili, na bahati nzuri mnaweza mkawa mnatuona Naibu Waziri yupo, Makatibu wa Wakuu wapo kuchambua *case by case.* Sasa hivi imeripotiwa *(be reported)* hoja ya Tunduma, ya kwamba watu hawana leseni tu wamepigwa faini milioni mbilimbili. Lakini ukweli si huo, tumefuatilia kwa kina, wale watu wana *under declaration.* Mtu ana tani 20 anaandika tani tano, anaandika tani 10. Sisi mnapotuambia *internally* tutafuatilia kwa kina kujua kama tatizo ni la mtumishi tutamshughulikia yule mtumishi. Kama tatizo ni mambo mengine tutashughulika nayo. Kwa hiyo nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuwe pamoja katika ulinzi wa hizi rasilimali.

Mheshimiwa Spika, na operesheni hizi, tumesema mudawote, zimekuwa zikifanyika kwa nia njema, na katika hili hakuna atakayepona, yoyote atakamatwa kuhusu zoezi hili la watu kujishughulisha na uvuvi haramu. Sasa uvuvi haramu huu wakati mwingine nyingine hata Wabunge wengine hapa tunageukana. Akisha kamatwa ndugu yako au mtu wako wa karibu tayari unaigeuka Wizara, tayari unawageuka watumishi wa Wizara hiyo. Kwamba ni watumishi wabovu, amezungumza hapa Mheshimiwa Tizeba. Tizeba alikuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi; amezungumza hapa, mambo mengine nitayasema baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hili la vijana kusema wanaonea watu kwenye jimbo lake si kweli. Mheshimiwa Tizeba akiwa waziri amekuwa akipigia simu vijana wa mifugo na uvuvi kuwa-*harass* na kuwaambiwa hataki watu wake wakamatwe kwa ajili ya uvuvi haramu. Mheshimiwa Tizeba amekuwa akiwa-*harass* vijana wa uvuvi, hata sasa hivi akiwa mbunge, akisema kwamba hataki mtu wake akamtwe kwenye eneo la lake la uvuvi. Sasa ukifika hapa unabadilika inakuwa hawa vijana kwa sababu hawapo ndani ya Bunge hili wanashutumia kwa kiwango hivyo, si vizuri.

Mheshimiwa Spika, wapo vijana wetu ambao wanafanya kazi vibaya, tuletee tu tutawshughulikia. Hata hivyo vijana hawa wamefanya kazi nzuri sana. Leo tunajivunia kama taifa kupambana na uvuvi haramu, tunajivunia kama taifa kupamba na uvuvi haramu. Sasa wamefanya kazi nzuri hivyo hasa sisi vingozi wenyewe tuliozitunga sheria wenyewe, tumepewa mpaka na mamlaka kwa sababu wameguswa tu watu wako, kwa sababu limeguswa tu jimbo lako maafisa hawa wote wanakuwa ni wabaya. Twendeni case by case.

Mheshimiwa Spika, nalizungumzia hili suala la oparesheni, hizi operesheni zote, Oparesheni Sangara pamoja, Oparesheni MATT na Operesheni Jodari zimeleta mageuzi makubwa, lazima tujivunie. Uzalishaji wetu wa samaki umeongezeka, uzalishaji wetu wa mazao mbalimbali umeongezeka kwa kiwango kikubwa sana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mambo tuliyoyafanya baada ya oparesheni hizi; mauzo yetu ya nje ya samaki yameongezeka sana. Uzalishaji wetu wa ndani wa samaki umeongeza sana. Nilikuwa nasikiliza kwenye *tv* mama mmoja anahojiwa anasema mimi jambo ambalo namkumbuka Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na kumpongeza ni moja; tulikuwa tunanunua samaki sato kwa shilingi 14,000 leo tunanunua kwa shilingi 7,000/ Tulikuwa tunanunua samaki sangara kwa kilo shilingi 9,000 leo tunanunua kwa shilingi 6,000. Samaki wapo kila sehemu wameongezeka. Ilitokea Watanzania walianza kula vifaranga; hatusahau jinsi rasilimali hii ya uvuvi ilivyovurugwa na uvuvi haramu, hatuja sahau.

Mheshimiwa Spika, Watanzania leo wanakula samaki wazuri, bora na wenye viwango, tena kwa bie ndogo, na wanapatikana kila sehemu na mauzo yetu ya nje yanazidi kuongezeka. Mlikuwa mnazungumzia mauzo kwamba mauzo yetu yanapungua; hivi unawezaje kuongeza mauzo ya samaki ilhali samaki wazazi waliobaki; kwa sababu uzalishaji wetu wa samaki takriban asilimia 90 wote ni Ziwa Victoria. Sasa samaki wazazi umabakiza 0.4, samaki wa kuvua umebakiza asilimia 3.3; utawezaje wewe kuleta mauzo makubwa nje ya nchi? Haiwezekani! Hata hivyo vilevile watu walitorosha, watu wanavua samaki wetu hapa, watu wanakuja hapa kutoka nchi mbalimbali wanapakia samaki wetu wanaondoka nao. Warwanda walikuja hapa wakapakia samaki wetu wakaondoka nao, Wakenya walikuja wakachukua samaki wetu, Warwanda walikuja hapa wakachukua samaki wetu, Waganda hivyo hivyo na nchi nyingine bila kulipa chochote; lakini leo tumewabana wanalipa; hatukatazi kuchukua rasilimali lakini tunawabana wanalipa, tatizo liko wapo?

Mheshimiwa Spika, nilitegemea Waheshimiwa Wabunge kwa makofi makubwa mngewapongeza sana vijana wangu kwa jinsi wanavyochapa kazi nzuri ya ujenzi wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Mabomu; hatujasahau watu walivyokufa Ukanda wa Pwani kwa kulipuliwa na mabomu, hatujasahau, watu wamepoteza maisha sana, Serikali ya Awamu ya Tano ikasema hapana tutakomesha mabomu. Watu wanavua kwa sumu, watu wanavua kwa mabomu, tuwachekelee tu, tuseme sawa tu vueni, ninyi ni wapiga kura wetu haturuhusiwi kuwakataza, hapana, hatuwezi kuwa nchi ya namna hiyo, haya lazima tuyakatae. Mwaka 2016 nchi hii mpaka wageni walianza kuikimbia wakikaa kwenye mahoteli mabomu yanalipuka, watu maskini wanaenda kuvua kwa ratiba zao kwa utaratibu wao wanalipukiwa na mabomu wanakufa.

Mheshimiwa Spika, leo mpaka tunavyozungumza uvuvi umeendelea kushuka 2017, 2018 na leo 2019, uvuvi wa

kutumia mabomu wameenda ku-*test* sifuri, hakuna mtu anafanya uvuvi wa mabomu, lakini Waheshimiwa Wabunge, leo kwa nini hatutaki kujivunia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, meli za uvuvi kutoka nje zilikuja hapa kuvua, zimekuja hapa kuvua meli za kigeni kutoka nje ya nchi, zikavua samaki na wakaondoka. Wamefanya uvuvi haramu uliopitiliza kwenye maji yetu, tumekamata meli ya *Buhanaga One,* tumekamata meli, tumesimamia kesi ile, walizoea mpaka na kesi wanafanya *maneuver* inakuwaje sijui, sijui inakuwa vipi, tumeshinda kesi Mahakamani, kwa nini isiwe suala la kujivunia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, meli za Kigeni zimekuja hapa nchini, Meli ya *Buhanaga One,* ambayo tuliipiga faini ya shilingi milioni sabini na saba, kama *to compound now*, milioni sabini na saba, wakasema tumewaonea. Wameenda Mahakamani wamepigwa faini ya bilioni moja au kifungo cha miaka ishirini, hivi sasa tunavyozungumza, Meli tuliyoikamata ya *Buhanaga One,* ipo Tanzania, samaki waliyokuwemo mle tani thelathini na mbili, wako ndani ya meli wanashikiliwa, wako Tanzania na yale mapezi ya papa na yenyewe yapo na Mmiliki wa meli amefungwa, Wakala amefungwa na Nahodha amefungwa miaka ishirini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanatakiwa *either* walipe bilioni moja au wafungwe miaka ishirini, kulipa bilioni moja au kufungwa miaka ishirini, kwa nini isiwe suala la kujivunia hili? Jambo kubwa namna hii, kwa nini Taifa mnalisoma kwenye kitabu hiki Waheshimiwa Wabunge mnaliona la kawaida, ni rekodi ambayo haijawahi kufanyika toka nchi hii ipate uhuru na hata Mungu aumbe dunia na akaiumba Tanzania, haijawahi kuitokea. Kwa nini mnalisoma na hamsemi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania sasa hivi imeheshimika Kimataifa kwamba tunasimamia rasilimali zetu na tunapongezwa. Juzi hapa nchi mbalimbali zilikuwa zinachukua vijana kwenda kusoma mafunzo nje ya nchi, tulikuwa tunachukua vijana wanne, watatu, wawili, sasa hivi

nimepeleka zaidi ya kumi na wanaombwa wengine watafika zaidi ya ishirini kwa sababu ya hatua Tanzania inazozichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukija hata kwenye hili suala la 0.4, Waheshimiwa Wabunge walitendee haki Bunge. 0.4 kwa samaki wanaovuliwa Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu, kulipia mrabaha wa dola 0.4, hili jambo halijaanzwa na Serikali, hili jambo limeanzia kwa Wabunge wenyewe na tukaweka maazimio humu ndani ya Bunge. Tukasema kwamba ni lazima Taifa linufaike, watu walikuja na meli zenye ukubwa wa mpaka tani 300. Wanalipa leseni ya dola 65,000 peke yake ni kama shilingi milioni 150 tu, anaingia na meli yenye uwezo wa kuchakata mpaka wa kubeba mzigo wa tani 300 za *tuna*.

Mheshimiwa Spika, mbona hawajajiuliza *tuna* akivuliwa hapa anauzwa kwa bei gani, kabla hawajaishauri Serikali kuondoa 0.4 mbona hawajajiuliza hilo swali,? Leo mbona hawajajiuliza swali, watu wanavua dagaa, dagaa ambao wanauzwa kilo moja Sh.10,000 au Sh.15,000, tunatoza ushuru wa 0.3 na wanalipa, leo kwa nini lizungumziwe Kampuni la Kigeni linalokuja kuvua hapa matani kwa matani ya rasilimali za Watanzania na kwenda nazo, halafu tuachwe watupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Bunge ndiyo liliiambia Serikali kwamba tumechoka kudhulumiwa, tumechoka kuonewa na hizi meli za uvuvi zinazotoka nje ya nchi. Serikali ya Awamu ya Tano ilipokuja ikatekeleza mara moja, ikaweka kile Kifungu kile cha 0.4 kwa mabadiliko ya Kanuni za mwaka ule wa 2009 zikabadilishwa mwaka 2016, tukaweka tozo ya 0.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge hapa ni mashahidi, Waziri aliyekuwepo, Mheshimiwa Tizeba, alitoa *holiday* ya miezi sita ya kutokulipa hii 0.4. Alipotoa ile *holiday* ya 0.4, Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Spika ikabaini kuna dosari na Tanzania imepoteza bilioni tano kwa *holiday* ile na Serikali tukalaumiwa kwa nini tumetoa *holiday,* tukapoteza

rasilimali hizo. Sasa Bunge linalalamika, kwa kutoa *holiday* tu ya miezi sita, Bunge hili hili na Wajumbe hao hao na wengine walichangia jana, ambao wameilalamikia Serikali kwa *holiday* ya miezi sita, leo wanageukaje ghafla kwamba 0.4 ni makosa, Serikali ilifanya njama za kuhujumu uvuvi wa Bahari Kuu. Waitendee haki Serikali yao. Hii Serikali ni ya kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakiwa mnazungumza Mheshimiwa Waziri mwenzangu Tizeba ndiye aliyeiweka na hakuiondoa, Mheshimiwa aliiweka tozo ya shilingi 0.4 na jana ananilaumu mimi tena kwamba sijaiondoa hii 0.4.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, *facts are facts,* naomba mtulie msikilize majibu, Watanzania hatupendagi *facts,* sijui tukoje. Ninyi msikilizeni Waziri aseme, angekuwa anasemwa mtu ambaye yuko nje ya Bunge hilo ni sawa kwa sababu hana nafasi ya kurekebisha. Kama Selasini umefanya jambo nakwambia Selasini umefanya hivi, usiseme usinitaje, hapana, wewe si uko hapa, *(Makofi)*

Endelea Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mbona hata mimi nimetajwa tu vizuri tu, mpaka wengine wakaenda mbali wakasema Waziri hasalimii watu, mbona nimetajwa tu, mbona hakuna Mbunge aliyekataa.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Ongea bwana.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema, Waziri aliyekuwepo aliweka hii Kanuni na yeye jana amegeuka kuwa mlalamikaji ya kwamba mimi nime-*frustrate* uwekezaji kwa kuweka 0.4. Kwa hiyo ninachotaka kusema Waheshimiwa Wabunge waitendee haki Serikali yao, 0.4 wameiweka wenyewe kwa nia njema ili kuweza kulifanya Taifa letu linufaike, ndiyo maana akaunda na Kamati ya kutushauri juu ya jambo hili tufanyaje ili uvuvi wa Bahari Kuu tuweze kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wanapozungumza kuhusu kutoza shilingi 0.4 Waheshimiwa Wabunge lazima tutafakari vizuri, 0.4 tunaiondoa, lakini mbadala wake ni nini, Taifa litanufaika na nini, twende kwa utaratibu gani, kama kuna *issue* yoyote ile ya kuhusu 0.4 kwa wavuvi wetu ndiyo wameshindwa kuja kuvua kwenye maji yetu, tutaitafutia majawabu, lakini nataka niwakumbushe, tulipoanza kufanya *Operation MAT,* Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu, meli ishirini na nne zote zilizokuwa zinavua, ndani ya *EZ* yetu tulizikamata kwa kujihusisha na uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lazima watu wajue, Tanzania, siyo Tanzania ile ya zamani, hatuwezi kuendelea kukubali kuruhusu watu wanakuja, eti kwa sababu tu lazima waje kwenye maji yetu kuvua, watufanyie wafanye uvuvi haramu, wahujumu raslimali zetu, halafu sisi tuendelee kuwaacha, tutaendelea kuwadhibiti. Hata hivyo, niseme, wako watu sasa hivi wanashindwa kuja kuvua, kwa sababu yawezekana bado wana hiyo kesi ya kutoroka kutokana na jinsi tulivyowatuhumu juu ya uvuvi wa Bahari Kuu, walivyotoroka kwa sababu ya uvuvi haramu au kwa sababu zingine. Sasa hili, hatuwezi kuliamua hapa, watupe muda Serikali, tufanye uchambuzi wa kina, tulinganishe wapi na wapi kwa sababu hiyo 0.4 iliwekwa kwa mazungumzo mapana ya Serikali ili nchi yetu kuiwezesha iweze kukusanya mapato makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niongelee suala la mapato na lenyewe limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengine wakaenda mbali sana, wakasema hii Wizara yenyewe inajivunia leo mapato haya, kwa sababu ya faini, Waheshimiwa Wabunge watendeeni haki basi hawa vijana wanaofanya hizi kazi. Hizi fedha wanazokusanya hawaweki mifukoni mwao, hizi fedha zote zinazokusanywa zinaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na sisi hao hao, ndiyo ambao tunaoiomba maji Serikali tunaomba Zahanati, barabara, umeme na huduma mbalimbali za Serikali. Fedha hizi, hakuna Afisa hata mmoja ambaye anachukua yeye anaweka mfukoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wamesema, suala la faini, Wizara kwa mfano, katika Sekta ya Mifugo katika *para* ya 23, mapato ya mwaka 2018/2019 ni bilioni 33.9, lakini mapato hayo faini kati ya fedha hizo ni bilioni tatu, ambayo ni sawa na asilimia tisa. Kwa hiyo siyo kweli kwamba mapato haya ni ya faini tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika upande wa Sekta ya Uvuvi, *para* ya 124 katika mapato ya mwaka 2018/ 2019 ni bilioni 30.3 na hii ni kuishia tarehe 15 Mei, mwaka haujaisha. Faini ni bilioni 6.5 ambayo ni sawa na asilimia 21.3.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba, jitihada hizi zilizofanywa na Wizara ni suala la kudhibiti, tumefanya usimamizi vizuri, wa kuhakikisha kwamba kila eneo linalotakiwa kutoza, linatozwa, wale watu waliokuwa wanatorosha mapato, waliokuwa wanatorosha mifugo yetu tumewadhibiti, waliokuwa wanatorosha rasilimali za uvuvi watu kama nilivyosema, walipakia samaki zetu hapa wakaenda bila kulipa chochote, tumehakikisha wanalipa. Wale watu waliokuwa wanakwepa kodi, tumewasimamia wanalipa kodi, lakini vilevile hata wahalifu lazima waendelee kulipa faini na hizi faini zitaendelea hadi pale wahalifu watakapoisha. Kwa sababu hakuna namna nyingine, sheria zimesema ukifanya hivi utapigwa faini hii.

Mheshimiwa Spika, pia kutoza faini sio dhambi kama kuna mhalifu, kwa hiyo wahalifu wakimalizika na faini hazitakuwepo zitaendelea kushuka kadri watu watakavyokuwa wana-*comply.*

Sasa Waheshimiwa Wabunge, leo nikizungumza *trend* ya mapato ya uvuvi, mwaka 2009/2010 yalikuwa bilioni 6.6 tu, mwaka 2010/2011 ilikuwa bilioni 8.2, mwaka 2011/2012 ilikuwa bilioni 8.9, mwaka 2012/2013 ilikuwa bilioni 8.3; mwaka 2013/2014 ilikuwa bilioni 10.8; mwaka 2014/2015 ilikuwa bilioni 15.5; mwaka 2015/2016 bilioni 17.87; mwaka 2016/2017 ilikuwa bilioni 18.58; mwaka 2017/2018 ilikuwa bilioni 26.9; na mwaka huu kuishia Mei tarehe 15 ilikuwa bilioni 30.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye mifugo mwaka 2009/2010 ilikuwa bilioni 2.7; mwaka 2011/2012 ilikuwa bilioni 8.7; mwaka 2012/2013 ilikuwa bilioni 5.6; mwaka 2013/2014 ilikuwa bilioni 6.8; mwaka 2014/2015 ilikuwa bilioni 6.4; mwaka 2015/2016 ilikuwa bilioni 14.1; mwaka 2016/2017 ilikuwa bilioni 12.5; mwaka 2017/2018 ilikuwa 21.7; na leo tarehe ya leo 23 Mei, 2019 ni bilioni 33.85 na ni kuishia tarehe 15 Mei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukija na mtiririko huo, ukija na mtiririko huo mwaka wa 2000 kwa jumla yake, mwaka 2017/2018 ilikuwa bilioni 17.3 na leo 2018/2019 tuna makusanyo mpaka sasa hivi ya bilioni 64.15 na tutafika bilioni 70 ifikapo tarehe 30 Juni, kwa malengo tuliyopewa ya bilioni 40. Makusanyo zaidi ya bilioni 30 na haya makusanyo ya bilioni 30 ambayo yamekusanywa na Wizara hii, yote yako kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, yanaendelea kutekeleza Mipango mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa mmempongeza Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, amejenga Zahanati ndiyo hizo fedha, mmempongeza Waziri wa Maji, ndiyo hizo fedha. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Rudia,

**MBUNGE FULANI:** Rudia tu.

**MBUNGE FULANI:** Arudie.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, sisi tunatafuta hizi hela, lakini wanawapongeza, wamempongeza sana Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa amepata pongeza nyingi sana, amejenga zahanati nchi nzima, ni fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamepongeza miradi ya maji imejengwa, tunaishukuru Serikali na wakawa wanaomba hata tozo ziongezeka, sisi tumetoa mchango wa ziada siyo ile tuliyopewa na Serikali, wa ziada ya bilioni 30. Nataka niwaulize bilioni 30 kama hawa watumishi wangu na mimi

Waziri ni mla rushwa, kama sisi ni wala rushwa hizi fedha tungezifikishaje Hazina,? Wapongezeni Vijana hawa, kwa sababu kama wangekula rushwa hizi fedha zisingepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nawaomba, tuwe wakweli tukiwa hapa, hata Ilani ya Uchaguzi ya CCM inatueleza kutekeleza Ilani hii, hata hiyo ya CHADEMA au ya Chama kingine, sijaona Ilani ambayo itatekelezwa bila pesa, hakuna Ilani ya Chama chochote duniani ambayo inaweza kutekelezwa bila fedha. Kwa hiyo kama kuna njia zozote za kupinga ukusanyaji wa mapato ni kuzipinga hata Ilani za vyama vyenu, kwa sababu hakuna Ilani duniani ambayo unaweza kuitekeleza bila kukusanya kodi, lakini tutaendelea kukusanya kodi hizo na hatutawaonea wananchi kama inavyozungumzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yamezungumzwa mambo mengi, migogoro ya wafugaji; utatuzi wa migogoro, Wizara yetu imefanya mambo makubwa katika historia ya utatuzi wa migogoro na hata dada yangu yule aliyeanza kusema, Mheshimiwa Gimbi, aliyesema kwamba Mpina ameonea wafugaji, Mpina amewasaliti Wasukuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza moja, nikubali kabisa kwamba mimi siyo Waziri wa Wasukuma, mimi ni Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. La pili, hatutawa-*favor* watu kwa ukabila wao, wakivunja sheria watashughulikiwa. Niliwahi kusema hapa, kwenye uvuvi haramu hata Mzee Mpina mwenyewe tukimkuta ameshiriki uvuvi haramu tutamkamata. Leo nazungumza Mzee Mpina yuko pale, kama atashiriki uvuvi haramu, tutamkamata, kwa sababu hakuna, hatuwezi kutengeneza mazingira ya ukabila ukienda huku unafanya hivi, lakini nataka nimhakikishie hakuna kipindi kingine ambacho migogoro ya wafugaji imetatuliwa kama kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Timu zimeenda maeneo mbalimbali, Wabunge wengine wamezungumza vizuri, kuna watu wengine walikamatwa, ng'ombe 540, Naibu Waziri

wangu akaenda tukawaomba watu wa Maliasili na Utalii, ni kweli ng'ombe walikuwa ndani ya hifadhi, tukawaomba wawasamehe, wakasamehewa, ng'ombe 500 wakatoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu nikamtuma siku ya Pasaka, kwenda Simiyu ambako ng'ombe zilikuwa zimekamatwa zaidi ya 200, siku ya Pasaka, akaenda kuomba na kwenyewe tukawaomba wenzetu wa Maliasili na Utalii watusaidie kutokana na mazingira yaliyokuwepo, mifugo ile ikatoka. Vilevile tumehangaika nchi nzima, kutafuta malisho ya wafugaji ambako leo, Wizara yetu imetenga hekta 373,000 za kuwapangisha wafugaji katika hatua hii wakati tunawatafutia maeneo mbalimbali kwa ajili ya malisho. Maeneo ya Serikali. haijawahi kutolewa offer hiyo katika kipindi kingine chochote kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo, Halmashauri tumezifuata moja baada ya nyingine kwenye migogoro mikubwa ya mifugo, tumepata mpaka sasa hivi hekta 199,000 ambazo na zenyewe tutaweka mifugo. Mambo haya hayajawahi kufanyika migogoro ya wafugaji kupigana mapanga na kufanya nini, leo imepungua, ilikuwa dhahama kubwa nchi hii, mbona haipongezwi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, migogoro ya mifugo tuliyoibua mikoa hiyo michache (mitano) tuliyokwenda ni migogoro 43. Katika migogoro hiyo 43 tuka-*solve* migogoro 27, sawa n a asilimia 63 ya migogoro. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye na mimi naungana sana na Watanzania wengine wote wanaoendelea kumpongeza aliamua kuunda timu ya Mawaziri wanane kwenda kushughulika na migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Tumetembea nchi nzima na tumetoa mapendekezo mengi juu ya kutatua migogoro hii. Ninaamini baada ya hatua hizi kufikiwa tatizo la migogoro la wananchi kukosa malisho litakuwa limepungua.

Mheshimiwa Spika, nawakumbuka wapiga kura wa Kongwa. Tayari tumetenga hekta 13,500 kwa ajili ya

wananchi katika *Ranch* ya Kongwa ili kuweza kuwanufaisha wananchi wa kongwa ambao wamekaa na *Ranch* hii kubwa sana na kwa muda mrefu lakini hawana mahali pa kuchungia. Kwa hiyo tumekwenda maeneo mbalimbali kutatua changamoto hizi. Mmeona hata juzi hapa Mawaziri tunazunguka nchi nzima kutatua migogoro tukiwa pamoja kama timu moja ya Serikali, kutatua migogoro ya wafugaji. Kwa hiyo mambo haya Waheshimiwa Wabunge Serikali hii tuko kazini na tunaendelea kuyapigania kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, suala la magonjwa ya wanyama. Tumefanya kazi kubwa sana kwenye suala la magonjwa ya mifugo ambapo kwa mara ya kwanza Serikali imeweza kuogesha ng'ombe nchi nzima baada ya kutoa dawa 8,823, tumeogesha nchi nzima. Katika bajeti hii mnayoipitisha tumetenga zaidi ya milioni 500 ambazo tutaogesha tena mwaka unaofuata; kwa hiyo tumejipanga vizuri. Kituo chetu kile cha *TVI* kinaendelea kuongeza uzalishaji wa chanjo. Tulikuwa tunazalisha chanjo nne tu hapa nchini, sasahivi tumeendelea kuzalisha chanjo, hata hii ya homa ya mapafu ya ng'ombe tayari tumeshaanza na tunaendelea, na tunategemea kwamba baada ya muda mfupi tutafikia chanjo zote 11 ambazo leo tunatumia mabilioni ya fedha za Watanzania kuagiza chanjo kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, naomba muendelee kutuunga mkono. Mama mmoja akanipigia simu akaniambia Mpina Waziri wa Mifugo hivi Nyerere amefufuka? Nikamuuliza kwanini mama? Mama mtu mzima mwenye umri wa karibia miaka 100 na kitu; Nyerere amefufuka? Nikamuuliza kwanini? Yaani Serikali imeanza kuogesha mifugo! Tunaona kila sehemu Serikali inaogesha mifugo! Nikamwambia mama Nyerere hajafufuka ila kuna kijana wake anait wa Magufuli, kijana wa Nyerere ndiye anayeyafanya haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, operesheni Nzagamba. Operesheni Nzagamba imefanyika kwa nia njema sana. Waheshimiwa Wabunge tukumbuke, lazima tujiulize hili swali;

kwanini viwanda vyetu vimekufa? Watanzania wengi wamejiuliza swali hili lakini ukweli ni kwamba viwanda hivi havikupata ulinzi wa kutosha ndiyo maana vilikufa. Tumeendesha operesheni hapa na matokeo ya operesheni Waheshimiwa Wabunge mmeyaona. Tumeendesha Operesheni Nzagamba, tumekamata watu mbalimbali kwenye maeneo mbalimbali wakijaribu kufanya utoroshaji mkubwa wa rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, hakuna mtu atakayekwenda kuwekeza kwenye nchi ambayo hailindi wawekezaji wa ndani. Yaani leo hii unamwambia mtu ajenge kiwanda, kesho watu wanaingiza maziwa hapa nchini, hayana vibali, hayajalipa chochote hayajapimwa hata ubora yanaingia hapa nchini yanauzwa kwa bei ya chini kiasi kwamba huyu hawezi kushindana. Unamwambia mtu ajenge kiwanda cha nyama wakati hoteli zote zinakula nyama kutoka nje, Watanzania wote wanakula nyama kutoka nje na zinauzwa kwa bei ndogo kumbe zingine zimeingizwa hapa zingine zikiwa zime-*expire,* Watanzania wamekula. Usipowalinda namna hiyo watakula chakula ambacho hakina ubora na hakina viwango. Tufanye nini?

Ukiwakamata tayari una-*frustrate* wawekezaji. Nani anaye-*frustrate* wawekezaji? Viwanda vyote nchi hii ilishindikana kuendelea. Wawekezaji wakawa wanapiga danadana wanakimbia. Leo tumeleta hapa mpango, viwanda vipya vinajengwa, uwekezaji wa takriban bilioni 200 kwa muda mfupi wa hatua ambazo Serikali sisi tumezichukua katika kupambana na watu waliokuwa wanaharibu soko la Watanzania ili kuwepo na ushindani ulio sawa.

Mheshimiwa Spika, huwezi kuupata ushindani ulio sawa kama haya mambo utayaendeleza. Leo tunajenga kiwanda cha chanjo chenye uwezo wa ku-*supply* chanjo 27, Tanzania, haitaagiza chanjo tena. Mnataka Serikali hii ifanye nini? Viwanda vikubwa vya nyama vinavyojengwa havijawahi kuwepo. Watu wengine walisema wingi wa viwanda si tija, tija ni ufanisi. Sasa hata hivyo viwanda vingi vya aina hiyo hatukuwa navyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima wawekezaji wetu wa ndani tuwalinde na ndiyo maana operesheni hizi zimekuwa zikifanyika. Wafugaji wetu hakuna namna yoyote ile ambayo tunaweza tukawaona kwa namna yoyote ile. Tozo tunazoziweka ni tozo ambazo zinalifanya walau Taifa nalo linufaike. Huwezi ukawa na mifugo nchi hii halafu hupati chochote. Mifugo hii, Tanzania kuwa ya pili Afrika kuwa na mifugo; na ninataka nisahihishe hizo takwimu, watu wamesema kwamba Tanzania ni nchi ya tatu, hapana Tanzania ni nchi ya pili baada ya Ethiopia kuwa na mifugo mingi. Sisi tunashikilia asilimia 1.4 ya mifugo yote iiyoko duniani; tunashikilia asilimia 11 ya mifugo yote iliyoko Bara la Afrika, halafu unakusanya mapato ya bilioni 12, hatuwezi kuruhusu hilo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, mtuamini, nia ni njema ya kujenga uchumi wa nchi yetu. Tuzalishe mifugo yetu, tupate malighafi ya viwanda, tuzalishe nyama, tuuze nje ya nchi, tuuze maziwa nje ya nchi, tutosheleze soko la ndani. Hivyo hivyo na kwenye samaki. Leo samaki tulikuwa tunaagiza kwa mabilioni ya fedha, uagizaji wa samaki sasahivi umeshuka kwa asilimia 67 tangu tuanze kuchukua hatua hii na mambo yanaenda vizuri. Leo kiwanda chetu cha Chobo kila wiki kinabeba tani 45 kutoka mwanza kuja Dar es Salaam kwa kutumia ndege zetu wenyewe za *ATCL.* Leo mageuzi haya yanafanyika, sasa tutapata kiwanda cha kuchinja ng'ombe 1,000 cha Chobo kule Mwanza. Tuna minofu ya samaki inayotakiwa kusafiri kila leo. Uvunaji wetu wa samaki sasahivi uko tani 180 mpaka 200 kwa siku; kwa hiyo tuna mzigo mkubwa wa kusafirisha kwenda nje ya nchi. Viwanda hivi vyote vya nyama tunavyovijenga vitatuwezesha kuzisafirisha nyama kwenda nje ya nchi, tutapata fedha za kigeni. Tumetengeneza ajira nyingi za Watanzania, tumetengeneza soko la Watanzania, tumetengeneza bei ya Watanzania katika rasilimali za mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo niwaombe endeleeni kuunga mkono jitihada za Serikali ambazo zina nia njema kabisa ya dhati katika kuhakikisha kwamba mageuzi ya kweli yanapatikana na taifa

linanufaika na rasilimali zake na kuhakikisha kwamba mtu yeyote yule hatachezea soko la nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tumetengeneza dawati la sekta Binafsi, dawati hili limeleta mageuzi makubwa sana hapa nchini. Sekta ya mifugo na uvuvi ilikuwa hata haikopesheki. Mpaka leo hii tunavyozungumza kupitia dawati hili tayari mikopo ya bilioni 17 imetolewa kwa wawekezaji wa sekta ya uvuvi na kwa wawekezaji wa sekta ya mifugo. Hivi tunavyozungumza mikopo ambayo inategemewa kutolewa hivi sasahivi kupitia dawati hili ni bilioni 55 ambayo nayo itatolewa muda wowote kupitia hili dawati ambalo limekuwa kiungo kikubwa sana kati ya Wizara na Serikali na kati ya wadau na wawekezaji wote na wafugaji wote, na wavuvi wote nchini. Leo tunavyozungumza mambo yanaendelea, wanaenda mbali zaidi hata kusaidia mpaka kuandika *business plans* ili kuwezesha tu mambo haya yaweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, wengine mmezungumzia kuhusu Kiwanda cha Azam. Nataka nizungumzie Kiwanda cha Azam, kiwanda cha Azam kiko Zanzibar, ni cha maziwa, ambapo wana-*import* maziwa ya unga kutoka nje na baadaye wanayachakata wanazalisha maziwa hapa nchini. Kiwanda hiki cha Azam cha Zanzibar baada ya Kanuni mpya ambazo ziliwataka kila wanapo-*supply* maziwa kutoka Zanzibar kuingia nchini wanatakiwa walipe shilingi 2,000 kiwanda kilifungwa, wakashindwa kufanya hivyo. Kilipofungwa kiwanda, kukawa hakuna tena ajira zilizopo pale za Watanzania, zikawa zimesimama hakuna kitu kinaendelea. Tukaamua kwa dhati kabisa kwamba tuwape unafuu.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba hatukuwapa punguzo lolote ila tuliwapa unafuu wa tozo. Kwa maana ya kwamba maziwa ya unga yanapoingizwa hapa nchini tunatoza 2,000, yanapoingizwa ya maji tunatoza 2,000. Sasa huyu anayeingiza ya unga akichakata anapata lita 8, anapoingiza Tanzania Bara anatakiwa alipe shilingi 16,000 kwa lita moja aliyoichakata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tulichoona kwamba hapa Zanzibar wameajiriwa Watanzania wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na hoja ilitoka kwa Wabunge hawahawa humu humu ndani, mkituomba kwamba hiki kianda tukiwezeshe kifanye kazi. Tulichokifanya sisi tunamtoza yule kwa *equivalent.* Tunamtoza kwa uwiano; kwa maana ya kwamba tunamtoza kwa *equivalent* ya kilo ya unga ambayo ni shilingi 2,000. Kwa hiyo unachukua shilingi 2,000 ukigawa kwa nane unakuta shilingi 250. Ndicho tulichokifanya ili kiwanda kile kiweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, lingine tulilofanya, sheria inasema maziwa yakitoka Zanzibar yakiingia huku yametoka nje ya nchi yanatakiwa kulipa *import levy* na maziwa yakitoka hapa *low milk* inayozalishwa hapa ikitaka kupelekwa Zanzibar kwa ajili ya kuchakatwa na yenyewe inatakiwa ilipe *export levy.* Tukasema sasa hii kwa sababu maziwa haya yamezalishwa na Watanzania, maziwa ya Watanzania hapa bara hayana soko, maziwa ya Watanzania yanayozalishwa Zanzibar hayana soko, tukasema hii tuiondoe kabisa, wakitaka kuingiza maziwa yaliyochakatwa kutoka Zanzibar ya Wanzanzibari wenyewe waliyoyazalisha, yakiingizwa hapa Bara wasilipe chochote.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile maziwa yatakayochukuliwa hapa kwenda kiwanda cha Azam yaliyozalishwa na Watanzania hapa yakienda kule wasilipe chochote, ndiyo *concept* ya Serikali. Hakuna *favour* yoyote tuliyompa, na ndiyo maana tunaendelea kumtoza kwa sababu tu ya yale maziwa anayoyaagia kutoka nje ya nchi. Baada ya hapo, akiacha kuagiza kabisa ya nje ya nchi atatozwa asilimia sifuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya niliyoyazungumza ninataka sasa nimalizie na baadhi ya hoja chache ambazo Waheshimiwa Wabunge wengine mbalimbali waliweza kuziuliza hapa. Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu baadhi ya hoja mbalimbali hapa ile asubuhi alipopata fursa ya kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge; na akajaribu kutoa *clarification* nyingi sana juu

ya hoja mbalimbali zilizotolewa za baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, akiwemo Mheshimiwa Zitto Kabwe.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, mlizungumzia sana suala hili kwamba Serikali ya Awamu ya Tano hakuna jambo lolote ambalo imelifanya; Ilani yote haijatekelezwa; kama Mheshimiwa Naibu Waziri ambavyo aliweza kuzungumza ile asubuhi. Lakini hoja hii ameizungumza kwa nguvu sana Mheshimiwa Zitto Kabwe, akasema na Wizara inajivunia tu faini n.k. hakuna kinachofanyika, Serikali ya Awamu ya Tano hakuna jambo lolote iliyofanya katika Ilani ya Uchaguzi. Nilikuwa nataka Mheshimiwa Zitto Kabwe angekuwepo hapa; kwa sababu kwa muda mrefu sana amekuwa hata akitoa takwimu za uongo juu ya ukweli na uhalisia wa utekelezaji wa shughuliza Serikali ya Awamu ya Tano, lakini wakati mwingine na kuonekana chuki dhahiri juu ya Serikali hii ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, anawadanganya watu kwamba mapato yalipanda mwaka ule wa 2014 na leo yameshuka, yamekuwaje, Serikali hii hakuna hatua yoyote nyingine ambayo imeichukua juu ya mambo haya.

Mheshimiwa Spika, sisi tunakwenda vizuri. Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi juu ya ujenzi wa bandari tumejipanga vizuri. Sasa hivi upembuzi yakinifu unafanyika na mkandarasi wetu yuko kazini anafanya kazi hiyo na Serikali imeshatenga na imeshaanza kumlipa na hivi karibuni atatoa ripoti ambayo itatuonesha tukajenge wapi bandari. Tayari mazungumzo tumeshayafanya na Serikali ya Korea na tuko vizuri katika kutafuta fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, *TAFICO* imeanzishwa na tayari tumepata billion 4.2 kutoka Japan kwa ajili ya kuboresha baadhi ya miundombinu iliyoko pale. TAFICO *Business plan* imeshaandaliwa kwa kulitekeleza jambo hili. Sasa unaposimama hata kama una chuki namna gani, hata kama una chuki namna gani na Serikali hii ya Awamu ya Tano ni bora hata ukawa mvumilivu tu; kwa sababu hakuna namna

yoyote ambayo Serikali ya Awamu ya Tano inaweza ikashindwa kutekeleza majukumu yake eti kwa sababu ya watu wawili watatu ambao wana chuki nayo.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuhakikisha kwamba Serikali ya Awamu ya Tano inatekeleza majukumu yake, Ilani ya Uchaguzi inatekelezwa kwa kiwnago kikubwa. Ni vizuri sana Mheshimiwa Zitto Kabwe asiiharibu ile rekodi tuliyoiweka naye enzi hizo. Tuliweka rekodi nzuri ya michango mizuri hapa Bungeni ambayo imelisaidia taifa hili lakini ameanza na kuku-*attack* mpaka wewe Mheshimiwa Spika ambaye ndiye muasisi wa mageuzi, sio uchonganishi!

Mheshimiwa Spika, ninachosema, siku ya *ESCROW,* Mheshimiwa Spika, akiwa Naibu Spika wa wakati huo ndiye aliyeamua Mpina aingie kwenye Kamati ya *ESCROW,* Kangi Lugola, Hamis Kigwangalla aingie kwenye Kamati ya *ESCROW* na maombi hayo yaliombwa na Filikunjombe pamoja na Zitto Kabwe. leo hii Zitto Kabwe anasimama katika Bunge hili, na maeneo mbalimbali kuzungumza hata maneno ya uongo dhidi ya Mheshimiwa Spika ambaye mimi nasema kati ya watu ambao wametengeneza viongozi humu Bungeni kwa watu ambao hamuijui historia ni Mheshimiwa Job Ndugai Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Na watu waliomtengeneza hata Mpina Mheshimiwa Job Ndugai yumo, sio mtu mwepesi wa kusimama na kumnyooshea kidole, sio mtu mwepesi kihivyo *unless* ni kwa watu ambao wasioijua historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Job Ndugai amefanya mambo makubwa ya nchi hii. Sasa ukiendesha kwa chuki zako, Rais John Pombe Magufuli ni kwa sababu watu tu hawamjui, laiti wangekuwa wanaijua siri ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli hata wale ambao wanaongea haya na yale kule wasingepoteza huo muda. Hakuna mtu atakayemkwamisha Mheshimiwa John Pombe Magufuli kutekeleza majukumu yake, kwa chuki, kwa hila, kwa namna yoyote na wala wanaotegemea kwamba anaweza akayumba wala kuyumbishwa kwa maneno ya hapa na pale wasitegemee hilo.

Mheshimiwa Spika, Rais huyu ni Rais ambaye ameshavuka mipaka mingi ya viongozi, na historia ya Tanzania itaandika, sisemi haya mimi Mpina kwa sababu ni Waziri hapa, niwe mwananchi wa kawaida kabisa kwetu nyumbani Meatu Mwamuge nitasema haya, kwamba Rais Magufuli ni wa mfano na wa kuigwa mfano katika taifa hili. Niwe Mbunge wa kawaida nitayasema haya, niwe Waziri hivi nitayasema haya. Ni mara chache kupata viongozi wako *committed* namna hii, anatakiwa aungwe mkono na Watanzania wote katika mageuzi anayoyafanya ya ukombozi wa nchi yetu. Ni mara chache sana kumpata Rais ambaye akiamua kupasua hapa anapasua, na mnalijua tatizo la kupasua bila kuangalia. *(Makofi/Kigelegele)*

Mheshimiwa Spika, ukipasua bila kuangalia, utapasua mjomba wako, unapasua shangazi yako, utapasua mali za watu ambao hawakamatiki, utapasua mali za watu ambao huwezi kuwagusa nchi hii. Kwa hiyo ni mara chache sana ndiyo maana viongozi wengi wanayumba kwa sababu ya kukosa misimamo hiyo. Mimi nataka kama taifa tumuunge mkono Rais huyu tutafika mbali katika ukombozi wa nchi yetu, tuijenge nchi yetu, tuache hizi siasa nyepesi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, someni! Ooh! Nimejisahau.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana, lakini nimalizie kwa kusema kwamba, safari ya mageuzi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeanza, tena iko hatua nzuri. Nami na wasaidizi wangu kama tulivyoahidi na tunaendelea kuwaahidi Wabunge, tutatumika sisi kwa nguvu zote, watendaji wangu hawa, waoneni hawa, wana mateso makubwa, kuwa mtumishi halafu chini ya Wizara ya Mpina, wana mateso makubwa. Pale Wizarani tumeshakubaliana kwamba muda ni namba tu, kwa hiyo hatujali muda gani, hatujali sasa hivi ni usiku katika kufanya majukumu yetu na tunaendelea kuwahakikishia, sisi tutakuwa vibarua hivyo,

mpaka tutakapomaliza hili jukumu na tumejitoa hivyo mimi na wasaidizi wangu kuhakikisha kwamba mageuzi haya yanapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi na Naibu Waziri wangu hapa, tunafanya hivyo, hakuna *gain* yoyote, hakuna *any personal gain* tunayoipata zadi ya maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kusema kwamba, sasa baada ya kuwa nimemaliza kutoa maelezo yangu hayo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wasitucheleweshe, waipitishe hii bajeti tu mara moja, tusifike hata hiyo saa kumi na mbili ili tuwahi kwenda kutekeleza, kwa sababu, majukumu ya wafugaji na wavuvi yanatusubiri sana na wengine wadau wako hapahapa wanamhitaji Waziri, kwa hiyo, kuendelea kuchelewesha kupitisha bajeti itachelewesha utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Joelson Luhaga Mpina, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana sana kwa ufafanuzi mkubwa na kwa kweli maneno mengi uliyoyasema yalikuwa yanatoka moyoni kabisa. Si wengi wanajua unahangaika kiasi gani. *(Makofi)*

Tunaendelea Katibu!

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 99 – Mifugo**

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management*............Sh. 2,735,467,800

**MWENYEKITI:** Tayari *Chief Whips* wameniletea baadhi ya majina hapa, kwenye masuala ya Sera, kwa mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Tuanze na Mheshimiwa Mattar Ali Salum, CCM, Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, namwomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu ya uhakika na kama hakunipa majibu ya uhakika nitazuia mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mrabaha wa *0.4 US dollar* kwa kilo ya samaki ambayo inavuliwa bahari kuu ni tatizo sana katika nchi yetu kwa sasa. Kwa sasa meli zote za uvuvi kutoka nje haziji kabisa, tukiangalia hesabu yote kwa mwaka huu ni zero kabisa. Kwa hiyo, tatizo hili linasababishwa na huu mrabaha wa 0.4. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumwombe Mheshimiwa Waziri, atupe *commitment*, ni lini hii 0.4 ataiondosha ili meli za nje ziweze kuja katika nchi yetu ziweze kuvua kwa uhakika na Serikali yetu ipate mafanikio makubwa sana. Kwa maana hii hata leo akiondosha Mheshimiwa Waziri, kuna meli zaidi ya 50 zinahitaji kuja kuvua katika nchi yetu lakini kutokana na tozo hii hawawezi kuja kuvua. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri atupe *commitment*, lini atauondoshea hii 0.4 ili hizi meli ziweze kuja kuwekeza katika Bunge letu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mattar, unapendekeza itoke 0.4 iwe ngapi!

**MHE. MATTAR A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa sasa naomba iondoshwe kabisa, kwa sababu

sisi hatuna meli za uvuvi, tukiweza kuleta meli za uvuvi na kushughulikia basi tunaweza tukarudisha kwa sababu hii ni kanuni ambayo tunaweza tukaiondosha na kuiweka tena. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ufafanuzi wa jambo hilo Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, tafadhali.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimetoa ufafanuzi wakati natoa hoja yangu na nimetoa maelezo marefu sana juu ya jambo hili na sitaki kurudi tena kule kwenye maelezo ambayo niliyatoa, ninachotaka kusema hapa Mheshimiwa Mbunge, kwamba, hoja hapa ni dola za Marekani 0.4 kwa ajili ya samaki wanaovuliwa kutoka ukanda wa uchumi wa bahari kuu, yaani *EZ,* wanapovuliwa kulipa huo mrabaha wa 0.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, hii tozo iliwekwa makusudi na kwa ushauri wa Bunge lenyewe, lakini vilevile na kwa ushauri wa Bunge lenyewe na baadaye Serikali ikaridhia kuiweka na shabaha yake ilikuwa ni kuiwezesha nchi yetu iweze kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachotaka kukiomba, kwamba, kuna tatizo hapa limetokea la meli kutokuja, Serikali ipewe nafasi ya kutathmini tatizo la meli kutokuja ni nini! Isiwe suala ni kuondoa 0.4, kwa hiyo, sisi tupewe nafasi ya kufanya tathmni na kuondoa changamoto zilizopo ambazo zinasababisha meli zisije. Sasa kama katika kuondoa chagamoto itakuwa labda kupunguza hiyo 0.4 au kufanya nini, tuachiwe hivyo kama Serikali. Nimwahidi Mheshimiwa Mbunge, sisi tutafanya kwa muda mfupi, kufikia tarehe Mosi, Julai, tutakuwa na majawabu juu ya jambo hili, kama Serikali kwa sababu na sisi ukweli ni kwamba tungetaka tunufaike sana juu ya uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hata tusipofanikiwa kuzipata hizi meli za kutoka nje, tulivyojipanga kitaifa, kwa Shirika letu la *TAFCO*, kwa Shirika letu la *ZAFCO*, tuko vizuri, tutavua wenyewe!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salum.

**MHE. MATTAR A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimesikiliza vizuri majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini yanaonekana bado majibu hayaridhishi, lakini niwaombe Wabunge wenzangu wanisaidie ili tuweze kuijadili kwa vizuri, tupate *commitment* kwa halali ya hii Wizara ili wawekezaji waje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Bahati mbaya umebaki peke yako, hoja yako imeshindwa, tunaendelea na Mheshimiwa Edward Mwalongo. Hamkufika kumi!

**MHE. MATTAR A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imetimia.

**MWENYEKITI:** Edward Mwalongo!

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba ufafanunuzi wa Serikali...

**MWENYEKITI:** Mtu akitoa hoja, mnatakiwa kusimama palepale, siyo tusimame, tusubiri, watu wakonyezane, huwa haiendi hivyo. Mheshimiwa Mwalongo, tuendelee.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba ufafanuzi wa Serikali juu ya suala la chanjo, suala la chanjo limekuwa ni tatizo, wafugaji wengi wanapata tabu sana juu ya chanjo, hazipatikani, lakini hata upatikanaji wake, hakuna uhakika kwamba chanjo hii inaweza ikasaidia kutibu mifugo, watu wanapata chanjo feki, wanapata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano chanjo ya mbwa haipatikani kabisa na ina vyanzo mbalimbali, fikiria kwamba mbwa wanachanjwa na chanjo feki, matokeo yake mbwa wale wanaendelea kuwa na kichaa. Kwa hiyo, naomba sasa ufafanuzi vizuri wa Serikali, ni kwa namna gani wamejipanga

kuhakikisha kwamba chanjo zitapatikana kwa urahisi na wananchi watachanja kutoka kwa dawa zinazopatikana kutoka kwenye vyanzo ambavyo vina uhakika ili kusudi mifugo isipate madhara. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Chanjo, ufafanuzi Mheshimiwa Waziri, tafadhali.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mwalongo kwa swali lake zuri. Nataka nimwambie, moja kabisa, kwamba, kweli tulikuwa na watu walikuwa wanaingiza na mpaka kuuza chanjo ambazo zingine zimepitwa na wakati, zimepitwa na muda wa matumizi na zingine hazina ubora. Hata hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mpaka sasa hivi, kwa ukaguzi na *operations* tulizozifanya, wafugaji wetu wako salama, hakuna mtu tena ambaye anaweza kuwauzia chanjo wala dawa ambazo zimemaliza muda wa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kweli kabisa kwamba kulikuwa kuna shida hiyo ya upatikanaji wa chanjo na kwa sababu chanjo nyingi ni za kuagiza kutoka nje, hatua ya kwanza ya Serikali ni pamoja na kukaribisha lile shirika ambalo litazalisha chanjo karibu zote sasa hivi haa nchini. La pili, ni lile shirika letu kuliwezesha la *TVRA*, kupita Taasisi yake ya *TVI* kuzalisha chanjo kufikia 11 kutoka tano mpaka 11 na tumejipa zoezi hili ndani ya mwaka mmoja tu ili tuweze kuhakikisha kwamba zile chanjo zote za muhimu zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kuwaweka pamoja waagizaji wetu wa ndani na tunaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kwamba changamoto wanazozipata katika uagizaji wa madawa yao zinapungua, lakini mlolongo pia wa taasisi zilizokuwa zinahusika kutoa vibali, ambazo ni *TFDA*, *TBS* na watu wengine na Wizara yenyewe na zenyewe tuko kwenye mazungumzo mazuri kuhakikisha kwamba huu urasimu tunauondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, atupe tu nafasi, sisi tumejipanga kama Wizara, Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa alituagiza Mawaziri watano kushughulikia jambo hili la kuondoa mlolongo wa uombaji wa vibali, kwa sababu wengine walikuwa wanacheleweshwa tu, anaomba kibali anamaliza miezi mitatu hajapewa kibali hicho. Kwa hiyo haya yote yataondoka, watu wataomba kibali watapewa siku hiyohiyo, wataagiza dawa wataleta hapa nchini, watahudumia wafugaji wetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwalongo ameridhika tunaendelea, Mheshimiwa Joyce Sokombi.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi hii nami niweze kuchangia na Mheshimiwa Waziri asiponijibu vizuri nitashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anipe ufafanuzi kuhusiana na wavuvi walioathirika na mabadiliko ya matumizi ya nyavu, kutoka nchi sita kwenda nchi saba. Kubadilika kwa nyavu hizi kumewaathiri sana wavuvi na ukizingatia kwamba ni sera ya Serikali kuhakikisha wananchi wake wanajikwamua kiuchumi, naomba majibu ya kuridhisha, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali hili zuri la Mheshimiwa Sokombi. Naomba tu nimweleze yeye lakini na Waheshimiwa Wabunge wengine na wavuvi wote, pamoja na wale wafanyabiashara wa nyavu. Tumefanya mabadiliko ya kanuni hapa karibuni, ni mabadiliko mapya, haya mabadiliko lengo na nia yetu ni baada ya kilio cha muda mrefu cha wavuvi, ni kile tulichokisema kwamba, sisi katika nchi yetu tulikuwa tunavua samaki mwisho *centimeter* 85, hali iliyopelekea samaki wengi watoroshwe kwenda nchi za nje. Ambapo wenzetu nchi za nje, nchi kama jirani ya Uganda,

ikatengeneza viwanda vinne kwa malighafi inayotoka ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukaa watafiti wetu, kujadiliana, tumekubaliana tunaruhusu *centimeter* 85 kwenda mbele, hata ingelikuwa *centimeter* 1,000, mvuvi avue tu, lakini tukakubaliana pia, kwa msingi huo basi na kwa matakwa ya kisayansi ya uvuvi, tutoe *inches* sita iende nchi saba. Sasa swali lake anataka kujua, kwa muda gani tunaweza tukawapa wavuvi hawa na wafanyabiashara wa nyavu, kwa sababu tayari wanayo *stock* ya nyavu zile za *inches* sita, sisi tumekubaliana ndani ya Wizara, mwaka mmoja, nyavu walizonazo zote waziuze ziieshe, hatutawakamata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pale, ukipita ule mwaka mmoja, sasa tutaanza *effectively* kuhakikisha tunasimamia mabadiliko ya kanuni yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joyce ameridhika.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli sijaridhika, kwa sababu hizi *inches* sita ni muda mchache tu, wananchi wameteseka kuanzia Bunge la mwaka jana nimeongea hapa kwenye Bunge la Bajeti, suala hilihili nimelizungumzia, wale wavuvi walichomewa nyavu, wakasema tumeingia kwenye *inches* sita, *inches* sita muda haujapita sasa hivi *inches* saba, kwa kweli siyo haki, siyo haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunaendelea, Mheshimiwa Mussa Mbarouk.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *no, no, no,* natoa hoja, natoa hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa Mbarouk. Kama ulishaunga mkono hoja huna nafasi, tunaendelea...

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *no, is not fair!*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa Mbarouk nakufuta naendelea na wengine.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi labda, ametoa hoja Mheshimiwa, niunge mkono kwanza hoja yake....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa sasa ukinipangia nakufuta hapa, nimekwambia kama una la kusema ni zamu yako kuendelea.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Labda niseme tu kwamba, kilio cha wavuvi wa Tanzania, kuanzia ukanda wa Pwani kwa maana ya bahari kilomita 1,445 kuanzia Jasini karibu na Mombasa mpaka Mtwara, lakini vilevile pia kwenye maziwa yote, Ziwa Tanganyika, Ziwa Victora na Ziwa Nyasa, kilio cha wavuvi ni kuchomewa na kumamatiwa nyavu zao na kupigwa faini ya shilingi milioni mbili kwa kila mvuvi au kwa kila mvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vilevile, wapo wavuvi ambao wamekamatiwa mashine zao zinatumika kama bondi, pale waliposalimisha nyavu, wakatakiwa kwamba, kama hawana faini ya shilingi milioni mbili, wapeleke mashine. Sasa nataka Waziri anijibu na atoe ufafanuzi, kwanza, watafidiwa vipi nyavu zao baada ya kuwa wameshabadilisha hizi kanuni na sheria, lakini pia, mashine zao watarudishiwa lini, kwa sababu mpaka sasa hivi mashine zimeshikiliwa, hawajarudishiwa na wavuvi wale sasa wamekuwa maskini hali ya kuwa wana familia zinawategemea. Mheshimiwa Waziri asiponipa majibu mazuri nitashika shilingi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbarouk, rudi tena, unataka ufafanuzi kuhusu jambo gani, la sera.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nasema, hoja yangu ni kwamba, kilio cha wavuvi, Tanzania nzima ni kukamatwa kwa nyavu na kupigwa faini za milioni mbili kila mvuvi, lakini pia wengine mashine zao zimeshikiliwa, pale waliposalimisha nyavu za milimita nane, milimita 10, milimita 16, waliambiwa kama hawana faini ya milioni mbili, wapeleke mashine kama bondi. Sasa ninachoomba, nataka Waziri anipe ufafanuzi, kwanza, hizimashine zao watarudhishiwa lini, lakini pia kwa sababu wameshabadilisha sheria na kanuni, je, hawa waliochomewa nyavu, ambao sasa wamerudi kuwa maskini, watafidiwa vipi na Serikali. Kwa hiyo, nataka Waziri anipe majibu mazuri, asiponipa majibu mazuri ya kuridhisha, nitakamata shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali baada ya kuona changamoto ya wananchi wa ukanda wa Pwani, kuvua kwa kutumia milimita 10, dagaa aina ya mchele, kwamba zamani walikuwa na dagaa anayeitwa papa, ambaye yeye ni mkubwa na alistahili kuvuliwa kwa milimita 10, lakini kadri mambo yanavyokwenda, wameibuka dagaa wengi sana ambao ndiyo wavuvi wengi wanavua, dagaa aina ya mchele, huyu mchele havuliwi kwa milimita 10. Sasa baada ya kuongea na wavuvi, tukawasikiliza na tumeenda kwenye maeneo hayo, kuzungumza na wavuvi, wakatuambia kama Serikali na sisi Serikali tukaona ni kweli hoja ya msingi wavuvi wetu hawawezi kuvua na shughuli uvuvi zitasimama na wananchi wengi wanategemea shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukaamua kuibadilisha kanuni, ili kuwezesha sasa wananchi wetu hawa wavue kwa kutumia zile milimita nane, kabla ya hapo, ilikuwa hairuhusiwi kwa mujibu wa sheria kuvua kwa milimita nane, lakini hata hivyo, nilipoenda kwenye ziara maeneo yale, niliwaambia wananchi kwamba milimita nane mlizonazo kwa sababu tumekubali hoja yenu ya kubadilisha sheria kuipeleka

kwenye milimita nane wenye milimita nane, hawatachomewa nyavu zao pamoja na kwamba zimekamatwa zikiwa harama wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikasema sasa zihifadhiwe hizi za milimita nane ili kama tutafika mpaka mwisho tukakubali hii kanuni ipite wananchi hawa warudishiwe. Kwenye kuzichuguza zile nyavu kama alivyosema Mheshimiwa Keissy hapa kwenye kuzichunguza zile nyavu zote zilikuwa na mapambio, mapambio, kwa maana gani, nyavu ni milimita nane lakini ina vipande vingi vya milimita sita, milimita nne, milimita tatu. Sasa ukishakuwa na nyavu ya aina hiyo si tena milimita nane. Kwa hiyo zile nyavu zikachomwa zikatekelezwa kwa mujibu wa Sheria hapakuwa na namna nyingine yoyote. Kwa hiyo Serikali haikufanya kosa lolote, ilichoma nyavu ambazo ni halali na hivyo hawezi kufidia kwa sababu waliofanya hivyo walikuwa wahalifu kwa wakati huo.

**MWEYEKITI:** Mheshimiwa Mussa umeridhika, lakini pia ukumbuke Mheshimiwa Mussa mapendekezo ya kubalika kwa hizi milimita na kadhalika yalitolewa na ninyi Wabunge wa *CUF* kupitia Mheshimiwa Mbwege siku ile; hata sisi hatukujui habari ya mchele ni nini alituelimisha kweli kweli habari ya mchele, dagaa wanaitwa mchele ambao ni lazima Serikali ibadilishe ili hili jambo liweze kwenda vizuri. Sasa Serikali imekubali jambo lenu, leo tena unakuja kivingine haya endelea.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Mheshimiwa Waziri mimi hayajanitosheleza na hayajaniridhisha kwa sababu hata wakati wa mazungumzo yake hapo kama mmemsikia Wabunge wenzangu anasema ndiyo maana tukazichoma nyavu halali. Sasa mimi niseme tu kwamba hao dagaa mchele anaosema sisi kwetu tunawaita uono, maumbile yao ni madogo, hata waishi miaka 50 wanakuwa maumbile yao ni hivyo hivyo. Sasa na hii kusema kwamba wamechoma nyavu halali; na nina majina hapa ya watu ambao nyavu zao zimechomwa mimi nataka kutoa hoja ili Wabunge wenzangu waniunge mkono

ili tulijadili jambo; kwa sababu pamoja na nyavu lakini zipo mashine zimeshikwa baada ya watu kusalimisha nyavu zao, je Serikali nao ni wapi mashine hizo yatawarudishia lini?...

**MWENYEKITI:** Inatakiwa *issue* iwe moja.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK**: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni hiyo hiyo.

**MWENYEKITI:** ... na i*ssue* yako ni ya nyavu, sasa utajadili mambo mangapi?

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo hiyo nyavu twende hiyo hiyo natoa hoja Wabunge wenzangu waniunge mkono ili tuijadili...

**MWENYEKITI:** ... hata hiyo ya nyavu, sasa wnajadili nini kwa mfano, wanajadili nini kwa mfano.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nyavu zimechomwa Mheshimiwa Waziri amesema...

**MWENYEKITI:** Ndiyo zimechomwa ameeleza..

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wamechoma nyavu halali kwenye majibu yake ya sasa hivi, nimemnukuu hivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mabarouk naomba hebu mkae kidogo. Habari ya kusema na kulaumu ni kitu cha kawaida lakini hebu kaa kwanza kidogo. Tuwe wakweli katika mambo yetu, kama hoja yako si hoja hailazimishi sana, mtu mzima ameeleza zilikamatwa wakazitunza kwa maana ya kwamba kanuni ikibadilika ikaruhusu lile zitatolewa; lakini walipozichunguza wamezikuta zina matatizo ikabidi wazichome; sasa unasema watu wajadili, wajadili nini?

Unasema una majina kwani kakataa kwamba hakuna nyavu zilizokamatwa? zilikamatwa za majina hayo ambayo huna pia, lakini walipokuja kuzichunguza wakakuta

zile nyavu, ametumia neno pambio, zina mapambio kibao, kwa hiyo zikachomwa ndiyo majibu ya Serikali, sasa unataka wajadili nini? Hebu kama utarudia tena, kijadiliwe kitu gani?

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uchunguzi wao haiwezekani nyavu zote zikawa na hayo mapambio haiwezekani...

**MWENYEKITI:** Sasa wewe ulikuweko huko?

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko karibu sana na wavuvi wangu na wengine wamekwenda na pia vilevile tulifikisha kilio chetu mpaka kwa Waziri Mkuu*...(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Basi tupe ushahidi kwamba..

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba hizi nyavu ziwekwe...

**MWENYEKITI:** Tupe tu ushahidi.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na wakaahidi kwamba hawatazichoma. Sasa mimi ambacho nashangaa, kwanza tuliahidiwa na yeye Waziri, tulikutana naye sisi Wabunge wa upande wa Pwani, akaahidi nyavu zile hazitachomwa. Na haiwezekani nyavu zote ziwe na mapambio, haiwezekani. Nyavu zingine wamezichoma bila huruma, nyavu mpya kabisa, nyavu moja takribani shilingi milioni 15. Leo wavuvi wale, Wabunge wenzangu ni mashahidi, familia za baadhi ya wavuvi inabidi tuzigharamie sisi Wabunge. Nyavu zingine zimechoma hali ya kuwa hazina mapambio*...(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Toa ushahidi kwamba kuna nyavu ushahidi wangu ni huu halafu Waziri anajibu.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa...

**MWENYEKITI:** Yeye kasema maelezo yake kakuta zina mapambio.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja tujadili.

**MWENYEKITI:** Nafikiri hakuna hoja hapo, tunaendelea...

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaaaaa!

**MWENYEKITI**: Nani anasema aaaa! Lazima pale na hoja, atoe ushahidi kwamba hicho kitu hakikuwa hivyo. Mheshimiwa Yussuf aliyekuruhusu useme nani? Usinitarai. Unapata maelezo si suala la ubishi tu wa kitoto, unapata maelezo wewe una maelezo yako tofauti njoo *contrary,* toa ushahidi. Maelezo ya Serikali tumeyasikia sisi wote au hatukusikia? wewe unasema maelezo haya si sahihi eleza ya kwako toa ushahidi kwamba ya kwako ndiyo sahihi halafu tuwabane hawa; kwamba una wavuvi wako ambao nyavu zao zilikuwa safi hazina shida zimechomwa; Sasa majina ndiyo ushahidi.

**MBUNGE FULANI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ushahidi nitakuja nao vipi ilhali nyavu zenyewe zimechomwa?

**MWENYEKITI**: Ndiyo hapo sasa hoja inakosa nguvu. Tunaendelea, Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Bunge ni kusimamia na kuishauri Serikali na kwa kiti chako ukiwa kama Spika Novemba 2017 uliunda Kamati maalumu ya kuchunguza na kushauri Serikali juu ya kuongeza mapato kutokana na uvuvi wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahari buu ina kilometa za mraba 223,000 sawa asilimia 14, lakini mapato yake kiujumla

kati ya trilioni 1.1 inaingiza milioni 200 kama ishina kitu; na Kamati yako ile mwaka jana Novemba Mei ilikabidhi ripoti kwa Seriakli ikiweka mapendekezo takribani 22 ambayo inaishauri Serikali mambo ya kiutendaji, sera, sharia na kanuni ili kuweza kuboresha na kuongeza mapato ya Serikali. Sasa ningeomba maelezo ya Serikali ni kwa kiwango gani mapendekezo na maoni yale ya Kamati yamechukuliwa katika bajeti hii ya 2019/2020 na yame-*reflect* ongezeko la mapato? Maelezo ya Serikali yasipojitosheleza nitaweza kutoa hoja tulijadili, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ufafanuzi Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani hatujamuelea vizuri ni hoja ipi inayozungumzia....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo, rudia tena kwa kifupi zaidi.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kunyanyua uchumi wa nchi na kama kazi ya Bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Kwa kupitia kiti chako uliunda Kamati maalum Novemba 2017 na ilifanya kazi kuanzia Januari 2018 na ripoti ikakabidhiwa Serikalini mwezi Mei 2018 ambayo ilikuwa inashauri masuala ya uvuvi wa Bahari Kuu yanaweza kuchangia kiasi gani mapato ya nchi hii. Mapendekezo yaliyotolewa ndani ya ile Kamati yalikuwa si chini ya 20 yakilenga kwenye utendaji, sera, sheria na kanuni ili tuweze kuongeza mapato yanayotokana na uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kimsingi ukiangalia kwenye takwimu ambazo zimetolewa kwenye hotuba ya bajeti ya Waziri, bahari kuu tuna umiliki wa kilometa za mraba 223,000 lakini tunachangia mapato kwa asilimia 14 ilhali Ziwa Victoria tuna kilometa elfu thelathini na tano na themanini na nane lakini tunachangia mapato kwa asilimia 63. Sasa kimsingi Kamati yako ambayo uliiunda kuishauri Serikali ilitoa

mapendekezo si chini ya 20; na mapendekezo hayo yalilenga kwenye kuongeza mapato na takwimu zilitolewa ndani ya ile ripoti. Sasa ningeomba Waziri atuambie ni kwa kiwango gani mapendekezo yale 22 ya Kamati yako yamechukuliwa na kufanyiwa kazi?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, umeeleweka Mheshimiwa, kama utakumbuka ni mambo gani yamechukuliwa yamefanyiwa kazi Mheshimiwa angependa kujua katika ushauri wa Bunge kwa Serikali.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yote ambayo yalipendekezwa na Kamati ya Bunge uliyoiunda kwa ajili ya kuangalia namna bora kuiwezesha nchi yetu kunufaika na uvuvi wa bahari kuu Serikali mapendekezo yote nayafanyia kazi. Zoezi hili niseme tu kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa yupo, kikao cha kwanza kimekaa cha mwisho kabisa na tumebakiza kikao kimoja tu kukamilisha ripoti ili tukuletee jinsi Serikali ilivyotekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini changamoto iliyokuwepo ni kwamba katika mapendekezo yaliyowekwa na hiyo Kamati mengine yalikuwa yanahitaji mpaka uchunguzi, kwa hiyo haikuwa rahisi kwa Serikali kupokea tu mapendekezo yale na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa Mheshimiwa Spika. Hata hivyo mpaka sasa hivi tuko hatua nzuri. Mengine mengi mnayoyaona na *speed* tunazokimbizana ndiyo hayo yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge tumesema kwa mfano *TAFICO*, baada ya kuiangalia ina mali ambazo za Dar es Salam peke yake ni bilioni 118, sasa mali zingine bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii kampuni inakopesheka na inaweza hata ikachukue yenyewe tu ikanunua baadhi ya meli hapa. Kwa hiyo kukimbizana kote huku kuandika *business plan* ni hayo hayo ambayo ulituelekeza. Kwamba kwa vyovyote vile Serikali lazima iingie. Kwa hiyo wakati sisi tunaandaa kuleta ripoti hiyo kwako

wakati huo huo tumetekeleza mambo mengi kupitia ripoti yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo nafikiri ni jibu jema, kwamba tusiibie mtihani tusubiri tu tutapata mrejesho rasmi kutoka Serikalini. Mheshimiwa Kitwana Dau.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la wkangu limeshakuwa *capture* na la Mheshimiwa Mbogo lilikuwa la Bahari Kuu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Nitaomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri husika juu ya hali tunayoiona ya uingizwaji wa bidhaa za mifugo na uvuvi nchini. Kwa mfano katika sekta tu ya mifugo tunatumia fedha nyingi za kigeni kuagiza nyama; na Mheshimiwa Waziri aliwahi kutoa taarifa kwamba tunazalisha tani takribani 2,000 kwa siku, na tani hizo hizo 2,000 ndizo zinazoagizwa. Vilevile kwa upande wa maziwa tunaagiza takribani lita milioni 13 ambazo zinagharimu takribani bilioni 17.9. Vilevile samaki tunauzalisha tuko *under capacity,* tunazalisha tu chini ya tani laki tatu na, na tunaagiza tena laki tatu na, za samaki hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hela nyingi sana za kigeni, ni matrilioni ya shilingi ambapo sasa tunanunua kwa dola, tunaotumia kuagiza *products* hizi za mifugo na uvuvi kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kupata ufafanuzi, kwamba Serikali ina mkakati upi wa kuzilea sekta hizi mbili ili kwamba tunachokizalisha tuwe tuna ki-*export,* tunakitoa nje, na badala yake tuna *under production* na tuna *import?* Je, ni suala la *under declaration* ya wafanyabiashara ama ni kweli tunachokitengeza au tunachokipata kutoka kwenye mifugo na uvuvi ni kidogo sana katika sekta hii kiasi kwamba inabidi sasa fedha za kigeni za nchi yetu zitoke nje

kuagiza bidha hizi? Nisiporidhika basi nitaomba Wajumbe tuchangia suala hili ili tuweze kutoka hapa.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi kuhusu jamo hilo, Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimefurahi sana kuulizwa swali hilo na Waziri Kivuli wa kutoka Kambi ya Upinzani. Swali ni zuri sana, na Mawaziri Kivuli kama hawa wa kuuliza maswali mazuri hao ni wazuri kwa sababu yanakuwa manufaa makubwa sana kwa taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nikubaliane naye; ni ukweli kabisa kwamba moja tuliua viwanda vya ndani sisi wenyewe kwa sababu mbalimbali. Kwanza viwanda tulivyokuwa navyo vya kuzalisha maziwa hapa nchini vilifungwa, viwanda tulivyokuwa navyo vya kuzalisha nyama na kuuza nje vilifungwa. Kwa hiyo hatimaye viwanda, uzalishaji wa samaki ndani ya nchi nao ulipungua kwa kiwango kikubwa sana kwa sababu mbalimbali ikiwemo hiyo ya uvuvi halafu ikapunguza sana uvuvi wetu wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo taifa likawa sasa halina samaki, ikawa ni lazima tuagize samaki kutoka nje, hayo mambo yalifanyika kwa utaratibu huo. Sasa leo tumefanyaje; kwa mfano kwa takwimu tulizonazo za sasa hivi uingizaji wa samaki kutoka nje ya nchi uliishia mwezi wa kumi, kutoka mwezi wa kumi mpaka leo hakuna hata kilo moja ya samaki iliyoingizwa hapa nchini. Hii ni kwa sababu samaki tunao wengi ndani ya nchi na bei zimeshuka sana. Ukienda sasa hivi kuuliza bei ya dagaa kwanza wapo wazuri na wananunuliwa kwa bei nzuri, samaki, sangara, sato na wale wa baharini wote wako vizuri na wanauzwa bei nzuri. Kwa hiyo sasa hivi hakuna Mtanzania ambaye anatamani tena samaki wa kutoka China wala nchi nyingine yoyote kwa sababu hiyo rasilimali tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge suala kama hili la samaki hawa tutakuwa tumefikia

hatua nzuri na kama kutoka Oktoba mpaka sasa hivi hawajaingiza tuko hatua nzuri. Kwa hiyo Serikali imechukua hatua ambazo kwanza zimewawezesha wananchi wenyewe wavuvi wa hapa nchini kupata soko kwa sababu ilifika mahala wavuvi wanavua wakifika pale soko la Feri au la Kirumba wanakuta kuna samaki wa kutoka nje, wanarudi na samaki wao au mpaka wanaharibikiwa na samaki wao. Leo mvuvi akitoka kuvua anauza anapata pesa kwa sababu hakuna tena mchezo huo wa kupata samaki wa kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu viwanda vya nyama, Mheshimiwa Dkt. Sware kama tulivyozungumza, kwamba viwanda vya kuuza nyama nje ya nchi vyote vili-*collapse* kutokana na ushindani ambao haukuwa sawa. Kama nilivyosema maziwa yanaingia ndani ya nchi hayajalipa kodi, hayana vibali hayana kila kitu halafu yanakuja kushindana na viwanda hapa, viwanda vilikuwafa; vya nyama navyo ni hivyo hivyo. Leo viwanda tulivyonavyo vya kuzalisha maziwa, baada ya udhibiti huu tulioufanya; na ndiyo maana unaona wana furaha kubwa; wakizalisha leo; kuna kiwanda kinaitwa Galax cha Arusha kimeanzishwa sasa hivi kwa siku wakizalisha lita 5,000 zinanunuliwa zote siku hiyo hiyo. Ukienda *Tanga Fresh* siku hiyo hiyo ya uzalishaji maziwa yote yananunuliwa siku hiyo hiyo, Azam nao hivyo hivyo, hakuna mwenye *stock* kutokana na hatua nzuri za Serikali za Serikali ya Awamu ya Tano inazozichukua juu ya wafanyabiashara hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa viwanda vya nyama vimeibuka na vyenyewe vingi kama nilivyovitaja *TanChoice*, Eliya, na maeneo yote yale; na hiki cha Misri kinachojengwa ambacho kitakuwa ni kikubwa sana, kama tulivyokielezea, sitaki kurudia. Hivi viwanda vyote, na hivi viwili vinafunguliwa vinafunguliwa Septemba tu, *TanChoice* na Eliya zina funguliwa Septemba, vitaanza kuuza mazao haya ya mifugo kwenda nje kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama Serikali ya Awamu ya Tano imeshalitekeleza hilo tupeni muda tu kwa

sababu haya mambo si ya siku moja unaweza kuyafanya yakakamilika, ni hatua.

**MWENYEKIT:** Mheshimiwa Sware amekubaliana na wewe, kwa hiyo, bado nakupa muda kama una la kusema.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa sababu suala hili ni nyeti sana tunasema tunataka kujenga uchumi wa viwanda na rasilimali zinazotoka kwa ajili ya hivi viwanda ni sekta hii ambayo imebeba Watanzania wengi ili tuweze kuvuka hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa amegusia samaki japokuwa bado, tunatakiwa tuzalishe angalau kwenye maji tu ya ndani ya baharini tani 600,000 mpaka 700,000, bado tunazalisha chini ya hapo, tani 300,000; kwa hiyo bado kuna *demand;* na hatujagusa Bahati Kuu kabisa hilo ni suala linguine. Kwenye suala kwenye *product* za mifugo hali ni ile ile, nyama bado hali ni ile ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nitoe hoja ili tuchangie ili tuweze tu kutoka hapa na Mheshimiwa Waziri apate mawazo ya wajumbe na kupata *way forward.* Kwa sababu hata suala la ngozi inatugharimu takribani Dola za Kimarekani milioni 51 kuagiza *product* za ngozi ilhali sisi kwa Afrika ni nchi ya tatu kuwa na mifugo, *especially* hii ya ng'ombe; sasa haviendani idadi ya ng'ombe na *products* na bado tunaagiza kutoka nje. Kwa hiyo suala hili ni nyeti sana ili liweze kutuvusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa umeongea mengi sasa kijadiliwe kitu gani katika hayo iliyoongea, kimoja maana yake *issue* ni moja, ambayo unadhani ni vizuri sasa hiyo ndiyo rudia tena.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatokaje au tunaboreshaji kwamba *export* iwe kubwa na *importation* iwe ndogo. *(Makofi)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Haya mnaojadili msije na lawama, suala zima ni tunatokaje hapa, ndiyo *issue* ambayo nimeiona, ndiyo, niandike, Katibu kote kote, wanatosha inatosha hiyo orodha kubwa sana; na Mheshimiwa Keissy pia nimemuona. Tuanze na Komu, dakika mbili mbili, mbili na nusu, chap chap, tunatokaje hapo, hoja ya Mheshimiwa Semesi. *(Makofi)*

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nimesimama kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Sware kwa sababu ni kweli kwamba kuna tatizo kubwa sana, hata ukisoma vitabu vyao na kitabu cha Kamati unaona kabisa kwamba wanakiri kuna tatizo. Sasa naomba namna ya kutoka hapa ni lazima Serikali ituambie kwa mfano *implementation* ya ile kitu kinachoitwa *Blue print.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumza hapa na Waheshimiwa wengi sana wamezungumza, tukichukua *item* moja tu ya maziwa, tunazalisha maziwa bilioni 2.4, tuna *process* maziwa lita 37,000 tu, lakini ukiangalia ni kwa nini ni tatizo ambalo liko kwenye Serikali kwa sababu ya zile *Regulatory Authorities* kwa sababu ya tozo na kodi. Sasa hayo ni mambo ambayo Serikali inapaswa ituambie ni kwa nini maana yapo ndani ya uwezo wao, ni kwa nini wasiyamalize sasa hivi ili tukatoka hapa mahali, tukaacha hii fedheha. Leo tunajivuna kwamba bajeti yetu labda tunatoa tiba bure kwa watu wa *TB* lakini kwa sababu hatusindiki maziwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Komu. Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Suala la *Forex* ni jambo la muhimu sana, ndio

linatupa nguvu kama Taifa kuwa na misuli ya kununua vitu vya muhimu kama madawa na vitu vya elimu. Ukiangalia kwa mfano hata masuala ya dagaa, sisi kama nchi tuki-*export* kuna ushuru ambao amezungumza Mheshimiwa Waziri wa 0.16 dola kupeleka kwenye soko *East Africa,* wakati wenzetu wanaotuzunguka hawana huo ushuru. Kwa hiyo utakuta wale wanaotuzunguka katika nchi za Maziwa Makuu wanakuwa na uwezo wa ku- *export* zaidi, wanapata faida zaidi, wanaweza wakauza kuliko sisi tunavyoweza kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo huu ushuru ambao umewekwa unasababisha watu washindwe kufanya biashara. Kwa hiyo naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Dkt. Sware kwamba vitu kama hivi vinatufanya tusiwe na nguvu ya ushindani kibiashara kwa sababu tunajikwaza sisi wenyewe, kwa hiyo, ningeomba hii hoja ya Mheshimiwa Dkt. Sware ichukuliwe kwa uzito wake tuwe na misuli ya kuingiza dola zaidi ndani ya nchi kuliko kutoa tunapo-*import* vitu kutoka nje. Kwa hiyo hiyo hoja ndio naiunga mkono na ningeomba Waheshimiwa Wabunge wote tuiangalie kwa mapana yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante san. Mheshimiwa Anatropia huko huko unakopiga *story*.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru. Changamoto tunayoiona hapa, sisi tunataka kumkamua ng'ombe bila kumshibisha na tunasahau kwamba ng'ombe ukimkamua zaidi bila kumlisha chakula, mwisho utakamua damu. Mfano mdogo, Kamati wametoa taarifa ya *export loyalty* inayotozwa kwa wafanyabiashara wa Kanda ya Ziwa ambao wanasafirisha kayambo ambao ni samaki wa maji chumvi, wanasema kwa tani moja ambayo ni kilo 1000 wanalipa hiyo *export levy* ya 1,149, 5000 *point something* kwa tani moja, hivi ni mfanyabiashara gani yuko tayari kuendelea na biashara ya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunadhani tunakusanya kwa kutaka huyo ng'ombe aendelee kukamuliwa maziwa

yawe mengi, tunasahau kwamba tunavyopunguza au kuondoa hiyo tutapata wafanyabiashara wengi, tunauza leseni, tutapata kodi na tuta-*gain* zaidi. Hiyo ndio hoja yangu katika hilo, lazima tuiangalie. Tukitaka kupata zaidi Mheshimiwa Rais aliyemaliza muda wake alisema, ukitaka kula ni lazima na wewe ukubali kuliwa. Hivyo, ni lazima tupunguze ili tupate zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ukitaka kula, uliwe kidogo. Mheshimiwa Munde.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niungane mkono na Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri ametuambia wakati Serikali ya Awamu ya Tano inaingia madarakani viwanda vyote vilikuwa vimekufa vya nyama na vya maziwa, kwa hiyo wao wameanza na kazi kubwa ya kufufua viwanda hivi, lakini Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wanafanya kuboresha ametueleza, kuanzia Oktoba mpaka sasa hakuna samaki yeyote wa nje ya nchi walioingia ndani. Hii ni kazi kubwa sana nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hatua hii aliyofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili sio la siku moja, ni suala linataka muda, tuipe muda Wizara ifanye kazi vizuri, itufikishe kwenye malengo yake aliyotuambia hapa Mheshimiwa Waziri. Vilevile tukumbuke hili ni suala mtambuka, kuna *TRA*, Kilimo, Fedha na mambo chungu mzima, tusimwangalie tu Mheshimiwa Mpina kama Mpina ndiye yeye peke yake anaweza kuwa bila Waziri wa Viwanda, *TRA*, *TFDA*, mpaka kuja kukamilisha kiwanda, sio yeye peke yake, ni suala mtambuka. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge aiachie Serikali sasa ijipange, iboreshe ili kuja kuweka viwanda na ili tuweze ku- *export* tupate fedha nyingi za nje. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri kaeleza vizuri, sisi wenyewe

tuliua viwanda tuko humu humu na wengine labda walikuwa Mameneja kama Mheshimiwa Komu anafahamu. Tuliua viwanda vya nyama, viwanda vya maziwa na kila kitu, hakuna mtu anapenda kuagiza nyama kutoka nje, samaki kutoka nje, kusema kweli ni makosa, tunategemea nchi yetu sisi kuuza nyama nje, kuuza samaki nje. Mheshimiwa Waziri kazungumza ukweli kwamba viwanda tunafufua kwa sasa, tumpe muda anafufua viwanda vyote vya nyama na kila kitu ili tutosheleze nchi yetu na tuuze nje. Tumpe muda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nafikiri hata Mheshimiwa Waziri sijui hana haja ya kuongea katika hili zaidi ya kumrudishia mtoa hoja kwa sababu wote mnaongelea kitu kinachofanana, tunatoa mawazo mazuri sana kwa Serikali ya namna gani ya kwenda mbele kutokana na hali hiyo ambayo mmeileza ambayo wote tunakubaliana. Serikali ya Awamu ya Tano inasema kwamba hali hii mbaya sote ni mashahidi ndio iliyokuwepo, sasa tunapambana kutoka hapo kwenda kwenye hali bora zaidi na kaeleza baadhi ya *measures* ya viwanda ambavyo sasa vinajengwa hivyo vya nyama na kadhalika, jinsi akina *ASAS*, akina *Tanga Fresh* ambapo wanatengeneza mpaka *long life milk* na kadhalika. Tunategemea hata sisi Dodoma tupate viwanda vya maziwa na *program* za maziwa hapa ili wananchi wetu, huko ndiko mwelekeo ulipo.

Kwa hiyo wazo la Mheshimiwa Semesi lilikuwa ni wazo zuri na hili sio tu kwa mifugo, tulipojadili kilimo ilikuwa ni hayo, tulipojadili sijui nini huko hizi sekta za uchumi za uzalishaji ilikuwa ni mambo hayo kwamba hawa akina *TRA*, sijui *TBS,* nani *TFDA*, sijui *OSHA*, sijui *NEMC* sijui nani yaani imekuwa inajirudia, kila ukiangalia mjadala wetu una-*hinge* hapo hapo.

Ujumbe wetu kwa Serikali ni hapo kwamba haya makundi haya kwa kweli yamekuwa ni *anti* maendeleo, tuangalie *AG* atuletee hapa na Serikali, tufumue hizi sheria ambazo zinatuletea matatizo ya kutowezesha huku ndani kuweza kubadilika na kusonga mbele kabisa.

Mheshimiwa Sware tufungie, hoja yako imekubalika na Bunge zima kwa kweli. *(Makofi)*

**MHE. DKT. IMMACULATA S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi. Nakubaliana kwamba hoja hii ni muhimu kama wajumbe wenzangu walivyoiunga mkono na nafikiri Serikali imechukua na nafikiri ni wakati muafaka kujiwekea *time frame* kwa sababu hata ukiangalia *trend* ya thamani ya mauzo tu katika Sekta ya Uvuvi kwa kipindi tu cha miaka minne imetoka kwenye dola za Kimarekani milioni 800, mpaka 250, hiyo hali haiko sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nafikiri tunavyopitisha bajeti hii ni vizuri Serikali kupitia Wizara hii ikajipanga upya na kujiwekea *time frame* na mikakati madhubuti ya kututoa hapa tulipo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana na Mheshimiwa Waziri Kivuli uwe karibu nao kwa mawazo. Muda unasemaje?

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:** Bado dakika mbili.

**MWENYEKITI:** Bado dakika mbili, sawa, angalau basi Mheshimiwa Saada, dakika mbili zimebaki jitahidi utumie moja.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sehemu ya uvuvi wa bahari kuu ndio sehemu ambapo Muungano wetu unapo-*converge* vizuri na katika kutekeleza hii Serikali imeunda hiyo *Deep Sea Fishing Authority* ambayo inafanya kazi pamoja na mambo mengine ku-*manage* uvuvi wa bahari kuu. Kuanzia mwaka 2019, Mamlaka hii ambayo inategemea sana mapato yake kutokana na leseni zinazovuliwa, yaani leseni zinazoombwa kwa ajili ya kuvua sasa zimekuwa zero na mapato ya Mamlaka hii yameshuka *tremendously.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri kweli alikuwa anazungumza kutoka

moyoni kabisa mambo ambayo yanahitajika kufanya, lakini kubwa ni pale ambapo tulipokuwa tunatoza mrabaha wa ile wa samaki jodari ambao unavuliwa. Sasa nataka tu *commitment* ya Mheshimiwa Waziri lini tuta-*review* hii tozo ambayo imekuwa ni kikwazo kikubwa kwa Mamlaka kujiendesha na kwa maana hiyo inakosesha mapato Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mamlaka yenyewe itashindwa kujiendesha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saada bahati mbaya hili lilikwishaulizwa na Mheshimiwa Mattar kule na limetolewa majibu na naamini kwa msisitizo wako pia Serikali imesikia. Kwa hiyo tuchukulie kwamba Serikali imesikia na itafanyia kazi kwa hakika na kwa kuwa muda wetu sasa kama mnavyojua mwezi Mtukufu huu, muda hauko upande wetu, sasa nikamkaribishe Katibu tuendelee na utaratibu wa *guillotine*.

**Fungu 99 – Mifugo**

Kif. 1001- *Administration and Human Resources Management Division*……..……Sh.2,735,467,800
Kif. 1002 – *Finance and Account Unit* …………Sh.1,247,862,112
Kif. 1003 – *Policy and Planning Unit*……………Sh.1,380,043,860
Kif. 1004 – *Research, Training and Extension Unit*...................................…...Sh.8,267,625,500
Kif. 1005 – *Information, Education and Communication Unit*…………..………Sh.354,780,000
Kif. 1007 - *Internal Audit Unit*………………………Sh.329,918,000
Kif. 1008 - *Procurement Management Unit*……Sh.466,195,400
Kif. 1009 – *Legal Services Unit* ……………………Sh.215,788,000
Kif. 1010 – *Information and Communication Technology Unit*...................................…Sh.233,892,000
Kif. 1011 – *Environment Management Unit*…Sh.15,472,162,672
Kif. 7001 – *Veterinary Services* …………………..Sh.8,615,234,489
Kif. 7005 – *Veterinary Council of Tanzania*………Sh.466,077,386
Kif. 8001 – *Livestock production and Marketing*........................................Sh.2,841,676,300
Kif. 8002 – *Grazing Land and Animal Feed Resources Development*.................Sh.1,044,717,153

Kif. 8003 – *Animal Breeders Rights Unit*……………..Sh.334,510,000
Kif. 9001 – *Fisheries Development Division*……...…………Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 64 – Uvuvi**

Kif. 1001- *Administration & Human Resources Management Division*…..Sh.1,091,743,110
Kif. 1002 – *Finance and Account Unit*……………..Sh.415,128,081
Kif. 1003 – *Policy and Planning Division*………..…Sh.740,501,640
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit*……………………..…Sh.262,072,410
Kif. 1005 – *Legal Unit* ……………......……………...Sh.153,634,940
Kif. 1006 – *Procurement Management Unit*…..…Sh.313,666,611
Kif. 1007 – *ICT Unit*……………….............……..…..Sh.241,014,000
Kif. 1008 – *Fisheries Laboratory* …………………Sh.269,300,000
Kif. 1009 – *Environment Management Unit*…….Sh.136,940,000
Kif. 9001 – *Fisheries Development Division*……..Sh.4,203,762,390
Kif. 9002 – *Aquaculture Development*…………Sh.2,190,428,930
Kif. 9003 – *Fisheries Aquaculture Research and Training Ext. Services*…….........…..Sh.8,414,268,888

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 64 – Uvuvi**

Kif. 1003 – *Policy and Planning Division* …………Sh.499,460,000
Kif. 9001 – *Fisheries Development Division*……Sh.12,255,787,551

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 99 – Mifugo**

Kif. 1003 – *Policy and Planning Unit*……………..Sh.140,000,000
Kif. 1004 - *Research, Training and Expenditure Unit*…..............................Sh.200,000,000
Kif. 7001 – *Veterinary Services*……....………...Sh.1,000,000,000
Kif. 8001 – *Livestock Production and Marketing*...................................Sh.1,180,000,000
Kif. 8002 – *Grazing Land and Animal Feed Resources Development*…......………Sh.480,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mheshimiwa Waziri taarifa, tafadhali. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2019/ 2020 Mafungu kwa Mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote, hivyo basi naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa hatua hii kama kanuni zinavyotutaka napaswa nilihoji Bunge kuhusiana na hoja ambayo Mheshimiwa Waziri ameitoa ili muweze kuiamua na hoja yenyewe ni kwamba sasa Bunge likubali kupitisha Makadiro ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

*(Hoja ilitolewa na iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Naomba niseme kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge wote nawashukuruni sana kwa michango yenu ya siku hizi mbili, imekuwa ni michango ya kujienga sana Wizara hii Wizara muhimu sana katika maisha ya watu wetu, inayowagusa watu wengi sana wafugaji, wakiwemo wapiga kura wetu wengi sana na wavuvi, wakiwemo wapiga kura wetu wengi sana katika makundi hayo. Kwa hiyo tukupongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, timu yote kabisa ya Wakurugenzi kwa kazi nzuri sana ambayo mmekuwa mkiifanya. Eneo hili lina changamoto nyingi sana, pande zote mbili upande wa mifugo na upande wa uvuvi na ulipoanza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri mmezikuta changamoto hizi kilio kilikuwa kikubwa sana. *(Makofi)*

Bunge lililopita wale mliokuwepo mnakumbuka tulivyokuwa tunalipuka wengine kama petroli mambo ya wakulima na wafugaji Kiteto na Kongwa huko kadhalika watu walikuwa wanachinjwa utafikiri tuko Somalia na kadhalika, mahali pengi mlikuwa mnasikia matatizo makubwa Kilosa, sijui Mvomero huko na mahali pengine pengi, ilikuwa ni tatizo kubwa, lakini sasa hivi kwa kiasi kikubwa Serikali ya Awamu ya Tano imejitahidi sana. *(Makofi)*

Hali ilikuwa mbaya sana ilikuwa mbaya mno, ilikuwa ni ngumu sana, baadhi ya watu walikuwa wanachinjwa ulikuwa huwezi kuangalia mara mbili, mpaka watoto wadogo mpaka kina mama. Unakuta ng'ombe kadhaa 50,100 wamekatwa ng'ombe wamekatwa miguu wako wamelala chini wamekatwa, unakuta ng'ombe wametiliwa sumu 200 au zaidi wamelala chini ng'ombe hawana hatia unawawekea sumu ya nini. Palikuwa na ukatili wa kila aina, jamani tumesahau mambo haya ilikuwa juzi tu. Kwa hiyo

Serikali imejitahidi mno, Mheshimiwa Waziri tunakupongezeni sana.

Pia ile rula ile jamani kwani mmeishikia tena kwani mwaka jana si tulikuwa tunagombana shauri ya rula tu angalau rula nayo kidogo na kwa kweli mengi ambayo tuliyapendekeza yale ya nyavu sijui milimita ngapi wamekiri wamerekebisha, tulipendekeza tu sijui kitu gani wamerekebisha, sijui kitu gani wamerekebisha. Sasa mwendo huu ndio mwendo mzuri kwa sababu ni watu kwa kweli wasikivu kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Pia na sisi Watanzania wakati tunaiambia Serikali ipunguze iangalie mambo, kuna umuhimu sana wa kuangalia masuala ya kodi kwa kweli umuhimu huo ni mkubwa kabisa kwa kuangalia mambo ya kodi, lakini bado *base line* ni kwamba Watanzania lazima tulipe kodi, kwa hiyo ni kuangalia kuchekecha hapa na pale namna gani inaweza ikawa wapi ambako ni uwanja ambao bado haukusanyi kodi vizuri, pale ambapo kodi imezidi sana inaumiza wafanyabiashara, sio kwenye mifugo tu na uvuvi peke yake lakini *across* na haya mambo ni mchakato vilevile, kwa hiyo Wizara ya Fedha wanahusika, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo, Wizara ya TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu kadhalika.

Sisi tunaiomba Serikali iendelee iangalie haya mambo kwa upana wake na kulinganisha na majirani pia, tusiwe tunakuwa na kodi ambazo nazo ni *anti* maendeleo nalo ni tatizo lakini lazima pia tulipe kodi hii lazima ieleweke kwa Watanzania, iendelee kuwa sasa ndio *culture* yetu kulipa kodi, tena kulipa kwa hiari, sisi wenyewe na kwa wakati. *(Makofi)*

Kwa hiyo msifunjike moyo kabisa Mheshimiwa Waziri, mnachapa kazi vizuri na nasema msivunjike moyo katika mambo haya hamko peke yenu mnaolaumiwa hamko peke yenu, sisi wenzenu vilevile ni madongo kila kukicha, unakaa unafikiri wakati mwingine unasononeka kweli. Wakati mwingine hata miongoni mwa Wabunge humu kwenye *canteen* wapi kusengenyana kufanya hivi, hakuna mtu

anaweza akaonea mtu, mkiona kuna jambo ndugu zangu kuna tatizo, tena tatizo kubwa na matatizo ukiwa kiongozi lazima upambane, sasa unafanyaje. *(Makofi)*

Kwa hiyo tuelewane Waheshimiwa Wabunge, hatuwezi kuendesha nchi hii kwa njama njama, ujanja ujanja, kupaka watu matope, kufanya hivi, lazima tuwe ni watu wa ukweli tusimamie ukweli ulipo, tuwe watu wa ukweli tu itatusaidia tutafika mbali, lakini hii, eeeh hatuwezi kufika, hatuwezi kutengeneza magenge ya umoja katika maovu, hakuna Taifa la aina hiyo hakuna. Kwa hiyo mtasoma siku hizi, watu ni wa mitandao, mtasoma Ndugai hivi na nini, haiko hivyo hata siku moja, ni kwa sababu huyo Ndugai hayuko kwenye hiyo mitandao, kujibu hoja kwa hoja kila wakati kwa kila jambo, ndio maana.

Kwa hiyo wanasema, wanarudia wao wenyewe, wanapaka wanavyotaka, wanatukana wanavyotaka, wanafanya hivyo wanavyotaka na wewe ukiwa mwepesi basi kila unachosoma unakiamini, hii ndio hivi wakati sio hivyo na sisi tuko pamoja hapa, kama kuna jambo si unauliza tu, bwana kuna hili naona linasemwa ni vipi, unapata maelezo ya kutosha. *(Makofi)*

Sasa kuna lingine ambalo wanalipotosha hivi sasa ninavyoongea kwa madhumuni ambayo nayajua vizuri na wamekuwa wakifanya hivyo kwamba sijui Mheshimiwa Ndugai amesema sijui Profesa Asad ameingia mikataba gani na Sweden bila yeye kupewa taarifa, kwa hiyo, wanasema sijui madudu gani, inazunguka sana. Ni mambo ya kijinga, ya kipuuzi tu, ya kijinga tu, ya kipumbavu, si tulishamaliza hapa, tunasonga mbele, leo tuko Mifugo na Uvuvi, tunaendelea na mambo mengine, wao wako kwenye mambo ambayo sisi hatuko huko sisi, tulikwishavuka.

Tulieleza *what was the business* na tulimaliza, kwa maana ya Bunge, tulimaliza, sasa hizo hoja nyingine ni za nini sasa, kuna nini tena cha kurudi nyuma, hatuna cha kurudi nyuma, hatuna cha nini, tunasonga mbele na shughuli zetu kama kawaida, hatuna ugomvi na mtu, tunasonga mbele.

Baada ya maelezo hayo, naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 23 Mei, 2019, Saa Tatu Asubuhi)*